NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

### Kikao cha Nne – Tarehe 7 Septemba, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG.YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**MWENYEKITI:** Hati za kuwasilishwa mezani Waziri wa Katiba na Sheria .

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**
Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa mwaka 2018 *(The written Laws Miscellaneous Amendments (No.2), Bill, 2018).*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho

ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2018 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2018).*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana sasa namkaribisha Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Katiba na Sheria, karibu Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill, 2018).*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mtolea kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Katibu tuendelee.

**NDG.YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali yetu tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini aulize swali lake.

Na. 40

**Ujenzi wa Vituo Vya Afya Kila Kata**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Kutokana na sera ya Serikali kujenga vituo vya afya kila kata.

Je, ni lini Serikali itajenga vituo hivyo katika Kata za Maretadu, Maghangw, Endamilay, Dinamu, Geterer,

Masieda na kupandisha hadhi Zahanati ya Hayderer kuwa Kituo cha Afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imejenga vituo vya afya 210 nchi nzima kwa gharama ya shilingi bilioni 93.5 vikiwemo vituo vya afya saba vilivyoko Mkoa wa Manyara kwa gharama ya shilingi bilioni 3.1ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ilipewa shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Dongobeshi na Halmashauri ya Miji Mbulu ilipewa shilingi bilioni moja kwa ujenzi wa Vituo vya Afya vya Tlawi na Daudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutimiza azma ya kuwa na kituo cha afya kila kata hapa nchini Serikali imeweka vigezo maalum juu ya ujenzi wa vituo vya afya, lengo mahsusi ni kusogeza huduma za afya ili zipatikane ndani ya umbali wa kilometa tano kama ilivyoelekeza kwenye Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupandishwa hadhi kwa Zahanati ya Hayderer kuwa kituo cha afya miundombinu iliyopo katika zahanati hiyo haikidhi vigezo vya kuhuishwa kutoa huduma kama kituo cha afya. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu imeendelea kufanya uhamasishaji kwa wananchi kujitolea kujenga vituo vya afya katika kata zilizotajwa za Maretadu, Maghangw, Endamilay, Dinamu, Geterer na Masieda. Hadi sasa wananchi wa Maretadu wametenga eneo lenye ukubwa wa ekari 10 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika kata hiyo .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaunga mkono nguvu za wananchi katika ujenzi kulingana na upatikanaji wa fedha na rasilimali nyingine kama watumishi na vifaa tiba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massay kama una swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana pamoja na majibu haya ya Serikali Jimbo la Mbulu Vijijini lina Kata 18 na tuna kituo kimoja tu cha afya na kama alivyosema kwamba tumetenga maeneo na wananchi wameshakusanya *material* yaani mchanga, simenti na wengine tumeanza kujenga, je, Serikali itaongeza nini katika jitihada hizi za wananchi ambao wenyewe wameamua kujenga vituo vya afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa wamekiri kwamba Zahanati ya Hayderer miundombinu yake haifai ili zahanati ile ikahuishwe ikawa kituo cha afya, je, uko tayari sasa kuja pale ili kuangalia namna gani na kutusaidia ili tukapata walau kituo cha pili katika Jimbo la Mbulu Vijijini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika majibu yangu ya msingi tunakubaliana kabisa na jithada zinazofanywa na wananchi katika kujiletea maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vya afya kama kazi nzuri ambayo imeanzishwa na wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Flatei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Flatei Massay jinsi ambavyo amekuwa akipigania wananchi wake kuhusiana na suala zima la afya, na sisi Serikali kwa kuunga mkono ndio maana katika hospitali 67 za Wilaya ambazo zinajengwa na wao ni wanufaika. Naomba nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwa kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu na hasa kwa wananchi ambao tayari wameonesha jitihada zao katika kujenga vituo vya afya na zahanati sisi kama Serikali tutakuwa tayari kwenda kushirikiana na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini juu ya utayari wangu hata kabla yeye hajasema anajua kwamba mimi niko tayari kwenda kule kwake ili tuende tukaone kitu gani kiko *site* tuweze kushauri namna bora ya kuweza kupeleka huduma kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Paresso kwa niaba ya Mheshimiwa Maryam.

Na. 41

**Wanufaika wa Mradi wa TASAF - Pemba na Unguja**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. MARYAM SALUM MSABAHA)** aliuliza:-

Mradi wa *TASAF* ni mradi wa kusaidia kaya maskini nchini.

Je, ni wananchi wangapi ambao wananufaika na mradi huo katika Visiwa vya Pemba na Unguja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ulianza rasmi januari 2013. Mpango huu ni wa miaka 10 iliyogawanyika katika vipindi viwili vya miaka mitano mitano na unatekelezwa hadi 2023 katika Halmashauri zote Tanzania Bara na Zanzibar. Jumla ya kaya maskini milioni 1.1 zenye jumla ya watu takribani milioni tano zimeandikishwa katika jumla ya vijiji, mitaa na shehia 9.986.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar, Unguja na Pemba kaya zilizonufaika na mpango huu kwa kupatiwa ruzuku na ajira kwa kushiriki kwenye kazi katika miradi ya kutoa ajira ya muda mfupi na vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza kwa lengo la kukuza uchumi wa kaya ni 32,262 kutoka katika shehia 168. kati ya idadi hiyo kaya 18,092 ni kutoka Unguja na kaya 14,164 ni kutoka pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya shilingi bilioni 32 zimetumika tangu mpango uanze kama ifuatavyo:-

- Miradi ya kutoa ajira za muda shilingi 7,240,498,800;

- Ruzuku kwa masharti ya elimu na afya ni shilingi 25,24,002,721; na

- Vikundi vya kukuza uchumi wa kaya zilizotolewa ni shilingi 464,000,000.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, fedha hizi za *TASAF* tunafahamu ni mkopo kutoka *World Bank* na fedha hizi zimekuwa zikitolewa kwa kaya maskini na fedha hizi hazijawahi kuonesha matokeo ya moja kwa moja kwa wale wananchi wanaopewa. Je, Serikali sasa iko tayari kufanya uchunguzi wa kina na tathimini na kuleta taarifa hapa Bungeni yenye kuonesha matokeo ya moja kwa moja kwa kaya hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni ukweli usiopingika kwamba fedha hizi za *TASAF* zimekuwa zikitolewa kisiasa kwa wana CCM na fedha hizi wakati panapotokea chaguzi ndogo zimekuwa zikitumika sana kushawishi kama sehemu ya rushwa kwa wana CCM ili CCM iweze kuchaguliwa. Nini kauli ya Serikali ikizingatia kwamba fedha hizi ni mkopo na zitarudishwa na Watanzania wote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi naomba nianze kumpongeza muuliza swali Mheshimiwa Msabaha kwa swali lake zuri, lakini pia nataka niwapongeze walengwa wa *TASAF* Unguja na Pemba. Katika nchi yetu mikoa inayoongoza kwa kufanya vizuri miradi ya *TASAF* ni mikoa ya Unguja na Pemba na kwa maana hiyo nataka nimpongeze Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed anayesimamia *TASAF* kule Pemba na Zanzibar ambaye anamsaidia Makamu wa Rais ambaye ndio Waziri mwenye dhamana ya *TASAF* Zanzibar. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo naomba nitoe majibu ya maswali niliyoulizwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba *TASAF* haijaonesha matokeo; mimi ninanomba tusichanganye mambo, hoja kwamba mnaomba taarifa ya utekelezaji wa *TASAF* ikoje ni hoja ya msingi na inaweza ikaletwa. Mheshimiwa Mao Tse Tung anasema *no research no right to speak. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndio Waziri wa *TASAF* na juzi nimetoka Kilimanjaro nimeona jinsi walengwa kule na wengi ni wakina mama walivyopambana na umaskini kwa kutumia *TASAF* wameanza biashara ndogo ndogo mwingine amenunua ng'ombe, wengine wamejenga majumba mimi ninamuomba ndugu yangu, ng'ombe ananunuliwa baada ya kudunduliza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba muuliza swali akubali ombi lake la mwanzo kwamba tupewa taarifa ya utekelezaji wa *TASAF* lakini kwa uhakika Kamati husika ya Bunge inapewa taarifa ya utekelezaji wa *TASAF* kila baada ya muda. Mheshimiwa Spika akisema taarifa ya *TASAF* anataka ailete humu ndani italetwa pasipo na mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kwamba zinatolewa kisiasa, zinatumika chaguzi ndogo ndogo nini kauli ya Serikali jamaa zangu ndio yale niliyosema jambo hujalifanyaia utafiti usiliseme. Walengwa wote wa *TASAF* wanapendekezwa na wana vijiji wenyewe, wana vijiji wanaambiwa andika jina la mtu unayemuona kijijini kwako hapo anastahili kupata msaada wa *TASAF,* wakishafanyiwa hivyo sasa ndiyo Watendaji wa *TASAF* wanazunguka kwenda kuthibitisha kwamba je, huyu yuko na katika kuthibitisha hivyo wengine tumewafuta kwa kuona hawastahili kupata.

Mimi nataka niwaambieni hakuna mtu anayechanganya siasa katika *TASAF* wala hakuna ushahidi kwamba hela ya *TASAF* inatumika katika uchaguzi, mimi ningeweze kumuomba Spika kwamba Mheshimiwa athibitishe kauli yake, tusifike huko mimi nimekusamehe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Mwanne Mchemba na Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwanza mimi nikiri kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI na kwamba Kamati ilikwishafanya ziara mara kadhaa kwa ajili ya kukagua miradi ya *TASAF* na nikiri kwamba kuna maeneo ambayo *TASAF* inafanya vizuri tulitembelea Maswa pale tukakuta mama mmoja amejenga kajumba kake kwa njia hiyo vizuri, lakini sasa ni ukweli pia kwamba fedha hizi zinagawanywa kibaguzi na katika ziara tulielezwa na hofu inakuja jana tumemsikia Mheshimiwa Rais anasema ukiwa na chakula chako unawapa kwanza watoto wako halafu ndio unawapa jirani.

Sasa mimi naiomba Serikali isipuuze hili suala la ubaguzi kwa sababu litagawa nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini uliza swali basi.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara iko tayari kubeba hili dukuduku, haya mashaka na kuyafanyia kazi kwa ajili ya mtengamano wa nchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachompenda Mheshimiwa Selasini ni mtu mkweli, maana utangulizi wake amesema maeneo mengine *TASAF* wanafanya vizuri, mimi nampongeza kwa kuwa mkweli, lakini tulivyo sisi binadamu katika matarajio ya utendaji hawaweze watoto wote 100 wakafanya vizuri kama unavyotaka wewe. Mimi kama Waziri mwenye dhamana ya *TASAF* nakubali rai yake kwamba yale maeneo yenye malalamiko niyafanyie kazi na kwa uzoefu wangu mnavyo nifahamu hili jambo tutaliweka vizuri na naomba Mbunge yeyote ambaye ana ushahidi kwamba mahala fulani hizi pesa zinafanyika kwa upendeleo mimi nitalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanne.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kuuliza swali dogo. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini kwa kuwa huu sio mchango ni maswali ya nyongeza mimi naomba niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *TASAF* inafanya kazi nzuri sana hapa nchini na kwa kuwa *TASAF* imefanya kazi maeneo mengi sana hapa nchini kama vile upande wa afya, elimu sasa hivi *TASAF* inasimamia wanafunzi kwenda shuleni ambao zamani walikuwa hawaendi kutokana na kupunguza umaskini. Lakini nimesema hivi kwa uchungu kwa sababu gani *TASAF* kazi inayofanya haichagui vyama, haina

mpango wa vyama tumeshuhudia Pemba, tumeshuhudia Unguja na tumeshughulikia na hapa Tanzania vyama vyote sichangii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niulize swali kwa kuwa *TASAF* inafanya kazi nzuri, je, Serikali ipo tayari kuwaongezea fedha ili wakidhi haja zote?

**MWENYEKIT:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kumshukuru Mheshimiwa Mchemba kwa pongezi alizolitoa kwa *TASAF* na sisi tutaendelea kuchapa kazi zaidi, lakini kuhusu swali lake kwamba je, *TASAF* iko tayari kuwaongezea fedha? Nataka niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya *TASAF* ni ya kuwafikia walengwa wote wanaohitaji kusaidiwa, mpaka sasa tumefikia walengwa asilimia sabini ndio maana kuna vijiji *TASAF* haijafika, kuna vijiji *TASAF* imefika lakini hatujawapata walengwa wote, huu mpango wa *TASAF* uko sehemu “A” na “B”. sehemu a ndio hii tunayoitekeleza sasa, *TASAF* ya Awamu ya Tatu “B” malengo ya Serikali ni kuwafikia walengwa wote, na ili kuwafikia walengwa wote ni dhahiri lazima tuongeze fedha.

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa Ndassa swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba nimuulize bwana Waziri.

Mheshimiwa Bwana Waziri *TASAF One* ilifanya vizuri sana, *TASAF Two* nayo imefanya vizuri, na pia sasa *TASAF Three* nayo inaendelea vizuri. Lakini Mheshimiwa Waziri vipo viporo vya *TASAF Two* mfano, Barabara ya Bungulwa kwenda Hundya ambayo ilitengeneza makalavati 100, yapo pale Bungulwa zaidi ya miaka mitano sasa. Barabara ya Chibuji -

Upamwa miaka mitano zaidi ilikuwa ilete pesa za ukamilishaji wa miradi hiyo miwili ya barabara ni viporo.

Mheshimiwa Waziri Mkuchika ni lini viporo hivyo vya barabara hizo vitaletwa ili kusudi barabara zitengenezwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la rafiki yangu Mheshimiwa Ndasa kama ifuatavyo kuhusu viporo anavyouliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuagiza Mkurugenzi wa *TASAF* huko aliko anakonisikiliza apeleke timu katika maeneo hayo, nipate taarifa ya hiyo miradi na baadae nitafanya maamuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, tunaendelea na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Zoezi la Upimaji Ardhi katika Manispaa Nchini**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Kwa sasa kumekuwa na wimbi kubwa la upimaji wa viwanja kwenye Manispaa mbalimbali nchini.

(a) Je, kwa nini wananchi wanalazimishwa kuuza maeneo hayo kwa Manispaa na kulipwa bei ndogo badala ya kufanya zoezi hilo kwa ubia?

(b) Kwa sababu maeneo hayo mengi ni mashamba, je, Serikali haioni kufanya hivyo kunasababisha Watanzania kukosa kazi maana asilimia 75 ni wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa eneo lolote likishatangazwa kuwa ni eneo la upangaji yaani *planning area* linapaswa kupangwa kwa kuzingatia Sheria ya Upangaji Mijini. Wananchi wanaokutwa kwenye maeneo hayo wanatakiwa kutambuliwa, kuelimishwa na kushirikishwa katika hatua zote za upangaji hadi umilikishaji. Pia Sera ya Ardhi ya mwaka 1995, Sheria ya Upimaji wa Ardhi Namba 4 na Namba 5 za mwaka 1999 na kanuni zake za mwaka 2001 na Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2007 pamoja na kanuni zake na miongozo yake, zinaelekeza Mamlaka za Upangaji kufanya upangaji na upimaji kwa kushirikisha wadau wote muhimu katika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Aidha, Sheria ya Utwaaji Ardhi Namba 47 ya mwaka 1967 pamoja na mambo mengine inazingatia mamlaka za upangaji miji uhalali wa kutwaa ardhi iliyopangwa na inayohitaji kupangwa kutoka kwa wamiliki na kuwalipa fidia kwa kufuata miongozo ya ulipaji fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Sheria za Ardhi zinaelekeza umuhimu wa kutathmini ardhi na maendelezo ya wananchi waliokutwa nayo na kulipwa fidia sambamba na kupima na kumilikisha kwa makubaliano yatakayoridhiwa na pande zote mbili bila kuathiri sheria. Hata hivyo uzoefu unaonesha kuwa mamlaka za upangaji hupenda kutumia njia ya kulipa fidia ya Ardhi na maendelezo hali ambayo imeleta malalamiko mengi kutoka kwa wananchi. Serikali inazielekeza mamlaka zote za upangaji kutowalazimisha wananchi kutumia njia moja ya kulipa fidia na badala yake wananchi washirikishwe kuchagua njia wanayoona inafaa kati ya kuingia ubia au kulipwa fidia.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote ambayo yametangazwa kuwa ni maeneo ya upangaji yaani *planning area* yanapaswa kuendelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Upangaji Mijini. Ni kweli kuwa kuna maeneo yanayotwaliwa na kuingizwa kwenye mpango ya kuendelezwa kimji ambayo ni mashamba ya wananchi. Mamlaka za Upangaji kwa kuwashirikisha wananchi wenye maeneo hayo hupanga matumizi mbalimbali yakiwemo makazi, kilimo cha mjini, viwanda vidogo vidogo, masoko, biashara kubwa na ndogo, huduma mbalimbali za kijamii kwa kutegemea maendeleo ya kimji na matakwa ya sheria. Kwa hatua hii wananchi huwa na fursa ya kupata kazi za kuwaingizia kipato kwa kupata viwango vya matumizi watakayo pendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa kitendo hicho cha kuwachukliwa ardhi wananchi sio kitendo chema, je, Serikali haioni kwamba wananchi hao tayari imewatumbukiza katika dimbwila umaskini?

Swali la pili, kwa kuwa mwananchi huyo ameridhia zoezi la kuchukuliwa ardhi yake pasina ridhaa yake, je, kwa nini Serikali isingelitoa sehemu mbadala ili kuondoa manung'uniko kwa wananchi hao kuona wameporwa ardhi yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anasema kitendo cha kutwaa maeneo ya wananchi pasipo ridhaa yao ni kwamba ni kuwaingiza katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Sheria ina ruhusu eneo likishatangazwa kuwa ni eneo la upangaji miji, Mamlaka za Upangaji kisheria zimeruhusiwa kuyatoa yale maeneo. Hiyo ni *alternative* ambayo iko kisheria, lakini katika hali halisi ambayo inaendelea sasa na kwenye kanuni ambazo zipo tumesema kwamba unapotaka kutwaa ardhi ya mtu, wananchi wanapaswa kushirikishwa. Kwa hiyo, kile kitendo cha kutwaa ardhi bado sheria inawaruhusu Mamlaka za Upangaji kuitoa ile ardhi na kupanga kile wanachoona inafaa katika utaratibu huo.

Sasa tunasema tunayo hiyo *room* ya kufanya makubaliano au maelewano na wananchi, lakini Serikali inapotaka kufanya jambo na eneo limeshaanishwa hauwezi tena wewe mwananchi kuzuia shughuli za Serikali zisifanyike. Sasa katika ule utoaji ndio hapa sasa tunasema hekima na busara pia itumike katika kuwaelimisha wale wananchi ili waweze kuelewa lengo na nia njema ya Serikali ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anaongelea habari ya kwamba Serikali kwamba kwa nini isitoe maeneo mengine ambayo bado hayajaendelezwa ili kuondokana na taratibu hizi. Sasa labda nitoe tu rai kwa Mamlaka za Upangaji Miji. Kwa sababu suala la upangaji miji ni suala ambalo liko chini ya Halmashauri zetu. Kwa hiyo kwa vyovyote vile wanapoandaa mipango yao ile ni *master plan* waangalie utaratibu mzima namna ya kuukuza ule mji ili uweze kwenda vizuri kutegemeana na mahitaji ya wakati huo. Lakini kikubwa kinachofanyika pale ushirikishwaji hata kama utatwaa eneo ambalo ni la wananchi ni yale makubaliano kwa mfano kama umepanga hapani eneo la biashara au la huduma za jamii maana yake mwananchi atapaswa kupisha. Kama ni biashara mpe nafasi yeye ya kwanza kama anaweza kuendeleza yeye mwenyewe apewe kipaumbele badala ya kumuondoa na kuleta mtu mwingine mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hilo tumekuwa tukilisema sana kwa sababu imekuwa ni kelele, watu wanalalamika. Kwa hiyo narudia kusema pale mnapopanga matumizi ya

maeneo yenu, mnapoweka mikakati ya mipango kabambe, lazima mwananchi aliyepo afikiriwe mwanzo kama ni viwanda basi kama yeye ataweza ajenge, hawezi atauza lakini mmilikishe na umpe masharti kwamba hili ni eneo la viwanda utapaswa kujenga kiwanda, hawezi ataingia ubia, hawezi atauza ataondoka.

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa Gashaza na Mheshimiwa Maryam Msabaha tafadhali.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kwanza niipongeze Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya chini ya Waziri mwenye dhamana Naibu Waziri na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la ardhi limekuwa na changamoto kubwa hususan katika kutatua migogoro kutokana na uchache wa watumishi kwenye Mabaraza ya Ardhi hususan Mabaraza ya Wilaya. Kwa mfano Wilaya yangu ya Ngara Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya anahudumia zaidi ya Wilaya mbili, na hivyo kupelekea kesi kukaa muda mrefu bila kukamilika, na wananchi wanatoka maeneo mbalimbali na kutumia gharama kubwa hata kuweza kukata tamaa.

Ni lini Serikali itaweza uajiri Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Ngara ili kuondoa usumbufu huu atakaekuwa yuko *stationed* katika Wilaya hiyo ya Ngara?

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gashaza ametaka kujua ni lini Wizara itapanga Mwenyekiti wa Baraza katika eneo lao, napenda tu nitoe taarifa kwamba upangaji wa Wenyeviti wa Mabaraza kutokana na uchache wa Wenyeviti tulionao unapangwa kutegemeana na wingi wa mashauri katika eneo lile. Lakini kwa habari tu nzuri kwenu ni kwamba sasa hivi tayari tumetangaza nafasi 20 tumepewa,

kwa ajili ya kuajiri Wenyeviti watakaokwendakatika Mabaraza.

Kwa hiyo, kitakachofanyika ni tathimini kujua ni Wilaya ipi ina mashauri mengi na inahitaji kuongezewa nguvu na Wilaya zipi ambazo zinakwenda kuanzishwa ili kuweza kupewa Wenyeviti kama Wilaya ya Mbulu ambao huwenda wakapata Mwenyekiti kwa sababu ya shughuri hizo. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi tu kwamba tutalifanyia kazi na kuweza kujua kama watahitaji kuongezewa mtu mwingine.

**MWENYEKTI:** Asante Mheshimiwa Maryam Msabaha swali fupi la nyongeza.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naomba nimuulize Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mashamba mengi ya mkonge yalikuwa wanamilikiwa na wakulima wale wahifadhi wa mikonge. Lakini mashamba yale yamekuwa Mashamba pori na wananchi wengi na hasa wa hususa wananchi wa Korogwe wanahangaika mashamba ya kulima na mashamba yale hayaendelezwi. Je, Serikali ina mpango gani kurudisha mashamba haya kwa wananchi wa Korogwe ili nao wapate kulima?

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa Naibu Waziri haya mashamba hayo sasa.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake anataka kujua ni lini pengine yale mashamba ambayo yamekuwa mashamba pori hayaendelezwi tuweze kuyarejesha pengine kwa wananchi waweze kuyatumia.

Napenda tu nilifahamishe Bunge lako suala la kutambua shamba hili ni shamba pori, halijaendelezwa na limekiuka taratibu jukumu hilo analo Afisa Ardhi Mteule katika Halmashauri husika. Kwa hiyo ni jukumu la Halmashauri husika

kuanza kufanya zile hatua za awali za kuweza kuchukua taratibu zote za kisheria, kuweza kuona kwamba huyu mtu amekiuka taratibu zake basi utaratibu wa kumnyang'anya unafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niwaombe sana kwa sababu tulishasema, ni jukumu la Halmashauri sisi kama Wizara mkishakamilisha kazi yetu ni kumshauri Mheshimiwa Rais kuweza kuyafuta na yanarudi kupangiwa matumizi. Lakini pia kwa nafasi hii nitoe rai mashamba yote yale ambayo yanafutwa na Mheshimiwa Rais, yakirudishwa katika maeneo yetu msiyapangie matumizi ya makazi mashamba yote kwa sababu sasa hivi unajikutakwamba hata pale ambapo panahitaji kuendeleza kilimo watu wanagawana mashamba. Kinachotakiwa eneo lile likisharudishwa lazima pawekewe mpango mzuri wa matumizi. Kama linaendelea kuwa shamba basi tuweze kujua ni mwekezaji yupi atafanya kazi hiyo, au kama mnabadilisha matumizi kwa sababu mengine yanakuwa yameshavamiwa na wananchi basi pia tuwe na utaratibu wa kuwa na akiba ya ardhi kwa baadae, lakini tuwe pia na kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji, ili tena tusije tukapata shida, Kwa sababu ardhi haiongezeki na watu wanaongezeka. Kwa hiyo ni jukumu la kila Halmashauri kuona namna bora ya kutumia Wizara tupo kwa ajili ya kutoa ushauri, kwa ajili kutoa Wataalam kuweza kufanikisha azma ya Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Ardhi tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Faida Itokanayo na Kiwanda cha Sukari Kagera**

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Je, Kiwanda cha Sukari Kagera tangu kimepata mwekezaji mpya baada ya kile cha mwanzo kushindwa

kuendelea na uzalishaji kimetoa mchango gani kwa Wilaya ya Misenyi, Mkoa wa Kagera na Taifa kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Kiwanda cha Sukari cha Kagera kibinafsishwe, faida na michango mbalimbali imepatikana kama ifuatavyo:-

(i) Uzalishaji wa sukari umeongezeka kutoka tani 15,362 mwaka 2004/2005 hadi tani 75,568 mwaka 2017/2018, uzalishaji huu umesaidia kuokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza bidhaa hii toka nje ya Nchi.

(ii) Pia kiwanda kina utaratibu wa kuwatumia Wakulima wa nje *(outgrowers)* katika kulima Miwa inayotumika kuzalisha sukari. Mpaka sasa kuna wakulima 500 wanaolima eneo la ekari 5,019 za miwa. Kwa mwaka 2017/2018 tu wakulima hao waliweza kuzalisha tani 60,000 za miwa ambazo ziliwapatia kipato cha shilingi bilioni tatu.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwaka 2018 kiwanda kimetoa ajira 6000 ikilinganishwa na ajira 124 zilizokuwepo mwaka 2006. Aidha, kiwanda kimejenga Hospitali yenye vitanda 78 vyenye uwezo wa kufanya *operation* kwa kutumia Madaktari Bingwa. Hospitali hiyo sasa ndiyo ya Rufaa kwa zahanati 11 katika eneo hilo.

(iv) Katika juhudi za kuchangia elimu, kiwanda kimechangia vifaa vya ujenzi, ujenzi wa madarasa, kuchimba visima vya maji, kujenga vyoo, kujenga nyumba za walimu, kuchangia madawati, kujenga maabara na kuchangia vifaa vya kufundishia kwa shule 23 katika Wilaya ya Misenyi.

(v) Aidha, katika juhudi za kuhifadhi mazingira, jumla ya miti 20,000 imepandwa katika eneo la kiwanda, pia kiwanda kimejenga mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 1,250 kwa kiwango cha changarawe ambazo pamoja na kutumika kwa shughuli za kiwanda hutumiwa pia na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitatu iliyopita kuanzia 2015/2016, 2016/2017 mpaka 2017/2018 Kiwanda cha *Kagera Sugar* kimelipa jumla ya shilingi 44,461,815,798 kama kodi Serikalini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Balozi swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri ambayo na mimi nakubaliana nayo, lakini mafanikio haya yapo hatarini kupotea kabisa ama wafanyabiashara wasio waaminifu wataendelea kungiza sukari nchini kama wanavyofanya hivi sasa na kufanya *repackaging* ya sukari hiyo kwenye mifuko wakisingizia kwamba imezalishwa hapa nchini wakati sio. Na hivyo kusababisha viwanda kukosa soko kama ambavyo inatokea kwa *Kagera Sugar* hivi sasa wamezalisha sukari, imejaa kwenye maghala, hawana sehemu ya kuiuza. Je, Serikali inalitambua hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kama Serikali inalitambua hilo ni hatua zipi inazichukua kuhakikisha usemi wa kwamba Tanzania tunajenga Tanzania ya viwanda, tujenge kweli Tanzania ya viwanda kwa kulinda viwanda vyetu, lakini si kusema tunasema tunajenga ya viwanda huku tukiruhusu wafanyabiashara wasio waaminifu wanaingiza sukari ndani ya nchi, na wanafanya *repackaging* wanaua viwanda vyetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunayo sukari nyingi kwenye viwanda vyetu. Kiwanda cha *Kagera Sugar* kina sukari na imerundikana nje kama ambavyo mmeona kwenye vyombo vya habari. Hali ni hiyo hiyo Kilombero na *TPC.* Kwa majibu ya swali la kwanza na la pili Serikali tunatambua na kikosi maalum cha Serikali kinafuatilia na kwa ruhusa yako ningeomba nisiende zaidi kwa sababu katika kinachofanyika kuna jinai ndani yake na vyombo vya dola vinafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwambia wawekezaji wote wa viwanda vyetu Serikali inawafuatilia na itawalinda na wale wanaochezea viwanda vyetu nataka niwahakikishie uchunguzi ukikamilika tutachukua hatua kali. *Fair Competition* wako kazini, *TFDA* wako kazi, TAKUKURU wako kazini na watu wa *TRA* wako kazini. Ni timu makini na niwaeleze kwa utangulizi hili suala lina jinai na anayehusika atakiona cha moto. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Jaku na Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muunganiko wa nchi mbili na unapotaja viwanda vya Tanzania huwezi kuvitenga viwanda vilivyoko Zanzibar. Nataka kujua ni sababu ipi ya msingi inayoifanya Kiwanda cha Sukari cha Mahonda – Zanzibar kisiruhusiwe kuingiza sukari yake katika soko la Tanzania Bara, sababu ya msingi hasa ni ipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili swali limekuwa likijirudia mara kwa mara, lakini niseme tu kwamba pamoja na kwamba Tanzania ni moja, suala la ulinzi wa viwanda lipo kila mahali na kama ulivyoona hata Tanzania Bara imerundikana sukari ya kutosha. Kwa hiyo, pengine badala ya kutaka nyingine

iingie tushughulikie kwanza hii hali mbaya ya kuingiza sukari ya magendo inayoendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimuombe tu Mheshimiwa Naibu Waziri anisikilize kwa makini kabisa, ninachokizungumza ni Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri, Muungano wetu huu tumeungana watu nchi mbili, Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Watu wa Tanganyika ndiyo maana jina likapatikana likaitwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenkiti, kati ya mambo waliyokubaliana yalikuwa ni biashara na viwanda na swali la msingi linahusu viwanda vilevile. Nataka sababu za msingi nijue Kiwanda cha Sukari cha Mahonda hata Wabunge tungesimama mara nyingi mjue kuwa hili suala limetukwaza ndani ya moyo wetu. Bidhaa zinazotoka Tanzania Bara zinakwenda Zanzibar bila kigugumizi, leo viwanda vya Zanzibar kuzalisha na hii Jamhuri inaitwa Tanzania hebu tuelezeni ukweli Kiswahili tuweze kufahamu kwa nini maziwa ya Bakhresa hayawezi kufika hapa yanakwama na huku tukishuhudia wakati mwingine sukari inatoka nje mnaacha kununua kutoka Zanzibar. sababu gani zinasababisha bishaa hizo kupata kigugumizi. Za Tanzania Bara zinaingia Zanzibar, za Zanzibar kuja huku imekuwa kitendawili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Kamati kati ya Waziri wa Biashara wa Tanzania (mimi) na mwenzangu wa Zanzibar. Yamekuwepo malalamiko ya wafanyabiashara na kupitia vikao hivyo tunakaa chini na kujadili suala la Kiwanda cha Maziwa cha Bakhresa kilichopo Zanzibar mimi mwenyewe nimekwenda nikakiangalia. Nikakitembelea kiwanda kile, nikaangalia uzalishaji wao ni mzuri na maziwa yamekuwa

yanaingia. Tulichokubaliana ni kwamba mtu anapopata tatizo la kukwazwa na watendaji ilitolewa namba maalum na kikao cha Mawaziri wawili kwamba anayekwamishwa awasiliane na mamlaka. Kama kuna tatizo kuhusu maziwa mnijulishe mimi kusudi mimi niende kuwa-*task* wale wanaohusika. Lakini hao wawekezaji wenye viwanda napenda nikiri kwamba ninashughulika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye Kiwanda cha Sukari cha Mahonda. Serikali imeamua kusimamia Sekta ya Sukari kwa sababu kupitia sukari tunataka kuzalisha ajira. Kwa sababu ya nia ya kuzalisha ajira na kwa sababu ya fursa ya ajira katika sekta ya sukari hii sukari ni *classified product* na sasa hiyo Tume ninayowaeleza ikimaliza kazi ndiyo mtakuja kujua maana ya *classified product* kwamba sukari inakuwa *classified.* Kiwanda cha Mahonda wake wa kuzalisha ni tani 4,000 mahitaji ya Zanzibar ni tani 20,000. Mimi nawasiliana na watu wa Zanzibar, Waziri wa Zanzibar kwamba azalishe 4,000 auze kwao. Ndiyo!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** ...ninachozungumza ndiyo..., ngoja niwaeleze...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib naomba tafadhalini tulieni.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Magendo hayo.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waheshimiwa Wabunge wanataka kujua ninachokisema.

Ningeomba muwape fursa wale wanaotaka kunisikiliza niwaeleze suala la Mahonda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niku-*address* wewe Mahonda inazalisha tani 4,000. Itakapokuwa imezalisha tani 4,000 inataka kuziuza katika soko la Tanzania Bara haitazuiliwa, tutakaa chini tuzungumze, lakini huwezo kuwa unazalisha tani 4,000 lakini wewe soko lako ni tani 20,000 halafu wewe unakwenda kuuza tani 4,000 nje hizi nyingine unazipata wapi? Kwa hiyo, ndiyo utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa taarifa katika Bunge, tunataka ku-*classify* sukari. Mafuta ya kula ni *classified,* sukari itakuwa *classified* kwa sababu tunataka ajira. Niko tayari kulisimamia hilo mpaka nitakapoambiwa vinginevyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunamaliza swali la mwisho la nyongeza, Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nashukuru kwa majibu ya Wizara kwa maswali yote yaliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapata miaka kadhaa sasa bidhaa hii ya sukari nchini inapanda bei kila inapofika mwezi wa tatu na inampa wakati mgumu mlaji katika gharama kulingana na hali ya uchumi ya Mtanzania wa chini.

Je, ni kwa nini Serikali isitazame namna ya kuzalisha sukari hii ikamudu katika ule muda wa sukari kupanda kila mwaka kuanzia mwezi wa tatu ili kila Mtanzania kwa wakati mmoja aweze kupata bidhaa hii kwa bei nafuu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wawekezaji au wazalishaji wa sukari ni wafanyabiashara binafsi na Serikali imekuwa haiwaingilii sana katika upangaji wa bei, lakini tunawaomba fursa hii wanayoipata ya kulindwa wasiitumie vibaya. Tumefanya hivyo kwa viwnada vya saruji, tumeelewana vizuri na ninatoa rai kwao iwe ni mwiko kupandisha sukari kiholela.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo litaulizwa na Mheshimiwa Mwambalaswa.

Na. 44

**Hitaji la Kiwanda cha Marumaru – Busokelo**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y MHE. FREDY A. MWAKIBETE)** aliuliza:-

Tanzania imebarikiwa kuwa na madini mbalimbali na Jimbo la Busokelo pia limebarikiwa kuwa na madini hayo.

Je, ni lini Serikali itapeleka wawekezaji wa kiwanda cha marumaru katika Kata ya Lufilyo kwenye Mto Makalya?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete Mbunge wa Busokelo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Atupele kwa jinsi ambavyo amekuwa akishirikiana na Serikali kufuatilia ili kuona madini ya eneo tajwa yanapata mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano ambao moja ya sekta ya kipaumbele ni sekta zinazotumia malighafi zinazopatikana nchini ikiwa ni pamoja uonezaji wa thamani madini ikiwemo madini aina ya *granite.* Katika Jimbo la Busokelo Kata ya Lufilyo, Kijiji cha Kikuba eneo la Mto Makalya kuna mashapo ya madini aina ya *granite* ambayo ni malighafi ya kutengeneza marumaru zenye ubora wa kimataifa. Kampuni ya *Marmo Granite Ltd.* ya Jijini Mbeya ilikuwa ikichimba mawe ya *granite* kutoka eneo hilo na

kutengeneza marumaru na baadae ilisitisha shughuli hizo kwa madai kubwa barabara ya kwenda kwenye machimbo ni mbovu hivyo kutowawezesha kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na Wizara ya Madini inaendelea kuhamasisha upatikanaji wa mwekezaji mwingine katika mradi huo. Nimuombe pia Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete aendelee kutupa ushirikiano mpaka hapo mwekezaji mwingine atakapopatikana. Vilevile Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI itawasiliana na *TARURA* ili barabara hiyo iweze kurekebishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambalaswa swali la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Kwanza kabisa wananchi wa Busokelo Kata ya Lufilyo wanakupongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri na kukushukuru sana kwa utendaji wako. Ulienda Kata ya Lufilyo ukiwa Naibu Waziri wa Elimu, ulisaidia sana katika uanzishwaji wa ujenzi wa Kituo cha *VETA* pale kwenye kata hiyo. Wanakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza; la kwanza; madini ya *granite* ni mazito sana na ndiyo maana katika kuyabeba kutoka Lufilyo kwenda mpaka Mbeya inaharibu miundombinu hasa hasa ya barabara sababu ya uzito.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wawekezaji waweze kuweka mtambo wa kutengeneza madini hayo hapo hapo sehemu ya Lufilyo ili tusiharibu miundombinu? La kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, uwekezaji katika Kata ya Lufilyo na Jimbo la Busokelo unafanana kabisa na uwekezaji katika Wilaya ya Chunya. Mheshimiwa Waziri Mkuu

alifanya ziara Chunya mwanzoni mwa mwaka huu na alishuhudia uchenjuaji wa *tailings* (makinikia) kwa wazawa na wageni na alifurahishwa sana na uchenjuaji huo uko Chunya. Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba sasa hivi Serikali iko kwenye mchakato wa kuweza kuweka mtambo wa kuchenjua makinikia hapa nchini na akapendekeza kwamba Chunya inaweza kuwa sehemu mojawapo ya kuweka mtambo huu wa kuchenjua makinikia *(smelter).* Je, mchakato huo wa kuweka *smelters* nchini hasa Chunya umefikia wapi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Kwanza kabisa nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli *granite* zina uzito mkubwa, lakini katika hatua za ku-*process* ni mwekezaji mwenyewe ndiye ana jukumu la kuangalia ni sehemu gani anaweza akaweka mtambo wa ku-*process* ili uweze kumtengenezea faida. Kwa hiyo, anatakiwa afanye *cost benefit analysis* kusafirisha na ku-*process* katika eneo husika na sisi kama Wizara ya Madini tunapendekeza mtu a-*process* madini katika eneo la uchimbaji ili atengeneze ajira katika eneo lile, hiyo moja.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika uchenjuaji wa *tailings* kwa manufaa ya Wabunge wote kufahamu kwanza *tailings* na makinikia ni vitu viwili tofauti. *Tailings* ni mabaki ya dhahabu katika udongo ambao umechenjuliwa katika hatua za awali yaani unapochenjua kwa kutumia *mercury* zinabaki *tailings* kwa ajili ya ku-*process* katika *CAP* yaani katika *process* ya aina nyingine. Sasa kutengeneza mtambo wa makinikia ni kweli kabisa Wizara ya Madini inashirikiana na makampuni makubwa kutoka nje kuweza kuwekeza katika mitambo mikubwa ya kuweza kufanya *smelting.* Mpaka sasa hivi tuna kampuni 27 ambazo zimekuja kuonesha nia za kuwekeza, kuanzisha *smelters* pamoja na *refineries* na mpaka sasa hivi

tayari tuna kampuni 10 zime-*qualify,* kwa hiyo, Serikali kwa kushirikiana na hizo kampuni za nje muda si mrefu tutaanzisha zile *smelters* hapa nchini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba sasa aulize swali lake.

Na. 45

**Tatizo la Maji Wilaya ya Momba**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Tatizo la maji Wilaya ya Momba halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu mpaka sasa.

Je, ni lini Serikali ya Awamu ya Tano itamaliza tatizo hilo katika Wilaya ya Momba?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la maji katika Wilaya ya Momba katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Maji yaani *WSDP,* Serikali imekamilisha ujenzi wa miradi sita katika Vijiji vya Namtambalala, Iyendwe, Itumbula, Mnyuzi, Chilulumo na Kamsamba katika Jimbo la Momba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu ya Pili ya Utekelezaji ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, jumla ya vijiji 10 vimependekezwa ili kuendelea kuboresha huduma ya maji katika Halmashauri ya Momba. Vijiji vilivyopendekezwa ni pamoja na Vijiji vya Ikana, Namsinde, Nkangamo, Mpapa, Chole, Itelefya, Chitete, Tindingoma, Kasinde na Samang'ombe. Serikali itaendelea kutatua tatizo

la majisafi na salama kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kubaini vyanzo vipya vya maji na kujenga miundombinu ya maji katika Halmashauri ya Momba kwa kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imechimba visima virefu viwili katika vijiji vya Chitete na Tindingoma. Usanifu wa miradi hiyo miwili upo katika hatua za mwisho za kutangaza zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi. Uchimbaji wa kisima kingine katika kijiji cha Ikana umeanza na utakapokamilika usanifu wa mradi huu utaanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Unavyoona Wabunge wamesimama ujue ndiyo hali ya maji nchini tatizo jinsi lilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu amekiri kabisa kwamba tatizo la maji lipo Wilaya ya Momba na sio tu Momba peke yake lipo nchi nzima. Sasa kauli mbiu ya ahadi ya kumtua mama ndoo kichwani imekuwa ngumu kweli kweli kutekelezeka kama ilivyo ahadi ya kupeleka milioni 50 kwa kila kijiji. *(Makofi)*

Je, Serikali inaweza ikatueleza kwa nini imekuwa rahisi kununua ndege ama Bombadier kuliko kupeleka maji safi na salama kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya mijini maji tunayotumia ku-*flash* kwenye vyoo ni bora kuliko maji ambayo wanatumia wananchi wa vijijini kwa sababu maji yale wananywea ng'ombe na wananchi wa kawaida wanakunywa huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini sasa Serikali isiwe na huruma kwa wananchi wa vijijini nchi nzima ili muweze kutatua hili tatizo la maji na sisi tuondokane na hii kero ambayo wananchi wamekuwa wanauliza kila siku wanahitaji maji safi na salama? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza napenda nimjibu Mheshimiwa Mbunge kuwa Mungu anaposema kwamba yapaswa kushukuru kwa kila jambo, Serikali inafanya jitihada kubwa sana katika kuhakikisha inatatua matatizo ya maji. Tunaona miradi mikubwa ambayo inatekelezwa, tunatoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Tabora pamoja na miji ya Igunga, tunaona Mheshimiwa Rais anavyozindua miradi kila kukicha Nansio na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha tunwapatia wananchi maji kwa maana ya maji safi, salama na yenye kuwatosheleza na nimefanya ziara katika Mkoa wa Songwe kwa kuona changamoto hiyo, tumetenga kiasi cha shilingi bilioni tisa na katika Jimbo lako tumetenga bilioni 1.77 katika kuhakikisha tunatatua tatizo hilo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Mbunge kazi ya Mbunge ni kusimamia. Naomba asimamie fedha hizo katika kuhakikisha wananchi wako wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, lengo la Wizara yetu sio kuwapa wananchi maji masafi. Niwaombe sana wataalam wetu kwa maana ya wahandisi wa maji, wabuni miradi ambayo itakuwa na tija kwa wananchi wetu katika kuhakikisha wanapata maji yaliyo safi na bora ili kuhakikisha wanapata huduma hii muhimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware na Mheshimiwa Mary Nagu.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwa kuwa upatikanaji wa maji safi na salama huathiri afya, muda wa uzalishaji na hivyo

huathiri uchumi wa kaya au jamii kwa ujumla. Sasa Serikali yetu tunajua dhahiri kuna changamoto ya maji nchini.

Je, mnajua kwamba bila kutatua changamoto ya maji nchini hatutakaa kufikia lengo la uchumi wa kati 2020/ 2025? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwa maana ya kwamba tunatambua sasa hivi nchi yetu inaenda katika nchi ya viwanda kwa maana ya uchumi wa kati na tunajua kabisa maji ni rasilimali muhimu sana na maji hayana mbadala sio kama chai ukikosa chai labda utakunywa uji. Tunajua viwanda vinahitaji maji, wananchi wanahitaji maji, kwa hiyo tutaongeza jitihada kubwa sana katika kukarabati, kujenga na kuunda miradi mikubwa katika kuhakikisha tunatatua tatizo hili la maji na tuwe na vyanzo vya kutosha ili mwisho wa siku azma iweze kutimilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Nagu.

**MHE.DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo; vijiji vingi vya Wilaya ya Hanang havina maji na vile ambavyo vimebahatika kuchimbiwa visima, visima havijakamilika.

Je, Mheshimiwa Waziri ananiambia nini ili kuhakikisha vile visima vilivyochimbwa vinakamilika na wale waliobahatika kuwa na visima hivyo waweze basi kunywa maji na kutumia kwa matumizi mengine? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza napenda nimpongeze sana mama yangu Mheshimiwa Nagu amekuwa ni mtetezi

mkubwa sana wa wananchi wake katika suala zima la maji. Amekuwa analipigania na amekuwa akifuatilia katika Wizara yetu ya Maji na Waziri wangu ambaye ni Mheshimiwa Kamwelwe aliwaagiza watu wa *DDCA* kwenda kuchimba visima vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kwamba tutawaagiza watu wetu wa *DDCA* katika kuhakikisha vile visima wanavikamilisha kwa wakati, ili wananchi wako waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Na. 46

**Kero ya Maji – Sekondari ya Mahenge**

**MHE. ALLY S. UNGANDO** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais Mstaafu, Dkt. Jakaya Kikwete alipokuwa kwenye harakati za Uchaguzi Mkuu mwaka 2005 alikubali kuwa mlezi wa Shule ya Sekondari Mahenge na akaahidi kutatua tatizo sugu la maji katika shule hiyo.

Je, ni lini Serikali itaipatia shule hiyo maji safi na salama kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la maji safi na salama linalozikabili baadhi ya shule za sekondari hapa nchini, ikiwa ni pamoja na Shule ya Sekondari Mahenge iliyoko Wilayani Kibiti. Ili kukabilina na tatizo hilo katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni

36 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya elimu sekondari wilayani humo. Kati ya hizo fedha shilingi milioni 10 zitatumika kwa ajili ya mradi wa maji safi na salama katika Shule ya Sekondari Mahenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga na kutoa fedha za miradi ya maji katika maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo ya shule.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ungando bado una swali, naona majibu yamekaa sawa hayo, Mheshimiwa Ungando.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwanza tunashukuru Kibiti tumechimbiwa visima 12 vikiwa katika Kijiji cha Mtunda, Nyamisati, Mahege, Mlanzi na Kivinja A. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha miundombinu hiyo ili wananchi hawa wapate maji safi na salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwamba je, sasa Naibu Waziri yupo tayari kuongozana na mimi kwenda katika Wilaya Mpya ya Kibiti, ili kujionea adha ya wananchi wanayopata na ukizingatia sasa hivi Kibiti ni salama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge binafsi, Mbunge anafanya kazi nzuri sana. Nataka nimhakikishie wananchi wa Kibiti kwamba Mbunge wao anatosha mpaka chenji inabaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge sisi Wizara yetu ya Maji tumeona haja ya kuusaidia Mji wa Kibiti na tumechimba visima 12. Kubwa sisi tunataka tukamilishe miundombinu ile, ili wananchi wale waweze kupata maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge, sisi jukumu letu katika kuhakikisha miradi ile tunaikamilisha kwa wakati, ili wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala la mimi kwenda Kibiti. Nataka nimhakikishie kwa kuwa, sasahivi Kibiti ni salama, mimi kama Naibu Waziri niko tayari kwenda kuambatana naye kuzungumza na wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Wizara ya Maji. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto swali la Mheshimiwa Kepteni Abbas Ali Mwinyi litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Haji Othman Hija.

**MHE. JUMA OTHMANI HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante lakini jina langu ni Juma Othman Hija sio Haji Othman Hija.

Na. 47

**Malengo ya Kuanzishwa kwa *NHIF***

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA (K.n.y. MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI)** aliuliza:-

(a) Je, Mfuko wa Bima ya Afya una wanachama wangapi na ni asilimia ngapi ya Watanzania wamejiunga na bima hiyo?

(b) Je, kwa nini baadhi ya hospitali, hasa za binafsi, hazikubali malipo kwa kutumia kadi hizo za Bima ya Afya?

(c) Je, Mfuko wa Bima ya Afya umefikia malengo ya kuanzishwa kwake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kepteni Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mbunge wa Fuoni, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulianzishwa mwaka 2001 kwa Sheria Sura ya 395. Hadi kufikia Juni, 2018 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* ulikuwa una wanachama wachangiaji 858,137 ambao wanaufanya mfuko kuhudumia jumla ya wanufaika 3,918,999 sawa na 7% ya Watanzania wote. Katika kipindi hicho hicho Mfuko wa Afya ya Jamii *(CHF)* ulikuwa na jumla ya wanufaika 13,398,936 sawa na 25% ya Watanzania wote hivyo, kufanya wananchi wanaonufaika na Mpango wa Bima ya Afya nchini chini ya *NHIF* na *CHF* kufikia 17,317,935 sawa na 32% ya Watanzania wote, lengo la mfuko ni kufikia 50% ya Watanzania wote ifikapo mwaka 2020.

(b( Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya hospitali zinakataa kadi za *NHIF* kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo hospitali kutosajiliwa na mfuko, kufutiwa usajili na kufanya vitendo vya udanganyifu na kukataa bei za huduma za *NHIF.*

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unahudumia watumishi wote wa umma, kama ilivyokusudiwa wakati wa kuanzishwa kwakwe pamoja na kuchangia kwa kiasi kikubwa kwa rasilimali fedha katika sekta ya afya, mfano, zaidi ya 80% mpaka 90% ya mapato ya vituo vya kutolea huduma za afya zinategemea fedha za *NHIF.*

Hata hivyo, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unaendelea kutekeleza mkakati wake wa kuongeza wigo wa wanachama kwa kuandikisha makundi mbalimbali katika sekta rasmi na isiyo rasmi, ikiwemo wajasiriamali wadogo wadogo na watoto chini ya miaka 18 chini ya *Mpango wa Toto Afya Card* na makundi ya wakulima kupitia Mpango

wa Ushirika Afya ambao mpango huu ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, Shinyanga, hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Othmani.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kwamba, bado asilimia ni ndogo sana ya watumizi wa mfuko huu. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwaelimisha Wananchi, ili aweze kujiunga na mfuko huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatambua kwamba bado idadi kubwa sana ya Watanzania hawajafikiwa na huduma ya bima ya afya, lakini tunatambua vilevile gharama za matibabu zinazidi kuongezeka. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaendelea kupanua wigo wa vifurushi vyetu ili kuhakikisha kwamba tunaweza kuwafikia Watanzania wengi zaidi, lakini sambamba na hilo tunaendelea kuboresha vifurushi, lakini tunaboresha vilevile utaratibu wa wananchi kuweza kuchangia na moja ya mkakati tunaoufikiria ndani ya Serikali ni utaratibu wa jipimie, ambapo mwananchi atakuwa anachangia kadiri kipato chake kinavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mkakati wa muda mrefu ambao tunaendelea kuufanyia kazi, dunia ya sasa imeelekea katika Mpango wa Bima ya Afya kwa wananchi wote na sisi kama Tanzania tumeridhia azimio hilo la kidunia na sasa hivi tuko katika mchakato wa kuandaa muswada wa sheria ambao utafanya bima ya afya kuwa ni kwa lazima kwa Watanzania wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada Mkuya halafu Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kuniona na mimi nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba kwa upande wa Zanzibar majimbo mengi tulijikusanya na tukawa tumewalipia bima ya afya watu mbalimbali, lakini baadae Mfuko huu wa *NHIF* ukasitisha kile kifurushi. Na sasa hivi nadhani karibu miaka miwili tunaambiwa *assessment* inaendelea ili kuona kwamba tunapata *alternative* ya ile bima ya afya ambayo ilikuwa imesitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpaka lini au lini sasa hii *assessment* itakamilika ili tuje na mpango mpya tuweze kuwahudumia wananchi wetu katika majimbo yetu ambao wanahitaji hii huduma ya afya kupitia Bima ya Afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa kuna utaratibu wa kutoa bima ya afya kupitia vikundi, lakini kusudio lile naomba labda nianze kutoa maelezo ya awali ili Waheshimiwa Wabunge nanyi mnielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tunapokuwa tunazungumzia suala la bima tunwataka watu wanaojiunga ni wale ambao hawana magonjwa pale wanapokuwa wanaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawasawa unataka kukata bima wakati gari lako limepata ajali. Sasa baadhi ya watu kilichotokea ni kwamba kuna vikundi vilikuwa vinajikusanya ambavyo tayari wana magonjwa makubwa na ya muda mrefu wanatengeneza vikundi, wanalipa hela ndogo shilingi 70,000 halafu wanaenda sasa hospitalini

wanapata huduma kubwa, kwa utaratibu huo tungeweza tukaufilisi mfuko.

Kwa hiyo, baada ya kubaini kwamba, kulikuwa na changamoto hiyo, tulisitisha hilo fao, ili kuweza kupitia taratibu nzuri za kutengeneza vile vikundi na vigezo vya kuzingatia kwa hiyo, bado hiyo kazi inaendelea kufanyika na tutakapokamilisha tutautangaza upya utaratibu mpya wa kujiunga na vikundi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suluhu ya kudumu, sisi kama Serikali tuko katika hatua ya mwisho ya kuandaa muswada na utakapokamilika ndani ya Serikali tutauleta hapa Bungeni na mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono katika muswada huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally swali fupi la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na niseme wazi nimeyaelewa sana majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na majibu hayo mazuri na ufafanuzi huo, wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro wamehamasika sana kwenye *SACCOS* na sio vikundi vya ambao wameshapata maradhi tayari, bali ni vikundi vya akinamama ambao wanafundishana mambo mengi ikiwemo ujasiriamali, *scheme* za elimu pamoja hiyo kujiunga na *NHIF.* Ni muda mrefu sasa toka mwaka jana wameandikiwa barua kusitisha zoezi hilo, lakini kwao imekuwa ni usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri haoni kwamba itakuwa sasa ni usumbufu wale akinamama kurudi kuanza upya, badala ya kuweka muendelezo kwamba walikuwepo kwenye *NHIF* na waendelee?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sina maelezezo kamili kuhusiana na hivi vikundi vya Mkoa wa Kilimanjaro ambavyo Mheshimiwa Mbunge anaviongelea, mimi nimuombe sana Mama Shally Raymond baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu tuonane anipe maelezo na mimi nimtume Meneja wangu wa *NHIF* Mkoa wa Kilimanjaro aende akavitembelee na kuvikagua vikundi, kwa sababu tunapozungumzia vikundi vya washirika na vikundi hivi vya *SACCOS* ni vikundi ambavyo na sisi tumekuwa tunavihamasisha vijiunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka tuweze kupata maelezo kidogo tuweze kubaini changamoto zilizopo na tuweze kuchukua hatua kwa haraka zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nuru swali la nyongeza,

**MHE. NURU AWADHI BAFADHIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa wananchi wengi wamehamasika katika kujiunga na bima ya afya, wananchi hawa wanapofika hospitalini daktari anaweza akamuandikia dawa moja *paracetamol* nyingine anaambiwa akanunue. Je, Serikali inatwambiaje kuhusu hawa Wananchi wanaoambiwa wakanunue wakati wao wamejiunga na Bima ya Afya, ili waepuke makali ya maisha? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano imeongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 30 hadi shilingi bilioni 270 katika bajeti ambayo tumeipitisha mwezi Julai mwaka huu; hali ya upatikanaji wa dawa nchini sasa hivi ni zaidi ya 90%; lakini sambamba na hilo mwezi Februari tulitoa mwongozo wa utoaji huduma za afya na aina za dawa ambazo zitatumika katika kila ngazi kwa aina ya ugonjwa na orodha hii tumejaribu kuihuisha pamoja na wenzetu wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo tumeanzisha utaratibu wa maduka ya dawa muhimu ambazo haziko katika orodha yetu ya dawa zile muhimu ambazo ni 167 ili yale maduka yaweze kutoa dawa zile ambazo ziko nje ya utaratibu wetu wa hizi *standard treatment guideline* lakini zinahitajika katika utaratibu wa bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe na nimhakikishie Mbunge kuwa tunaendelea kuboresha mfumo huu kuhakikisha kwamba dawa zote ikiwa na zile ambazo zilikuwa zinahitajika kwa wagonjwa wa bima zinapatikana katika hospitali zetu za umma.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hawa kwa niaba.

Na. 48

**Mila na Tamaduni za Jamii za Wafugaji**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA (K.n.y. MHE. AMINA S. MOLLEL)** aliuliza:-

Baadhi ya mila na tamaduni katika jamii za wafugaji hapa nchini haziwapeleki watoto wa kike shule, badala yake wanawaozesha katika umri mdogo kinyume na ridhaa yao, hivyo kukiuka sheria za nchi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa mila na tamaduni hizo haziwanyimi watoto wa kike haki yao ya kupata elimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua haki za msingi za mtoto ikiwemo ya kupata elimu na kuendelezwa ili kupata nguvu kazi yenye tija itakayochangia kujenga uchumi unaotarajiwa katika nchi yetu. Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa mila na tamaduni zenye madhara zinazosababisha watoto kushindwa kwenda shule zinashughulikiwa ipasavyo. Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 inayoelekeza kutoa haki kwa mtoto bila kubaguliwa ikiwemo kuendelezwa kielimu na kutokomeza mila zinazoruhusu ndoa katika umri mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekezaji wa Sheria Namba 21 ya mwaka 2009 inayoelekeza utoaji wa haki na huduma ya msingi kwa mtoto ikiwemo elimu, malazi na huduma ya afya na utekelezaji wa Mpango wa Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/2018 ambao utaisha mwaka 2021/2022 ambao umelenga kushirikisha jamii kutokomeza mila na tamaduni zenye madhara kwa watoto na hasa watoto wa kike ili kumuwezesha kupata haki zake za msingi ikiwemo elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2017/2018 Wizara imetoa elimu kuhusu mila na desturi zenye madhara, ikiwemo ukeketaji, mimba na ndoa za utotoni kwa jumla ya wananchi 13,020 yakiwemo makundi mbalimbali ya mangariba, viongozi wa jadi na jamii ya wafugaji katika Mikoa ya Dodoma, Arusha, Mara, Shinyanga, Tabora, Lindi, Tanga, Dar es Salaam na Katavi. Aidha, Wizara imeandaa mdahalo mkubwa wa Kitaifa mwezi Oktoba mwaka huu utakaojumuisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini na viongozi wa kimila ili kujadili na kupata muafaka wa Kitaifa wa namna ya kutokomeza matatizo ya ukatili kwa watoto yakiwemo ukeketaji, ndoa na mimba za uototoni, ambayo yamekuwa yakiongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia, imeanzisha klabu za watoto na mabaraza ya watoto na kamati za ulinzi wa wanawake na watoto katika ngazi mbalimbali za utendaji kuanzia ngazi ya taifa hadi kijiji ili kujadili na kutafuta ufumbuzi wa masuala ya ukatili wa wanawake na watoto, yakiwemo masuala ya mila na tamaduni zenye madhara kwa watoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa swali la nyogeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa nitapenda nikuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi, chini ya Rais John Pombe Magufuli imedhamiria kwa dhati kabisa kutoa elimu bure kwa watoto wote; na kwa kuwa, wazazi wengi wa jamii ya kifugaji hawajajitokeza kuwaandikisha watoto wao badala yake wanaamua kuanzisha shule zao ama kufungua shule zao na kuwapeleka watoto wao. Napenda kujua sasa je, Serikali mna taarifa na uwepo wa shule hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu la pili, kama Serikali inafahamu uwepo wa hizo shule ni nini sasa mkakati wa kuhakikisha mnazisaidia shule hizo, ili ziweze kufanya vizuri? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani ilikuja na mpango wa elimu bure. Lengo ni kuhakikiksha kwamba kila mtoto wa Kitanzania anapata fursa ya kuendelezwa kwa mujibu wa sheria kupitia nyanja ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la msingi ambalo aliuliza kwamba, je, tuna ufahamu wa hizi shule bubu, ambazo naziita shule bubu;-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimuombe sana Mheshimiwa Mbunge kama ana taarifa ya hizi shule basi na sisi atujulishe kwa sababu shule zetu zote za msingi ni shule ambazo zinatambuliwa Kiserikali na zimesajiliwa na Serikali na zinapata ruzuku na sisi tunapeleka walimu. Kama kunakuwa na shule bubu napata shida kuelewa kwamba hizo shule zimesajiliwa wapi? Hao walimu wanawapata wapi na aina ya elimu ambayo wanaitoa ni elimu ya namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nimuombe sana Mheshimiwa Mbunge kama ana taarifa ya hizi shule, basi atujulishe Serikali, ili tuweze kuzitambua. Na kama tukiona kwamba, zina mazingira ambayo na sisi kama Serikali tunaweza kuzichukua, basi tutaweka utaratibu wa kuzirasimisha rasmi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija Nassir halafu Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuchukua hatua kali za kuzuia ukeketaji jamii zinazojishughulisha na ukeketaji zimekuja na njia mpya za kuwakeketa watoto wakiwa bado wachanga. Je, Serikali inalifahamu hili na kama inalifahamu ni hatua gani zimechachukuliwa mpaka sasa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa sita nilipokuwa mgeni rasmi katika Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika pale Arusha liliibuliwa suala la ukeketaji wa watoto

wachanga. Baada ya Serikali kubana na kutoa elimu ya kutosha na kwa watoto kujitambua mara nyingi watoto hawa ambao wana umri mkubwa wamekuwa wanatoa taarifa na sisi tumekuwa tunachukua hatua. Sasa kuna baadhi ya wazazi ambao wameendelea na sasa hivi wamehama kutoka kukeketa mabinti ambao umri umekuwa wamehamia katika kukeketa watoto wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunalitambua hilo na tumeshatoa maelekezo katika wizara yangu ya afya, maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto idara kuu ya maendeleo ya jamii kushirikiana na idara kuu ya afya kuweka utaratibu mahususi ambao tutaanza kubaini watoto wote ambao wanakeketwa wakiwa na umri mdogo hususani pale watoto wanapokuwa wanaenda kliniki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina amini swali la msingi lilikuwa linahusu watoto kunyimwa haki yao ya kwenda shule kutokana na mila na destruri. Pamoja na mila na desturi sasa hivi au kwa muda mrefu kumezuka tabia ya wazazi hususani wanawake wakitembea na watoto yaani wakiwa na watoto wao wadogo au watoto wa kukodi kwa ajili ya kuombaomba, hali inayopelekea watoto hawa wasiende shule kwa sababu wakiwa na wale watoto maana yake wananchi watawahurumia na kuwapa msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inajua kwamba kuna hili jambo na kama inajua ina mkakati gani kuhakikisha kwamba wazazi hao hawatumii watoto wao kama chambo cha kupata misaada na watoto hawa waweze kwenda shule kwa sababu bila hivyo watoto hawa wataendelea kuwa nyumbani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri swali zuri kabisa la wanawake.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Lyimo ameuliza swali zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haki za msingi za mtoto ni pamoja na kuendelezwa, kulindwa, kutunzwa na kutotumikishwa kazi nzito. Swali hili ambalo ameliuliza katika maudhuhi yake yote haya haki zote hizi za msingi za mtoto zinavunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,mimi niwaombe na tumeshatoa maelekezo kwa wataalam wetu ndani ya Wizara, kwanza tumefanya katika haya majiji makubwa sensa ya kubaini watoto wote ambao wanaishi katika mazingira hatarishi na tumebaini kama watoto karibu 7,000. Mpaka sasa hivi tumeweza tuwarudisha watoto zaidi ya 1,000 majumbani kwao kutegemea na *nature* ya matatizo ambayo tumekutana nao, lakini tunajua *database* ya watoto ambao tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuwasisitiza Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii hususani katika haya majiji makubwa kuhakikisha kwamba hawa wakina mama ambao wana tabia kama hizo ambao watoto hawaendi shule na watoto wanatumikishwa kazi nzito tunaweza kuwabaini na kuchukua hatua za msingi ili kukomesha kabisa matatizo kama haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad.

Na. 49

**Minara ya Simu Kujengwa Katika Makazi ya Watu**

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD (K.n.y MHE. MGENI JADI KADIKA)** aliuliza:-

Minara mingi ya simu imejengwa katika makazi ya watu na minara hiyo inatumia mionzi hatari kwa maisha ya binadamu.

Je, Serikali inaliangaliaje suala hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu ya swali hilo).

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI NA MAWASIALIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa baadhi ya minara ya simu hujengwa karibu na makazi ya watu kwa lengo la kutoa mawasiliano bora. Ili kuhakikisha usalama kwa binadamu kuhusiana na madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na huduma za mawasiliano hususani mionzi inayotumika katika mawasiliano, Tanzania huzingatia viwango na miongozo ya udhibiti wa mionzi inayotolewa na Tume ya Kimataifa ya Kudhibiti Mionzi ijulikanayo kama *International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIRP).* Tume hii ilianzishwa na Umoja wa Mawasialiano ya Kimataifa *International Telecommunication Union (ITU)* ili kutafiti juu ya madhara yatokanayo na mionzi inayotokana na vifaa vya redio hususani simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa kuzingatia tafiti mbalimbali za kisayansi hakuna madhara yatokanayo na mionzi ya mawasiliano hata watu wanaoishi karibu na minara ya simu. Kulingana na tafiti za Tume *(ICNIRP)* imebainishwa kwamba hakuna athari zinazoweza kusababishwa na mionzi au masafa ya redio, kwa vile nguvu iliyomo katika masafa au mionzi inayosafirishwa hupungua kwa kiwango kikubwa sana kutoka kwenye antena (mara 1000 katika umbali wa mita moja kutoka kwenye antena) na kwa vile antena

hufungwa mita kadhaa juu ya minara, nguvu ya mionzi hiyo huwa ni ndogo sana ifikapo chini kiasi cha kuweza kuleta athari yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 inaelekeza kukuza usalama katika matumizi ya bidhaa na huduma za TEHAMA. Sawasawa na maelekezo haya ya kisera, katika kuhakikisha kuwa viwango vya mionzi vinavyotokana na minara ya mawasiliano havizidi kiwango kilichoelekezwa kimataifa. *TCRA* kwa kushirikiana na Tume ya Nguvu za Atomiki *(Atomic Energy Commission)* imekuwa ikifanya ukaguzi mara kwa mara na kubaini kwamba hadi sasa hakuna mionzi yeyote inayotokana na minara hii inayoweza kuathiri watu.

**MWWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma swali la nyongeza.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:**Mheshimiwa Mwenyekiti,ahsante sana. pamoja na jibu la Mheshimiwa Waziri lakini zipo tafiti kadhaa na nyingi ambazo kimsingi zinaonesha kwamba bado kuna madhara makubwa ya watu kuumwa na kichwa na hata kupoteza kumbukumbu kutokana na mionzi inayotokana na minara hii ya simu.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja hasa ya kufanya tafiti za kina zaidi ili kubaini kwamba madhara haya yapo na namna gani Serikali itatumia njia ili kuyaondoa madhara hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, minara hii imejengwa na imo ndani ya Halmashauri, sasa kimsingi kuna malalamiko makubwa kwa wananchi ambao wamo ndani ya Halmashauri hizo ambazo minara hii imejengwa kwamba hawafaidiki na uwepo wa minara hii ingawa minara hii ipo kibiashara. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa kuandaa utaratibu maalum ili kuona kwamba wananchi na Halmashauri ambazo minara hii ipo zinafaidika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI NA MAWASIALIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafiti zilizofanyika na Umoja wa Mawasiliano Duniani *(ITU)* kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi siyo kwamba madhara hakuna kabisa, madhara yapo na hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa na makampuni ya simu kwa kuzungushia uzio eneo ambalo wamefunga mnara. Katika kufanya hivyo tunaamini kwa ule upungufu madhara wa mara 1,000 kwa kila mita moja kutoka kwenye mnara hakuna mtu anayeweza kudhurika. Hayo madhara mengine yanayotokana na mtu kuumwa kichwa ni yale ambayo siyo ajabu inawezekana hayatokani na matatizo ya mnara kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya wale ambao minara imefungwa kwenye maeneo yao na kutopata chochote kutokana na hilo na hilo limekuwa likishughulikiwa. Tumekuwa tukipata changamoto kama Wizara kwamba tunapowapa kazi wale watoa huduma labda Tigo, Vodacom, Airtel na kadhalika wanakwenda kwanza kuongea na wananchi kule vijijini. Kwa hiyo, wakishaongea nao wananunua maeneo yao kwa hiyo mwananchi wa kijijini kwanza anakuwa anapokea *rent,* lakini kunakuwa na tozo ya Halmashauri ambayo huwa inatoa kutokana na vikao walivyokaa Madiwani husika.

Kwa hiyo, hilo linakuwa ni gumu sana sisi kama Serikali kuendelea kuliingilia lakini nimuahidi Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba tunaendelea kulifuatilia kuhakikisha kwamba Serikali kupitia Halmashauri inapata tozo ambazo ni stahiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto swali fupi la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambazo anazifanya. Kwa kuwa wananchi wa Kilolo bado hawajaanza kupata athari yoyote ya minara hii sasa naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu nimekuwa nikiulizia swali la kupata mawasiliano ambayo hayapo kabisa katika vijiji vya Imalutwa, Mazombe, Isele, Kising'a, Mahenge, Maganailindi na Ilambo. Je, Serikali sasa safari hii itakuwa tayari hasa Mheshimiwa Waziri na ulitoa ahadi kwamba utafika ili wananchi hawa waweze kupata mawasiliano ili waendane na sera ya viwanda kwenye nchi yao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu mafupi kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI NA MAWASIALIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Venance kwa jinsi anavyofuatilia sana suala la wananchi wake kupata mawasiliano katika shughuli zao, kwa kweli amefuatilia sana na katika awamu hii ambapo tumetenga kata 173 za kupelekewa mawasiliano kuna Kata zake nafikiri tatu ambazo tayari tumeshazitengea kwenda kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuahidi tu kwamba hizo kata nyingine ambazo hazijapatiwa mwisho wa mwezi huu kuna kata nyingine 205 ambazo tunategemea zitaingizwa kwenye mpango wa kupelekewa mawasiliano ya simu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla, Mbunge wa Makete sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Kujenga Maghala ya Chakula kwa Kila Halmashauri**

**MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING** aliuliza:-

Mwaka 2016 - 2018 bei ya zao la mahindi ambayo ndiyo nguvu ya uchumi kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini imeshuka sana hadi kufikia shilingi 2000 kwa debe kwenye baadhi ya Wilaya kama Ludewa na Makete.

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza fedha *NFRA* ili mahindi yanayozalishwa yanunuliwe na kuwapa ahueni wananchi?

(b) Je, ni lini Serikali kupitia *NFRA* itajenga maghala katika kila Halmashauri ili kurahishisha uhifadhi wa mahindi na mazao mengine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama naomba nilitumie Bunge lako tukufu kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa imani kubwa aliyoionesha kwangu kuniamini kama naweza kutoa mchango wangu kumsaidia katika sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Mheshimiwa Spika kwa miaka mitatu niliyokaa hapa Bungeni jinsi alivyonihamisha kwenye Kamati tatu kuanzia Kamati ya Sheria Ndogo, Kamati ya *PAC* na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii imenipa uzoefu wa kutosha kufahamu shughuli za Serikali na Bunge kwa ujumla. Pia niwashukuru wajumbe wa Kamati hizo zote wakiongozwa na wenyeviti na makamu Wenyeviti hasa nikianza na ile ya Kamati ya Sheria Ndogo Mzee wangu Chenge nimekuja *PAC* Mama Kaboyoka na Kamati ya Ardhi ndugu yangu Nape na Wabunge wote wa Kamati hizo walinipa ushirikiano wa kutosha katika majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki kwa uvumilivu na ushirikiano wanaonipa hasa kwa wakati huu niliokuwa mbali nao kwenye kutimiza majukumu yangu ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nimshukuru mke wangu mpenzi na familia yangu, Bi. Husna Abbas Mgumba kwa uvumilivu na ushirikiano wa karibu sana wanaonipa na ushauri wake kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo na shukrani hizo, nianze kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge na kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla King, Mbunge wa Jimbo la Makete lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa nafaka hususan mahindi ili kuiwezesha *NFRA* kutekeleza jukumu la kununua na kuhifadhi akiba ya chakula. Pamoja na ruzuku ya Serikali, wakala hutumia vyanzo vyake vingine vya mapato kugharamia ununuzi wa nafaka ambazo hununuliwa kutoka kwenye maeneo yenye ziada katika uzalishaji wa chakula kupitia vikundi au vyama vya wakulima. Aidha, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* hauna uwezo wa kununua mahindi yote yanayozalishwa nchini bali inatekeleza na jukumu la kununua na kuhifadhi akiba ya chakula cha taifa kwa kuzingatia bajeti inayotototengwa na Serikali na vyanzo vingine vya mapato kwa lengo la kuhakikisha usalama wa chakula ili kukubaliana na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mikakati ya kutafuta masoko kwa ajili ya mazao ya wakulima ikiwemo mahindi kwa kuondoa zuio la kuuza mahindi nje ya nchi, kuongeza bajeti ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa ajili ya ununuzi wa mazao na kuongeza uwezo wa Wakala wa Kuhifadhi Nafaka kutoka tani 251,000 hadi kufikia tani 501,000 ifikapo mwaka 2019/2020. Aidha, mikakati mingine ni kuongeza matumizi ya mahindi kwa kuyaongezea thamani ili kuuza unga na pumba pamoja na kuliingiza zao la mahindi katika mfumo wa stakabadhi ghalani ili kuongeza wigo wa masoko ya mazao ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara imetenga jumla ya shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa maghala 15 katika Halmashauri za mikoa ya Mwaza, Manyara, Singida, Kigoma, Simiyu, Tanga na Tabora. Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* unajenga maghala na vihenge vya kisasa katika Halmashauri za Shinyanga, Babati, Makambako, Sumbawanga, Mpanda, Mbozi, Dodoma na Songea ambayo ni makao makuu ya kanda zetu saba yenye uwezo wa kuhifadhi nafaka tani 250,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika mradi wa kudhibiti sumukuvu jumla ya maghala 14 yatajengwa katika Mikoa ya Songwe, Dodoma, Manyara, Tabora, Kigoma, Mtwara, Ruvuma, Mwanza, Geita na Simiyu. Aidha, Wizara itakamilisha ukarabati wa maghala 33 kwa ajili ya hifadhi ya mahindi katika Halmashauri za Wilaya za Mlele, Nsimbo, Songea na Njombe pamoja na kuandaa mpango wa ukarabati na ujenzi wa maghala kwa nchi nzima. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa King swali la nyongeza.

**MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa maeneo yote yaliyotajwa kwa ajili ya ujenzi wa maghala hazijatajwa sehemu zile ambazo tunajua zinazalisha mahindi kwa wingi ikiwemo Wilaya ya Makete, nini kauli ya Serikali juu ya ujenzi wa ghala Makete?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuwatetea wananchi wake na kunihimiza kufika Makambako tarehe 3 mwezi huu kwenda kuangalia hali ya ununuzi wa mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia jibu langu la msingi niliyataja maeneo mbalimbali ambayo Serikali inakwenda kujenga maghala ya kuhifadhia mahindi kuanzia ya Halmashauri mpaka ya wakala wetu wa hifadhi. Moja ya sehemu hiyo ni Makambako; Makambako ni Makao Makuu ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo inajumuisha Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya pamoja na Songwe. Eneo analotoka Mheshimiwa Mbunge ni Makete, ni eneo la Mkoa wa Njombe na ni sehemu ya hii Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili eneo la Makambako ndiyo tunakwenda kujenga ghala kubwa kuliko sehemu yoyote Tanzania; maghala haya matatu tunayoenda kujenga yatakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 kwa mwaka. Maana yake tukiongeza na uwezo wa sasa wa ghala lile tani 39,000 tutakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 99,000. Hii maana yake maeneo ya mikoa yote hiyo miwili hususani Mkoa wa Njombe ambako lipo Makao Makuu na Wilaya ya Makete tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi mahindi kwa mwaka ujao Desemba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Kutokana na muda tunamalizia Wizara ya mwisho, Wizara ya Madini; Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

Na. 51

**Utekelezaji wa Mkataba wa *CSR* Katika Mgodi wa *GGM***

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA (K.n.y. MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA)** aliuliza:-

Katika kutekeleza Mkataba wa *Corporate Social Responsibility (CSR),* Mgodi wa *GGM* unatumia bei za manunuzi kutoka nchi ya Afrika Kusini, mfano bei ya bati moja ni shilingi 81,000 na bei ya mfuko wa saruji ni shilingi 48,000.

Je, kwa nini Serikali isiziite pande hizi mbili, Mgodi wa *GGM* na Halmashauri ili iweze kumaliza mgogoro huo na kuweka utaratibu mzuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Madini majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini kama lilivyoulizwa na Mheshimiwa Bukwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza matakwa ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 kifungu cha 105, Halmashauri ya Mji wa Geita na Halmashauri ya Wilaya ya Geita pamoja na Mgodi wa Dhahabu wa *GGM* zimeandaa Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii wa mwaka 2018 *(Corporate Social Responsibility Plan, 2018).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuandaa mpango huo uliokuwa shirikishi, *GGM* iliwasilisha bei ya bati la geji 28 kwa kipimo cha mita za mraba ambapo bei ya mita moja ya mraba ilikuwa ni shilingi 81,000 na bei ya mfuko wa saruji ilikuwa ni shilingi 48,000 kwa mfuko mmoja. Aidha, baada ya bei hizo zilizopendekezwa na mgodi kuonekana kuwa ni kubwa, pande zote mbili ambazo ni Halmashauri ya Mji wa Geita na Halmashauri ya Wilaya ya Geita pamoja na Kampuni ya *GGM* walikaa na kufanya majadiliano ya pamoja na kukubaliana bei zilizopendekezwa na *GGM* zirekebishwe kwa kuweka bei ya bati moja na siyo bei ya bati kwa mita za mraba ambapo bati moja geji 28 ilikubalika kuwa shilingi 27,000 na mfuko mmoja wa saruji kuwa shilingi 18,000.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bukwimba swali la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Menyekiti, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Inaonesha kwamba amefuatilia kweli katika Halmashauri ya Wilaya jinsi ambavyo imefanya kazi imekaa na *GGM.* Lakini vilevile niishukuru *GGM* kwa kuanza kutekeleza uwajibikaji wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017 katika kipengele cha 105.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa kuna baadhi ya makampuni ya uwekezaji katika sekta ya madini ambayo mpaka sasa hayajaanza kufanya utekelezaji wa sheria hii. Kwa mfano Mgodi ule wa Bacliff pale hawajaanza kufanya utekelezaji. Je, Serikai inasemaje sasa kwa makampuni ambayo hayajaanza kufanya utekelezaji wa sheria hii mpaka sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mgodi wa Bulyanhulu ambao uko Kahama umepakana sana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita, hasa katika Jimbo la Busanda katika Kata ya Butobela kule Nyakagwe pamoja na Kata ya Bukoli na wananchi walioko jirani na maeneo haya wananufaika, hasa wale wa Kahama, lakini wale wa upande wa Geita sasa ambao nimewataja wa Nyakagwe na Bukoli ni kilometa mbili tu kutoka kwenye mgodi ule lakini hawanufaiki chochote.

Je, Serikali inasemaje sasa kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Busanda pia, hasa wa maeneo ya Bukoli pamoja na Nyakago wanafaidika na mgodi uliopo Bulyanhulu ambao uko jirani sana na sisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kwamba

Mgodi wa Bacliff ni kweli kabisa haujatoa *CSR Plan* yao kutokana na mujibu wa sheria inavyosema. Lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Mgodi ule wa Bacliff mpaka sasa hivi hawajaanza uzalishaji. Kwa hiyo watakapokwenda katika uzalishaji ni lazima watupe *CSR Plan* yao na *CSR Plan* yao lazima iwe shirikishi kwa kushirikiana na Halmashauri husika waangalie namna gani wataweza kui-*finance* miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya au Halmamshauri hiyo.

Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba asiwe na wasiwasi, mradi huu wa Bacliff utakapoanza kufanya kazi basi lazima sisi kama Wizara tutahakikisha kwamba wamekuja na *CSR Plan* yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kwa kampuni yoyote, nipende kutoa wito kwa makampuni yoyote ya uwekezaji, makampuni yote ambayo yanawekeza katika sekta ya madini ni lazima yatii sheria na taratibu zilizowekwa. Sheria ya mwaka 2017 na Kanuni zake za mwaka 2018 zinahitaji kila kampuni ilete *CSR Plan* yao kuhakikisha kwamba wanashirikiana na jamii au Halmshauri husika katika kuratibu na kuhakikisha kuwa wanatoa fedha katika kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo katika halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kanuni za mwaka 2018 zinasema kuna masuala ya *local content plan* pamoja na kile kiapo cha uaminifu. Ni lazima kila kampuni ikamilishe yale mambo ambayo yameainishwa katika kanuni za mwaka 2018, bila kufanya hivyo sisi kama Wizara hatutasita kuchukua hatua katika kampuni zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuhusiana na wale watu ambao wamepakana na Wilaya ya Kahama na hasa ambao wapo karibu na Mgodi wa Bulyankulu, sisi tunafuata sheria. Sheria ndiyo zinazosema kwamba halmashauri husika iweze kufaidika kwa maana ya kupata *service levy.* Lakini vilevile nitoe tu wito kwa Mgodi wa Bulyankulu, kama inawezekana kata ambazo ziko karibu na mgodi huo basi waweze kuwasaidia wananchi wa maeneo

hayo kwa kuwapa ajira kupitia ile kanuni yetu sisi ya *local content* kwa maana ya kuwajali Watanzania wanaoishi karibu na maeneo yale kwa kuwapa ajira lakini vilevile kuwapa fursa ya kuweza kuuza bidhaa na kuuza huduma mbalimbali katika mgodi huo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Swali letu la mwisho linaulizwa na Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje.

Na. 52

**Migodi ya Makaa ya Mawe Kiwira na Kabulo**

**MHE. JANET Z. MBENE** aliuliza:-

Wilaya ya Ileje imejaliwa kuwa na rasilimali ya makaa ya mawe ya Kiwira na Kabulo na *STAMICO* imekaririwa kuanza rasmi kuuza makaa hayo kwa kasi ili kukidhi mahitaji ya viwanda vya saruji na kukuza pato la Taifa, aidha, *STAMICO* ilianza uzalishaji wa majaribio ya makaa ya mawe katika Mgodi wa Kabulo tarehe 30/04/2017.

(a) Je, Mgodi wa Kabulo utaendelea kuchimba baada ya majaribio hayo na ni nani anayefanya uchimbaji huo?

(b) Je, kuna makubaliano gani na Wilaya ya Ileje juu ya mrahaba na uchumi kwa wana Ileje?

(c) Je, ni lini Mgodi wa Kiwira utaanza kufanya kazi na ni nini hasa kinachokwamisha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba sasa nijibu swali la mama yangu,

Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Jimbo la Ileje, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* lilianzishwa mwaka 1972 likiwa na jukumu la kushiriki na kusimamia maslahi ya Serikali katika sekta ya madini pamoja na rasilimali ya madini. Aidha, mwaka 2005 Mgodi wa Kiwira ulibinafsishwa kwa kampuni binafsi ya wazawa ya *Tan Power Resources Ltd. (TPR)* kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa umeme na kufikia megawati 200. Mnamo tarehe 30, Juni, 2014 Serikali iliikabidhi *STAMICO* Mgodi wa Kiwira kutokana na mbia mwenza kukosa mtaji wa kuendesha mgodi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* ilianza uchimbaji wa majaribio katika leseni yake ya makaa ya mawe ya Kabulo mnamo mwezi Aprili, 2017 ambapo katika kazi hiyo jumla ya tani 8,674 za makaa ya mawe zilichimbwa. Baada ya kukamilisha majaribio ya awali *STAMICO* imeanza mchakato wa kumpata mkandarasi atakayefanya uchimbaji. Lengo ni mkandarasi huyo aanze kazi ya uchimbaji utakaozingatia taratibu zote za uchimbaji, mazingira na usalama mgodini katikati ya mwaka huu wa fedha yani 2018/ 2019.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* kama ilivyo kwa wamiliki wengine wenye leseni za uchimbaji wa madini inawajibika kulipa ushuru wa huduma kwa Halmashauri wa asilimia 0.3 ya mapato ghafi yatokanayo na mauzo ya makaa ya mawe. *STAMICO* tayari imeanza kulipa ushuru wa huduma kwa Halmashauri ya Wilaya hiyo kutokana na mauzo ya makaa yaliyofanyika ambapo kiasi cha shilingi 57,600 kimelipwa. Aidha, jumla ya shilingi 1,735,900 zimelipwa kama ushuru wa barabara kwa Halmashauri. Manufaa mengine ni pamoja na kutoa ajira kwa wananchi wa Wilaya ya Ileje na kuchangia huduma mbalimbali za kijamii ikiwemo afya, elimu na maji.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* ilikabidhiwa Mgodi wa Kiwira mnamo mwezi Juni, 2014 ili kuendesha na

kuusimamia kufuatia Kampuni ya *Tan Power Resources* kuurejesha Serikalini. Aidha, *STAMICO* imeendelea na jitihada mbalimbali za kutafuta fedha ikiwa ni pamoja na kutafuta wabia wenye uwezo watakaoshirikiana na shirika katika uendeshaji wa mradi huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbene swali la nyongeza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa mradi huu ni mradi ambao unatambulika kuwa ni mradi wa kimkakati na kwa kiasi mpaka 2013 ulikuwa unatengewa fedha ya maendeleo lakini kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015 hadi sasa hivi hakuna fedha yoyote ambayo imekuwa ikitengewa mradi huu ilhali sasa hivi mradi huu umeanza kufanya kazi na tayari mbia amepatikana na wiki hii ameshaweka saini pamoja na *STAMICO* ya kuanza kuchimba makaa ya mawe katika Mgodi wa Kabulo.

Je, Serikali imeuondoa mradi huu katika miradi ya kimkakati? Na kama ni hivyo, je, hiyo fedha ya kuendeleza hasa ukarabati wa Mgodi wa Kiwira wenyewe inayohitajika sasa hivi kwa sababu tayari mbia ameshapatikana itapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa mradi huu ambao umekuwa kwa muda mrefu ukinufaisha Wilaya nyingine ya jirani sasa hivi umeanza kutambulika rasmi kuwa ni mradi wa Ileje na kwa urahisi wa kuufikia mradi huu kuna daraja katika Mto Mwalisi ambalo liliharibika kwa muda mrefu la kilometa karibu saba na barabara yake, imesababisha mradi huu sasa kuwa unatumia njia ndefu ya kupitia Kyela ambayo ni karibu kilometa 36 na kuleta gharama kubwa na kuongeza gharama kubwa kwa mradi huu.

Je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha kuwa hii barabara pamoja na Daraja la Mwalisi ambalo ndilo linalounganisha Wilaya ya Ileje na Mradi wa Kiwira na Kabulo

inatengenezwa haraka sana ili mwekezaji huyu sasa hivi aanze kufanya kazi bila matatizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya. Ni mama ambaye yuko makini, anafuatilia sana majukumu yake ya kuwawakilisha wananchi wa Ileje kama Mbunge. Ni kweli mama huyu amejitosheleza sana katika jimbo hilo, Mungu ambariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni kwamba je, Mradi huu wa Kiwira tumeuondoa katika miradi ya kimkakati? Jibu jepesi kabisa na la haraka ni kwamba bado mradi huu tunautambua kwamba ni mradi wa kimkakati ikiwa ni pamoja na miradi mingine mikubwa ambayo kwa kweli tunafahamu kama Serikali kwamba miradi ya kimkakati ni ile miradi mikubwa ambayo inawezesha miradi mingine au sekta nyingine kufanya kazi. Na kwa sababu sasa hivi tunataka nchi yetu iende katika kuwa nchi ya viwanda, makaa ya mawe ni kitu muhimu sana katika uendelezaji wa viwanda vyetu na hasa viwanda vya simenti. Kwa hiyo, mradi huu bado ni mradi wa kimkakati tunautambua kama miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini sasa Serikali tutaiwezesha kujenga barabara hii ya Kiwira – Kabulo. Sisi kwa kushirikiana na *TARURA,* Wizara ya Madini tumekwishawaandikia *TARURA* barua ya kuhakikisha kwamba kilometa zile saba zinajengwa katika mradi huu ili kupunguza kilometa 36 ambapo mwekezaji huyu anatumia kwa maana ya kupeleka kusafirisha makaa ya mawe, inaingiza gharama kubwa kwa sababu tunatambua kuwa makaa ya mawe ni *bulky mineral,* ni mzigo mkubwa. Kwa hiyo unapoweka katika hali ya kusafirisha mwendo mrefu gharama inakuwa ni kubwa na mtumiaji wa mwisho analipa gharama kubwa kiasi kwamba inamfanya huyu mwekezaji apate shida katika kuendeleza mradi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumelitambua hilo na imetengwa shilingi bilioni 2.5 ya kujenga kilometa saba na vilevile imetengwa bilioni 1.5 ya kujenga daraja ambalo liko pale.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, sisi tunaendelea kulisimamia na sisi kama Wizara ya Madini tunahakikisha kwamba tuko pamoja na Serikali kuwawezesha wawekezaji wote katika sekta ya madini wafanye kazi kwa faida na wasifanye kazi kwa hasara. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini. Maswali yetu yameishia hapo kwa siku ya leo, sasa ni wakati wa matangazo.

Tutaanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii na tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika, kuna wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambao ni Mheshimiwa Mihayo Juma N'hunga, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, karibu sana Naibu Waziri wetu. Mwingine ni Ndugu Shaaban Mohammed, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, karibuni sana katika Bunge letu Waheshimiwa. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; mgeni wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Mbunge, Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi ambaye ni mwanafunzi kutoka Chuo cha Uhasibu cha Jijini Dar es Salaam, Ndugu Ashraf Mlawa, karibu sana mwanafunzi wetu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wanane wa Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mbunge, ambao ni wanachama wa *Uhuru Veterans Sports Club,* Tabora wakiongozwa na Ndugu Mesiack Mungaya, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge ambaye ni mtoto wake, Ndugu Raphael

Alex Gashaza, karibu sana mtoto wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 66 na walimu 11 kutoka Shule ya Awali na Msingi ya *Holy Trinity* ya hapa Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yafuatayo mengine ni matangazo; Waheshimiwa Wabunge wanatangaziwa kuwa kesho, Siku ya Jumamosi, tarehe 8 Septemba, 2018 kwenye Uwanja wa Jamhuri kutakuwa na mechi ya kirafiki kati ya *Bunge Sports Club* na *Uhuru Veterans* ya Tabora kwa michezo ya *football* na *netball* kuanzia saa tisa alasiri, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote mnakaribishwa.

Tangazo lingine ni kwamba kesho, Jumamosi, tarehe 8, Septemba, 2018 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote itakayotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Benki Kuu ya Tanzania kuhusu masuala ya uchumi na majukumu ya Benki Kuu Tanzania. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 4.30 asubuhi. Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hiyo muhimu.

Tangaza lingine ni Waheshimiwa Wabunge wanaarifiwa kwamba Siku ya Jumapili, tarehe 9 Septemba, 2018, kutakuwa na semina kwa Wabunge wote itakayotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu uelewa wa masuala ya haki na fursa kwa watu wenye ulemavu. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa tano asubuhi, Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hii muhimu.

Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa pia kwamba Siku ya Jumatatu, tarehe 10 Septemba, 2018 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote itakayotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania kuhusu kazi na shughuli za taasisi hiyo. Semina hii itaambatana na

uzinduzi wa filamu ya biashara kwa lugha ya Kiswahili yenye maudhui ya kuelimisha umma kuhusiana na mapambano dhidi ya rushwa. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa saba mchana, Wabunge wote mnaomba kuhudhuria semina hiyo muhimu.

Katibu tuendelee.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mwongozo wa Spika.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Mwongozo nitapokea mmoja huku Mheshimiwa Maftaha na Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) na kwa sababu ya muda naomba nisiisome. Leo hii wakati naingia kwenye viwanja vya Bunge, ndani ya majengo ya Bunge nilipigiwa simu na viongozi wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kutoka Chemba. Wamenishtua sana mpaka nikashindwa kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge sawasawa baada ya kunipa taarifa kwamba Mkuu wa Wilaya ya Chemba amekuwa anafanya mwendelezo wa kuwafukuza Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wa Chama cha Wananchi *(CUF)* na siku ya jana pia kafukuza Mwenykiti mwingine wa tano, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Chama cha Wananchi *(CUF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba mwongozo wako kwamba huyu Mkuu wa Wilaya ya Chemba yeye kazi yake ni kufukuza Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wa *CUF* na siyo wa CCM wala chama kingine. Nilikuwa naomba nipate mwongozo wako, kazi yake ndiyo kazi mabayo Mheshimiwa Rais kamteua ili kumuweka wape ili afukuze viongozi wa *CUF?* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako chini ya kifungu 68(7) kuhusu swali namba 43 linalohusu Kiwanda cha Sukari cha Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa bei ya sukari ni shilingi kilo moja ni shilingi 2600 mpaka shilingi 3000 na Kiwanda cha Kagera juzi nilikuwa naangalia *tv* sukari imejaa haijauzwa mahali popote watu wanapata taabu bei inaendelea kupanda na Mheshimiwa Waziri alivyojibu swali anasema kuna suala la jinai, sijui kuna kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, mimi nauliza hivi bei iendelee kupanda kwa sababu hiyo kesi mpaka iishe? Hili si kuwatesa wananchi wa Tanzania, kwa nini bei ya sukari isishuke mpaka shilingi 2000?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lubeleje, mwongozo wa Mheshimiwa Maftaha kuhusu taarifa ya Mkuu wa Wilaya ya Chemba, kwa vile hatuna taarifa hiyo na kwamba hiyo siyo kazi yake kufukuza watu. Kwa hiyo, naamini Serikali imesikia na itaenda kufuatalia suala hili na kujua kama kuna ukweli wa jambo hilo na kuweza kuchukua hatua zinazotakiwa.

Kuhusu swali la Mheshimiwa Lubeleje pia Serikali itakuja na jibu hapo baadae, Katibu tuendelee.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa mwaka 2018 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 2) Bill, 2018)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Sasa tunamkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ili aweze kuja kuwasilisha Muswada kwa dakika 30.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya (86) ya kanuni za kudumu za Bunge toleo la 2016, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa mwaka 2018 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill (No.2) of 2018)* kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho sasa usomwe mara ya pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe Muswada huu kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani; kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, naomba nianze kwa kumshuru Mwenyezi Mungu rahimu mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhai, kujalia afya njema na kutuwezesha kutekeza majukumu yetu kwa ufanisi. Nichukue fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kutekeleza majukumu ya Waziri wa Katiba na Sheria, namuaidi kuwa nitaendelea kuitumikia nchi yangu kwa uzalendo, weledi kwa akili na uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi na Watumishi wote wa Serikali kwa kuendelea kutimiza na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Sisi sote ni mashaidi wa juhudi kubwa anazozifanya Mheshimiwa Rais na viongozi wake wakuu kuhakikishia kuwa nchi yetu inaendeshwa kwa misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na uwajibikaji chini ya uongozi wao mahili tunaendelea kupata mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali. Niwatakie viongozi wetu wakuu kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge hili tukufu, Katibu wa Bunge, Makatibu wa Kamati na watendaji wengine wa Bunge kwa msahada na ushirikiano mkubwa muliotoa ambao umewezesha Kamati ya Katiba na Sheria kutekeleza majukumu yake ndani ya muda uliopangwa. Nalipongeza Bunge lako tukufu kwa

kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wake wa kikatiba wa kutunga sheria. Lakini pia wa kuishauri na kuisimamia Serikali inapotekeleza majukumu yake ya kikatiba. Kwa ujumla napenda kuwashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoipatia Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Muswada uliopo mbele ya Bunge lako tukufu kwa namna ya kipekee, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kuujadili Muswada huu. Maoni ambayo Kamati hii iliipatia Serikali kwa kiasi kikubwa yameiwezesha Wizara kuboresha maudhui ya Muswada huu wa sheria

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 2 wa mwaka 2018 *(The Writen Laws MiscellaneousAmendments Bill No. 2 of 2018)* unapendekeza kufanya marekebisho katika sehemu 13. Marekebisho yanayopendekezwa kwenye Muswada huu yana lengo la kuiwisha sheria kadhaa ili kuendana na mabadiliko yaliyotokea katika sekta ya sheria. Muswada huu unalenga kuweka masharti yatokanayo na mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuanzishwa kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Hati Idhini za Rais kupitia matangazo ya Serikali namba 48, 49 na 50 ya terehe 13 Februari, 2018. Aidha, mapendekezo ya sheria nyingine yanalenga kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kitaasisi katika maeneo mbalimbali ya kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala muhimu yanayozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na kubadilisha vifungu vya sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu vya sheria hizo na kuviandika upya, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipya. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(1) Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu, Mamlaka na Utekelezaji wa Majukumu Sura ya 27 *(The Administrator General Powers and Functions Act Cap. 27);*

(2) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20 yaani *Criminal Procedure Act Cap. 20;*

(3) Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu Sura ya 368 yaani *The Extradition Act Cap. 368;*

(4) Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza yaani *Interpretation of Laws Act Cap 1;*

(5) Sheria ya Ukomo Sura ya 89 *(The Laws of Limitation Act Cap. 89;*

(6) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania Sura ya 171 *(The Laws Reform Commission of Tanzania Act Cap. 171);*

(7) Sheria ya Mashirikiano katika Masuala ya Jinai Sura ya 256 yaani *The Mutual Assistance in Criminal matters Act Cap. 256;*

(8) Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mastaka Sura ya 430 yaani *The Nation Prosecution Services Act Cap. 430);*

(9) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Sura ya 268 yaani *The Office of the Attorney General Discharge of Duties Act Cap. 268);*

(10) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 *(The Prevention and Combating of Corruption Act Cap. 329);*

(11)Sheria ya Kuzuia Ugaidi Sura ya 19 *(The Prevention of Terrorism Act Cap. 19);*

(12) Sheria ya Mapato ya Uhalifu Sura ya 256 yaani *The Proceeds of Crime Act Cap. 256;* na

(13) Sheria ya Chama cha Wanasheria wa Tanganyika Sura ya 307 yaani *The Tanzania Laws Society Act Cap. 307.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya muswada huu ni kuimarisha utendaji wa Taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuondoa mwingiliano wa majukumu ya kitaasisi, kuuhisha, miundo ya baadhi ya taasisi ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa makujumu ya taasisi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 14, sehemu ya kwanza ya Muswada inaainisha masharti ya awali ambalo ni jina la Muswada na tamko kuhusu sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zilivyopangiwa katika sehemu zake mtawalia yaani Mtawalia maana yake *respectively.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inapendekeza kurekebisha kifungu cha pili cha Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu, mamlaka na utekelezaji wa majukumu Sura ya 27 kwa lengo la kuoanisha masharti ya sheria hiyo na masharti ya sheria ya Wakala za Serikali Sura ya 245 na pia kuanzisha nafasi mpya ya Naibu Kabidhi Wasii Mkuu ambaye atakuwa Afisa Masuhuli wa Wawakala wa usajili, ufilisi na udhamini *(RITA).* Sehemu hii ya Muswada inapendekeza pia kufanya marekebisho katika kifungu cha (4) cha sheria hiyo na kuweka masharti yatakayowezesha uteuzi wa Kabidhiwa Wasii Mkuu kufanywa na Rais badala ya Waziri kama inavyotekelezwa katika sheria ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za mapendekezo hayo ni kutokana nauzito wa majukumu na mamlaka ya Kabidhiwa Wasii Mkuu. Hadhi ya Ofisi yake na nafasi yake Mahakamani kwa majibu wa kifungu cha 4(3) cha sheria hiyo Muswada unaweka masharti kuhusu sifa za mtu anayestahili kuwa Kabidhi Wasii Mkuu na Naibu Kabidhiwa Wasii Mkuu ili kutoa mwongozo kwa mamlaka ya uteuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Mwenendo

wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20. Marekebisho yanayopendekezwa ni kuandika upya tafsiri ya maneno *public prosecutor* kwa lengo la kuwezesha utekelezaji bora wa sheria hiyo kwa kuzingatia kuanzishwa kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Aidha Muswada unapendekeza kurekebisha kifungu cha 57 kwa kuongeza masharti yatakayowezesha wapelelezi au wachukunguzi kufanya mahojiano kwa kutumia vifaa vya sauti au vya kidijitali na kwaba Jaji Mkuu atatunga kanuni kwa ajili utekelezaji bora wa masharti hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii inapendekeza pia kurekebisha kifungu cha 73 kwa kujumuisha makosa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ya mwaka 2015 katika orodha ya makosa ambayo Mahakama inaweza kutoa amri kwamba mtuhumiwa aendelee kushikiliwa. Marekebisho haya yanalenga kuviwezeshwa vyombo vya uchunguzi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Aidha, kifungu cha 169 cha sheria hiyo kinarekebishwa kwa kuimarisha vigezo ambavyo Mahakama inapaswa kuvitumia kabla ya kufuta ushahidi ambao unadaiwa kukusanywa kwa ukiukaji wa taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 188 cha sheria hiyo kinarekebishwa kwa lengo la kuainisha masharti ambayo yatatoa ulinzi kwa mashahidi wanaoitwa kutoa ushahidi wao Mahakamani, iwapo Mkurugenzi wa Mashtaka atafungua maombi kwa ajili hiyo. Ulinzi unaotajwa katika sheria ya sasa unahusu kutotaja majina yao kwenye magazeti. Muswada unapendekeza pia kufanya marekebisho ya kifungu cha 205 cha sheria hiyo kwa kuongeza kifungu kipya cha 205A kinachoainisha masharti kuhusu kupokelewa taarifa za wataalamu kama ushahidi Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Urejeshwaji Wahalifu Sura ya 368. Sheria ya sasa inaelekeza pamoja na mambo na mengine kuwa muhalifu arejeshwe katika ambayo alitenda kosa baada ya kupita siku 15 tangu Mahakama kutoa amri ya kurejeshwa. Muswada unapendekeza marekebisho ya vifungu vya 9 na 16 vya sheria

hiyo kwa kuondoa masharti hayo na hivyo kumpatia Waziri mwenye dhamana ya urejeshwaji wa wawahalifu, mamlaka ya kuwarejesha wahalifu pindi Mahakama inapotoa amri hiyo. Marekebisho haya yataimarisha zaidi utaratibu wa urejeshwaji wahalifu

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ya Muswada huu inahusu marekebisho katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza kwa kutoa tafsiri mpya ya maneno Maafisa wa Sheria ili iwiane na marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ulioainishwa katika Hati Idhini ya Rais ambayo ilichapishwa katika Tangazo la Serikali namba 48 la tarehe 13 Frebuari, 2018. Vilevile marekebisho haya yanapendekeza kuwajumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka, Kabidhi Wasii Mkuu na Wakili Mkuu wa Serikali au Waendesha Mashtaka wenye cheo kuanzia Wakili wa Serikali Mkuu katika tafsiri ya maneno Maafisa wa Sheria yaani *Laws Officer's.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii inapendekeza pia kurebisha tafsiri ya maneno Katibu Mkuu kwa kumuondoa Naibu Mwanasheria Mkuu kwa kuwa katika muundo wa Wizara ya Katiba na Sheria hapo awali Naibu Mwanasheria Mkuu pia alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara. Hivi Naibu Mwanasheria Mkuu ni msaidizi Mkuu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aidha, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana jukumu la kuwashauri Makatibu Wakuu wanapokutana kujadili masuala mbalimbali katika vikao vya Kamati za Makatibu Wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita ya Muswada inapendekeza kurekesha Sheria ya Ukomo Sura ya 89 kifungu cha 44 kinampatia Waziri mwenye dhamana ya sheria mamlaka ya kuongeza ukomo wa muda wa kufungua shauri Mahakamani. Muswada unapendekeza kifungu hicho kirebishwe kwa kuongeza masharti ambayo yatamwezesha Waziri kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa mamlaka ya kuongeza muda wa kufungua mashauri ya madai nje ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu vya 2, 4, 5, 6, 7, 8, 14,19 na 22 vya Sheria ya Tume ya Kurebisha Sheria Sura ya 171. Marekebisho hayo yanalenga kuongeza tija na kuimarisha utendaji wa Tume na kuendana na mabadiliko mbalimbali ambayo hutokea katika jamii. Aidha, marekebisho haya yanalenga kuweka masuala ya kisera chini ya usimamizi wa Waziri mwenye dhamana na mambo ya sheria badala ya kufanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mashirikiano katika Masuala ya Jinai Sura ya 254 kwa kuboresha mfumo wa kisheria kuhusu ushirikiano katika masuala ya jinai na nchi nyingine, Mkurugenzi wa Mashtaka anapewa mamlaka ya kughulikia maombi ya nyaraka za upelelezi za ndani na nje ya nchi na kumpatia majukumu ya masuala anayotakiwa kufanya kwa mujibu wa sheria.

Aidha, kifungu cha pili cha sheria hiyo kinarekebishwa kwa kufuta tafsiri ya maneno yafuatayo *foreign specified offence, interdict* na *specified offence*, kuboresha tafsiri ya maneno *serious offence* na kuongeza tafsiri mpya ya maneno *foreign serious offence* na *restrend.* Marekebisho haya yanalenga kuboresha utekelezaji bora wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4 cha sheria hiyo kinarekebishwa kwa lengo la kuongeza wigo na aina ya msaada ambao unaweza kuombwa nje ya nchi ikiwemo matumizi ya mifumo ya mawasiliano na *computer* inapobidi. Aidha, kifungu cha 9 kinarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 9(a), 9(b) na na 9(c) ambavyo vinaainisha masharti kuhusu usiri, lugha na gharama katika kushughulikia maombi ya ushirikiano katika masuala ya jinai, pia Muswada unapendekeza kurekebisha kifungu cha 11 kwa kuweka utaratibu mbadala wa kuchukua maelezo ya shahidi kwa njia ya kiapo bila kulazimika maelezo hayo kuchukuliwa mbele ya Mahakimu kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 11(2) cha sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unapendekeza pia kufanya marekebisho katika kifungu cha 32 cha sheria hiyo kwa lengo la kuwezesha mali zilizopatikana isivyo halali kurejeshwa bila ya kucheleweshwa. Aidha, sehemu hii inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 38(a), 38(b) na 38(c) kwa lengo la kupokea maelezo na uthibitisho wa nyaraka na viapo. Hivi sasa sheria haina masharti kuhusu namna kupokea maelezo na uthibitisho wa ushahidi zaidi ya nyaraka. Maelezo ya mashaidi na viapo ni miongoni mwa masuala yanayoweza kutumika kama ushahidi katika mazingira ambayo shahidi aliye nje ya nchi haweze kuja Tanzania kwa lengo la kutoa ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tisa ya Muswada inapendekeza, kufanya marekebisho katika Sheria ya Taifa ya Mashtaka Sura ya 430 kwa kuondoa masharti yaliyokuwa yakiipa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka kuhusu uendeshaji wa mashtaka na kuisimamia kiutawa Ofisi ya Taifa ya mashtaka. Mapendekezo hayo ni matokeo ya mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuanzishwa kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inayojitegemea. Pia Muswada unapendekeza kurekisha kifungu cha 27 na kurekebisha muundo wa Jukwaa la Taifa la Haki Jinai. Aidha Muswada unapendekeza kuongeza vifungu vingine vipya vya 27(a), 27(b) na 27(c) ambavyo vinaainisha masharti kuhusu Kamati ya Haki Jinai ya Mawaziri, Jukwaa la Haki Jinai la Mkoa na Jukwaa la Haki Jinai la Wilaya Mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Haki Jinai ya Mawaziri itakuwa na jukumu la kutoa mwongozo wa kisera na maelekezo ya mwenendo wa haki jinai, wakati Kamati ya Haki Jinai ya Mkoa na Jukwaa la Haki Jinai la Wilaya zitakuwa na jukumu la kujadili masuala ya kimkakati ya haki jinai katika Mkoa au Wilaya husika. Marekebisho yanalenga kuboresha usimamizi wa mfumo wa haki jinai nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Sura ya 268 kwa ujumla

marekebisho katika sehemu hii yanalenga kuoanisha masharti ya sheria hiyo na muundo mpya wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Hati Idhini ya Rais. Hivyo Muswada unapendekeza kuondoa majukumu ya uendeshaji wa mashtaka ya jinai na usimamizi wa masuala ya ufirisi chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na badala yake majukumu yao yatekelezwe na taasisi husika zilizoanzishwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, katika marekebisho haya masuala masuala ya kuendesha na kusimamia mashauri ya madai yameondolewa chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuweka chini ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho hayo yanalenga pia kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kujikita katika jukumu lake kuu la kutoa ushauri wa kisheria kama inavyoelekweza katika Ibara ya 59 ya Katiba. Pia Ofisi hii itakuwa na jukumu la kuandika miswada ya sheria na kuwasimamia Wanasheria wote walio katika utumishi umma nje ya wale walio katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Marekebisho yataimarisha utendaji na mahusiano baina ya taasisi za Serikali na kuongeza ufanisi wa utendaji kwa maslahi na maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 11 inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329; kifungu cha 34 cha sheria hiyo kinampatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali mamlaka ya kutoa hati zuio yaani *prohibitory notice* la kuhamisha mali yoyote baada ya kuridhika kuwa mali hiyo iilipatikana kwa njia ya rushwa. Kwa kuzingatia kuwa masuala ya jinai yanasimamiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka, Muswada unapendekeza kifungu hicho kirekebishwe ili hati idhini, hati ya zuio la kuhamisha mali iwe inatolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 12 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ugaidi Sura ya 19; kifungu cha 34 cha sheria hiyo kinarekebishwa kwa kuweka masharti yatakayomwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua maombi chini kifungu cha 188 cha Sheria

ya Uendeshaji wa Mashauri ya Jinai kwa ajili ya kulinda mashahidi na kutumia teknolojia katika uendeshaji wa mashauri ya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 13 inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Urejeshwaji wa Mali Zitokanazo na Uhalifu Sura ya 256. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha mfumo wa kisheria kwa kuhakikisha kuwa wahalifu hawafaidiki kutokana na mali walizozipata kwa njia za uhalifu; hatua hii itawezesha kuzuia uhalifu nchini kwa kuwa watuhumiwa wataona kuwa uharifu haulipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 3 cha sheria hiyo kinarekebishwa kwa kuboresha tafsiri ya maneno *serious offence* ili itumike pia kwa makosa mengine yote makubwa yanayozalisha kipato. Tafsiri ya sasa haijumuishi makosa yote ya jinai ambayo yanaweze kusababisha faida kama vile makosa yahusuyo wanyapori na makosa ya kodi. Vilevile sehemu hii inapendekeza kurekebisha kifungu cha 31 cha sheria kwa kuongeza vifungu vipya vya 31(a) 31(b) na 31(c) ambavyo vinaweka masharti kuhusu kuzuia akaunti ya benki, ukusanyaji wa taarifa au nyaraka kuhusu mali na utoaji wa taarifa za kiuchunguzi mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuviwezesha vyombo vya uchunguzi kupata taarifa inayoweza kusaidia katika uchunguzi na kuzuia utoaji wa taarifa ambazo zinaweza kuathiri uchunguzi wa mali itokanayo na uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii Muswada ina inapendekeza pia kurekebisha kifungu cha 38(1) kuweka masharti yatayomwezesha Mkurugenzi wa mashtaka kuwasilisha Mahakamani maombi ya upande mmoja yaani *exparte application* ya kukamata mali inayopatikana kwa njia za uhalifu na ambayo ipo hatarini kupotea au kuharibika, aidha kifungu kidogo cha 6 kimeongezwa katika Kifungu hicho ili kuiwezesha Mahakama kutoa amri ya kutaifisha au kuuza mali iliyokamatwa na ambayo inaharibika upesi au ile ambayo utunzaji wake ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 14 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, Sura ya 307 kwa kuweka vigezo ambavyo vitatumika kupata Wajumbe wa Baraza na taratibu za kufuatwa wakati wa utungaji wa Kanuni zinazosimamia chama hicho. Mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii yanalenga kuweka masharti ya kumtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuzipitisha kanuni zilizotungwa na baraza la Chama kabla ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. Lengo la marekebishao haya ni kumpatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali fursa ya kuangalia kama Kanuni husika zimezingatia masharti ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maelezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 2 ya mwaka 2018 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill No. 2 of 2018)* na ninaomba Bunge lako tukufu liujadili na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na mara ya tatu ili hatimaye uwe sehemu ya sheria za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ili aweze kuja kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati, Makamu Mwenyekiti kwa niaba, Dkt. Ndumbaro, karibu.

**MHE.DKT. DAMAS D. NDUMBARO - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016 naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 2 wa mwaka 2018 yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill No. 2 of 2018.* Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Agosti, 2018 Kamati ilipokea maoni ya wadau mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Jumla ya wadau 12 kutoka kwenye taasisi mbalimbali waliwasilisha maoni yao kwa kufika mbele ya Kmati na au kwa njia ya maandishi kupitia Ofisi ya Katibu wa Bunge. Hivyo napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao kwa nyakati tofauti waliwasilisha maoni yao mbele ya Kamati na wengine waliwasilisha kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia masuala ya awali katika utangulizi wa taarifa hii, napenda kuwasilisha katika Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ambayo yametokana na maelezo ya Serikali pamoja na uchambuzi wa Kamati katika sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada na ambavyo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa 2018 kupitia Hati Idhini iliyochapishwa katika Matangazo ya Serikali namba 48, 49 na 50 ya tarehe 13 Februari, 2018 Serikali ilifanya mabadiliko katika mfumo wa kisheria yaani *legal regime* nchini yenye kuweka au kuanzisha mfumo mpya wa uwakilishi na utetezi wa Serikali na taasisi zake zote katika masuala ya kisheria ndani na nje ya nchi. Kutokana na mabadiliko hayo, mfumo wa sekta ya sheria nchini kupitia ofisi mbalimbali za kiusimamizi na kiutekelezaji zilihitaji kufanyiwa marekebisho ili kuzingatia mabadiliko hayo ya kimfumo kwa lengo la kuondoa changamoto za kiutendaji miongoni mwa taasisi husika kupitia vifungu mbalimbali vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa muswada; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 2 wa mwaka 2018 una jumla ya Ibara 108 ambazo zinapendekeza kufanya mabadiliko katika sheria 13 kama zilivyoorodheshwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza ya muswada; sehemu hii inaainisha masharti ya awali ya muswada kama ifuatavyo:-

(a) Ibara ya Kwanza inabainisha jina fupi la sheria hii ambalo ni *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, 2018.* Muswada huu utakapotungwa kuwa sheria, ibara hii ndiyo itakayotoa jina sahihi ambalo litatumika katika rejea mbalimbali za kisheria na rejea nyinginezo.

(b) Ibara ya Pili inaonesha namna sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho zitakavyorekebishwa katika sehemu za muswada zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii Kamati iliridhia marekebisho ya Serikali kama yalivyopendekezwa. Sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya inapendekezwa zaidi na muswada huu kuwa Kabidhi Wasii Mkuu apewe mamlaka ya kuandaa kanuni za kudumu na nyaraka nyingine za kisheria kwa ajili ya uendeshaji bora wa *RITA.*

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati katika pendekezo hili ni kuwa muswada uboreshwe zaidi ili hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma kwa sababu watumishi wa *RITA* ni sawa na watumishi wengine wa Umma ambao tayari wanawajibishwa na Kanuni za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya muswada; sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 yaani *Criminal Procedure Act, Cap. 20* ambayo inaweka utaratibu unaopaswa kufuatwa katika uchunguzi na uendeshaji wa makosa ya jinai. Ibara ya 8 ya muswada inapendekeza marekebisho ya kifungu cha pili cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinachohusu tafsiri ya maneno na misamiati mbalimbali kwa kuboresha tafsiri ya Mwendesha Mashtaka. Tafsiri hiyo inapendekezwa kuboreshwa ili kuzingatia marekebisho yanayofanyika katika muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 9 inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 57 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinachohusu utaratibu wa kurekodi mahojiano kwa kuweka masharti mapya yanayopaswa kuzingatiwa na polisi yeyote anapokuwa anarekodi mahojiano kati yake na mtu yeyote kwa njia ya sauti au video.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara za 10 inafanya Maboresho ya kifungu cha 73 kinachohusu dhamana inayopaswa kuwekwa na wahalifu wazoefu kwa kujumuisha makosa ya madawa ya kulevya katika orodha ya makosa yaliyoainishwa. Marekebisho haya yataiwezesha Mahakama kumuamuru mhalifu mzoefu yaani *habitual offender* katika madawa ya kulevya kuweka dhamana au *bond* ikiambatana na wadhamini kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu ambacho atatakiwa awe amebadilika na kuwa na mwenendo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 11 inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 169 kinachohusu taratibu za Mahakama kupokea ushahidi ambao umepatikana kinyume na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 12 inapendekeza kufuta kifungu cha 188 kinachohusu mamlaka ya mahakama kuzuia uchapishaji wa majina ya mashahidi kwenye vyombo vya habari na kuandika upya. Kifungu kipya kinachopendekezwa kinampa Mkurugenzi wa Mashtaka

mamlaka ya kupeleka maombi Mahakamani kwa ajili ya kupokea ushahidi kwa njia ya video pamoja na kuzuia mashahidi au nyaraka zinazoweza kusababisha mashahidi hao kufahamika kwa sababu za usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 205A kinachohusu upokeaji wa ushahidi wa wataalamu na uchunguzi wa mitandao ya teknolojia, silaha, milipuko na utaalamu mwingine wowote.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vitendo vya uhalifu vimezidi kuongezeka kwa kasi duniani, ni jambo zuri kwa Mamlaka za udhibiti wa makosa ya kijinai kuanzisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika uchunguzi ili kupanua wigo wa udhibiti wa makosa ya kiuhalifu na kuongeza ufanisi kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ya muswada; sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu, Sura ya 368 yaani *Extradition Act, Cap. 368* ambayo inayohusu mahusiano ya kimataifa katika urejeshwajiwa wahalifu katika nchi walikotenda makosa. Muswada huu unapendekeza kuifanyia marekebisho sheria hii kupitia Ibara za 14 hadi 17 za sheria ili kuboresha utaratibu wa urejeshwaji wa wahalifu hususani kwa kuondoa matakwa ya mfungwa anayetakiwa kurejeshwa katika nchi alikotenda kosa kukaa kizuizini kwa siku 15 kabla Waziri hajaidhinisha urejeshwaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika hili, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yana lengo la kurahisisha utoaji haki jinai kati ya taifa letu na mataifa mengine katika kudhibiti vitendo vya kiuhalifu kwa kuzingatia matakwa ya sheria hii ya mahusiano ya kimataifa katika urejeshwaji wa wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ya muswada; sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya kwanza yaani *The Interpretation of Laws Act, Cap. 1.* Sheria hii inahusu

majumuisho ya kanuni za msingi zinazohusu maana, ufafanuzi na matumizi ya sheria zilizotungwa, na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Ibara za 18 na 19 za muswada kwa kuboresha tafsiri ya maneno Afisa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo kwa sababu yanafanyika ili kuendana na marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu nchini na Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu kama inavyoainishwa katika Hati Idhini husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita ya muswada; sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Ukomo, Sura ya 89 yaani *The Law of Limitation Act, Cap. 89* ambayo inaweka ukomo wa muda wa kufungua mashauri ya madai Mahakamani.

Mheshmiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuondoa sharti hilo la kiufundi yaani *legal technicality* kwani limekuwa likisababisha Serikali kushindwa mashauri mbalimbali ambayo hata kama ina ushahidi na vigezo vya kutosha vya kushinda lakini inapoteza mashauri ya madai kwa sharti la kigezo la muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kuwa maboresho yataongeza wigo wa Serikali kuwa na nafasi nzuri ya kushinda mashauri mengi ya madai hususani mashauri yanayotokana na mikataba ya rasilimali za nchi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na hujuma mbalimbali zinazoweza kufanyika kwa kutumia kigezo cha muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba ya muswada; sehemu hii ya muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171 yaani *The Law Reform Commission of Tanzania Act, Cap. 171.* Sheria hii inayoanzisha na kuainisha majukumu pamoja na mamlaka ya Tume ya Kurekebisha Sheria nchini inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(i) Kumpa Waziri mwenye dhamana ya mambo ya sheria mamlaka ya kutekeleza mambo mbalimbali kuhusu Tume;

(ii) Kuongeza wigo wa majukumu ya Tume;

(iii) Kurekebisha utendaji kazi wa Kamishna wa Tume;

(iv) Kufanya marekebisho ya kifungu cha sita kinachohusu masharti ya muda wa Makamishina kuwa madarakani; na

(v) Kuipa Tume mamlaka ya kuanza kutekeleza kazi zake yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kutumia mapendekezo ya maboresho ya sheria hii kwa kutekeleza maoni ya Kamati ya muda mrefu kuhusu kuboresha na kuimarisha mfumo wa Tume ya Kutunga Sheria katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ikiwa ni pamoja na kuainisha muda wa utumishi wa Makamishna wa Tume kwa lengo la kuimarisha nidhamu ya Utumishi katika Tume hii muhimu katika sekta ya sheria nchini.

Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa maboresho haya, yataongeza uhuru wa Tume na kupunguza mlolongo wa taratibu za kiutendaji zisizo za lazima yaani *bureaucracy* katika kufanya maamuzi pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane ya muswada; sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai, Sura ya 256. Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai, Sura ya 256 yaani *The Mutual Assistance in Criminal Matters Act* ni sheria mahsusi kwa ajili ya kuwezesha ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine katika masuala ya jinai.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yana lengo la kuboresha na kuimarisha

mfumo wa Kisheria katika ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine katika masuala ya jinai. Hii ni pamoja na kutambua matumizi ya teknolojia katika uhakiki nyaraka na ushahidi ili kuendana na nchini nyingine katika kushughulikia masuala ya Kijinai kati ya Tanzania na nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tisa ya muswada; sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430. Kimsingi sheria hii inarekebishwa ili kuondoa vipengele vinavyowezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushughulika na masuala ya uendeshaji wa mashtaka na kuisimamia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho ya vifungu mbalimbali ikiwemo:-

(a) Kupendekeza maboresho katika kifungu cha 3 kwa kutoa tafsiri ya maneno Afisa Sheria yaani *Law Officer.*

(b) Kuongeza vifungu vipya vya 27A na 27B vinavyoanzisha Kamati ya Mawaziri ya Haki Jinai na Jukwaa la Haki Jinai ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yana lengo la kuboresha na kuimarisha Ofisi ya Usimamizi na Udhibiti wa Makosa ya Jinai nchini ili kuendana na mabadiliko ya mfumo wa kisheria nchini kwa mujibu wa Hati Idhini iliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni pamoja na kuboresha na kuimarisha muundo wa Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka nchini, kutenganisha masuala ya utawala na majukumu ya usimamizi wa mashtaka pamoja na kuainisha mfumo thabiti wa kibajeti na udhibiti wa rasilimali fedha katika ofisi hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi ya muswada; sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, utekelezaji wa majukumu yake Sura ya 268. Kimsingi sheria hii

inarekebishwa ili kuendana na muundo mpya wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Hati Idhini iliyotolewa na Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa nia nzuri ya kuimarisha misingi ya nidhamu ya taaluma ya sheria nchini kupitia mapendekezo haya, hata hivyo Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali. Kwa kuzingatia sababu hizo kama zilizovyoainishwa hapo juu, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yana lengo nzuri la kuboresha mfumo wa sheria nchini kwa manufaa ya wana taaluma wenyewe, Serikali, jamii ya Watanzania kwa ujumla na kwa ustawi wa taaluma ya sheria hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 11 ya muswada, sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Ibara ya 89 ya muswada ambayo inarekebisha kifungu cha 34 cha sheria hiyo kinachohusu uhamishaji wa mali zitokanazo na uhalifu ili kuondoa maneno "Mwanasheria Mkuu wa Serikali" na badala yake kumuweka "Mkurugenzi wa Mashtaka."

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati inaridhia marekebisho haya kwa kuwa yanaendana na maboresho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Hati Idhini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 12 ya muswada; sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Ibara ya 91 ya muswada ambayo inapendekeza kufuta kifungu cha 34(3) cha sheria kinachohusu uwezo wa Mahakama ya juu ya makosa yaliyobainishwa na kuandikwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaridhia marekebisho hayakwakuwa yana lengo la kuweka masharti ya matumizi ya teknolojia katika uendeshaji wa kesi za ugaidi

na pia kumlinda shahidi kwenye kesi hizo ili kuendana na hali halisi ya matumizi ya teknolojia duniani katika masuala ya udhibiti wa vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 13 ya muswada, sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Urejeshwaji wa Mali zitokanazo na Uhalifu, Sura ya 256. Mapendekezo ya marekebisho haya ni muhimu kwa sababu yana lengo la kuimarisha udhibiti wa mali zinazotokana na uhalifu kwa mujibu wa sheria ya urejeshaji wa mali zinazotokana na uhalifu pamoja na sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya 14 ya muswada, sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307. Ibara ya 106 inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 15 kinachohusu muundo wa Baraza. Vifungu vinavyoongezwa vinaweka sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza. Aidha, marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kutoruhusu wafuatao kugombea ujumbe wa Baraza; mtumishi wa umma, Diwani, Mbunge au Kiongozi wa Chama cha Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 107 inapendekeza kuongeza kifungu cha 15A kinachohusu kuzuia mjumbe wa Baraza kujihusisha na masuala ya kisiasa zilizoainishwa na sheria. Ibara ya 108 inapendekeza marekebisho kwa kufuta Kifungu cha 31 kinachohusu utungaji wa kanuni na kuandika upya. Marekebisho yanayopendekezwa ni utungwaji wa kanuni ufanywe na Baraza kwa kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kisha kanuni hizo zitatakiwa kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yana lengo la kuimarisha misingi ya nidhamu, vigezo na mipaka ya kitaaluma kwa Mawakili wa Kujitegemea pamoja na sifa stahiki kwa viongozi wa vyama vya Mawakili nchini, ili kuimarisha taswira ya taaluma ya sheria ndani na nje ya nchi yetu. Hii ni pamoja na kutofautisha majukumu ya chama cha taaluma ya sheria

na vyama vya siasa kwa lengo la kutenganisha taaluma na shughuli za kisiasa pamoja na masharti mengine kama ilivyoelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mahususi;

(a) Maboresho ya Ibara ya 67 kwa kuweka misingi ya kisheria ya kushughulikia masuala ya maadili kwa watumishi wa Ofisi ya Kabidhi Wasii.

(b)Maboresho ya Ibara ya 9 ili kuimarisha Uzingatiaji wa Haki za Mtuhumiwa wakati anafanyiwa Mahojiano.

(c) Maboresho ya Ibara ya 12 kwa kuondoa sharti la Mwendesha Mashtaka ya Serikali kusikilizwa peke yake *(ex-parte hearing)* katika maombi yanayowasilishwa Mahakamani kuhusu kuchukua Ushahidi kwa mikutano ya video.

(d) Marekebisho ya Ibara ya 58 kwa kuanzisha Jukwaa la Haki Jinai la Wilaya.

(e)Maboresho ya Ibara ya 72 kwa kuweka mfumo wa mawasiliano kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi za umma kuhusiana na hatua za kinidhamu zinazo chukuliwa dhidi ya wanasheria walioajiriwa katika taasisi hizo.

(f)Maboresho mbalimbali ya kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa jumla, Kamati imeshauriana na Serikali na kukubaliana kuyafanyia kazi kwa wakati muafaka maoni na mapendekezo mbalimbali:-

(a) Kuhuisha Sheria ya Chama cha Mawakili nchini**;** Kamati inaishauri Serikali ifanye tathmini sheria hiyo kwa lengo la kuihuisha hususan katika masuala yafuatayo:-

(i) Kubainisha na kutenganisha mamlaka na majukumu ya Baraza la *TLS* na Sekretarieti yake;

(ii) Kuboresha masharti ya Mkutano Mkuu wa *TLS;*

(iii) Kuboresha masharti yanayohusu fedha za *TLS;* na

(iv) Kuweka masharti kuhusu *Chapter* za chama hicho;

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naomba niwatambue na kuwashukuru wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii. Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuu watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji wa kazi wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa kamati naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA.2) WA MWAKA 2018*(THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.2) BILL, 2018*
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI:

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 26 Juni, 2018, wakati wa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2018[*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2018]* ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza. Baada ya hapo, Mheshimiwa Spika kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 84(1) pamoja na aya ya 7(1)(b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni

za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, uliupeleka Muswada huo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Hivyo, kwa masharti hayo, Kamati iliujadili Muswada huo kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) Wa Mwaka 2018*(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2018.* Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria 13 zifuatazo:-

(a) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu, Sura ya 27
(b) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20
(c) Sheria ya Kubadilishana Wafungwa, Sura ya 368
(d) Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1
(e) Sheria ya Ukomo, Sura ya 89
(f) Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171
(g) Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai, Sura ya 254
(h) Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430
(i) Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Utekelezaji wa Majukumu yake, Sura ya 268
(j) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329
(k) Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19
(l) Sheria ya Kuhusu Mali zitokanazo na Uhalifu, Sura ya 256
(m) Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307

### 1.1 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliketi kwa muda wa wiki mbili katika **Ukumbi Na.9** uliopo Jengo la Utawala katika Ofisi za Bunge Dodoma na kufanya yafuatayo:

**a) Tarehe 20 Agosti, 2018** Kamati ilifanya maandalizi mbalimbali ya kiutendaji kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati;

**b)** **Tarehe 21 Agosti, 2018** Kamati ilipokea na kujadili uchambuzi wa awali wa Sekretarieti ya Bunge kwa lengo la kupata uelewa wa Muswada husika kwa mujibu wa Kanuni ya 21 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2018;

**c)** **Tarehe 23 Agosti, 2018** Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu madhumuni na sababu za Muswada ambayo yaliwasilishwa na mtoa hoja ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi (Mb);

**d)** **Tarehe 24 Agosti, 2018** Kamati ilipokea maoni ya wadau mbalimbali kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada. Maoni haya ya wadau yalitokana na barua za mialiko ambazo zilitolewa na Ofisi ya Bunge pamoja na matangazo kwa umma ambayo yalitolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Jumla ya **wadau 12** kutoka kwenye taasisi zifuatazo walifika kwenye Kamati na kuwasilisha maoni yao:

(i) Chama cha Wanasheria Tanganyika (*Tanganyika Law Society – TLS*)
(ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (*Legal and Human Rights Centre – LHRC*),
(iii) TWAWEZA
(iv) SIKIKA,
(v) Hakielimu, na
(vi) *Stallion Attorneys.*

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao kwa nyakati tofauti, waliwasilisha maoni yao mbele ya Kamati na wengine waliowasilisha kwa maandishi.

**e)** **Tarehe 25 Agosti, 2018** Kamati ilifanya tathmini ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu;

**f)** **Tarehe 27 na 28 Agosti, 2018** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada kwa kuzingatia uchambuzi wa Sekretarieti YA Bunge, Maelezo ya Serikali, Maoni ya

wadau pamoja na rejea mbalimbali na hivyo kuiwezesha Kamati kuujadili Muswada ipasavyo. Hatua hii iliiwezesha Kamati kuandaa jedwali la mapendekezo ya marekebisho ambalo liliwasilishwa rasmi Serikalini kwa mujibu wa Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2018;

**g) Tarehe 29 na 30 Agosti, 2018** Kamati ilifanya mashauriano na Serikali kuhusu marekebisho yaliyopendekezwa na Kamati na kuwasilisha Serikalini. Mashauriano haya yalifanyika kwa mafanikio makubwa ambapo Serikali ilipokea ushauri wa Kamati na kuufanyia kazi kwa kukubali kuandaa jedwali la marekebisho ya Muswada. Jedwali hilo lina marekebisho mbalimbali kuhusu:

(i) Marekebisho ya kimaudhui katika baadhi ya ibara za muswada;

(ii) Baadhi ya ibara za Miswada zimebainika kuwa na dosari za kiuandishi na hivyo imependekezwa ziboreshwe;

(iii) Baadhi ya maneno yanapendekezwa kufutwa na au kuandikwa upya katika baadhi ya Ibara za Miswada; na

(iv) Mapendekezo ya kuongeza baadhi ya maneno yaliyosahaulika katika baadhi ya vifungu ili kuleta mantiki iliyokusudiwa katika kifungu husika.

**h) Tarehe 30 na 31 Agosti, 2018** kufanya tathmini pamoja na kuandaa Taarifa ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 85 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2018.

## 2.0 MAONI YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuzungumzia masuala ya awali katika utangulizi wa Taarifa hii, napenda kuwasilisha katika Bunge lako tukufu maoni ya Kamati ambayo yametokana na maelezo ya Serikali pamoja uchambuzi wa Kamati katika Sehemu na Ibara mbalimbali za Muswada na ambayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Serikali.

## 2.1 MAELEZO YA JUMLA YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka huu wa 2018, kupitia ***Hati Idhini iliyochapishwa katika Matangazo ya Serikali Na.48, 49 na 50 ya tarehe 13 Februari, 2018,*** Serikali ilifanya Mabadiliko katika Mfumo wa Kisheria *(Legal Regime)* nchini yenye kuweka au kuanzisha mfumo mpya wa uwakilishi na utetezi wa Serikali na taasisi zake zote katika masuala ya Kisheria ndani na nje ya nchi. Kutokana na mabadiliko hayo, mfumo wa Sekta ya Sheria nchini kupitia Ofisi mbalimbali za kiusimamizi na kiutekelezaji zilihitaji kufanyiwa marekebisho ili kuzingatia mabadiliko hayo ya kimfumo kwa lengo la kuondoa changamoto za kiutendaji miongoni mwa taasisi husika kupitia vifungu mbalimbali vya Sheria**.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kubainisha mapungufu mbalimbali katika mfumo wa kisheria nchini pamoja na kuandaa marekebisho na kuyawasilisha kwenye Bunge lako Tukufu kupitia Muswada huu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria na kuimarisha misingi ya nidhamu katika taaluma ya Sheria nchini katika Wizara na taasisi zote za Serikali.

## 2.2 UCHAMBUZI WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Namba 2 wa Mwaka 2018 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Act, 2018]* una jumla ya Ibara 108 ambazo zinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Kumi na Tatu (13) kama zilivyoorodheshwa awali. Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa maudhui ya kila ibara kama yanavyobainishwa katika sehemu hii ili kupata mantiki ya mapendekezo ya Serikali kwa kulingana na sababu za maudhui ya Muswada. Katika hatua hiyo, Kamati ilibaini maeneo mbalimbali yaliyohoitaji maboresho na hivyo kushauriana na Serikali kama yanavyoonekana katika sehemu inayofuata.

Aidha, wakati Kamati inaufanyia kazi Muswada huu ilibaini baadhi ya masuala mbalimbali ambayo hayapo kwenye

Muswada lakini yanahusiana kwa namna moja au nyingine na marekebisho yanayopendekezwa na hivyo kuyatolea maoni na mapendekezo ya jumla ili, kwa kadri itakavyoonekana inafaa, Serikali iyafanyie kazi kwa wakati mwafaka.

### 2.2.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inaainisha masharti ya awali ya Muswada kama ifuatavyo:

a) Ibara ya 1 inabainisha jina fupi la Sheria hii ambalo ni *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, 2018*. Muswada huu utakapotungwa kuwa sheria, ibara hii ndiyo itakayotoa jina sahihi ambalo litatumika katika rejea mbalimbali za kisheria nyinginezo.

b) Ibara ya 2 inaonyesha namna sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho zitakavyorekebishwa katika sehemu za muswada zinazofuata.

**Mheshimiwa Spika,** katika sehemu hii Kamati iliridhia marekebisho ya Serikali kama yalivyopendekezwa.

### 2.2.2 Sehemu ya Pili ya Muswada

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu**, Sura ya 27** (*The Administrator General (Powers and Functions) Act, Cap. 27*). Sheria hii inahusu mamlaka ya Kabidhi Wasii Mkuu, pale anapoombwa na wahusika au kuteuliwa na mahakama, kusimamia mirathi kwa kukusanya mali, kulipa madeni na mwisho kugawanya mali kwa warithi kulingana na sheria inayotumika au makubaliano ya wanaogawiwa au kwa kufuata wosia, kama upo. Sheria hii inasimamiwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini nchini (*The Registration, Insolvency and Trusteeship Agency* - RITA).

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii yanakusudia kuboresha utekelezaji wa mamlaka na majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu kama ifuatavyo:

(a) Ibara ya 4 ya muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 2 cha Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu kinachohusu tafsiri ya maneno na misamiati mbalimbali ili kuboresha tafsiri za maneno na misamiati iliyotumika katika sheria husika.

(b) Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 3A katika Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu ambacho kinaliongezea Baraza la kumshauri Waziri majukumu ya ushauri kuhusu mwenendo na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu. Kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya Wakala za Serikali, Sura ya 245 Baraza hili linaongozwa na Katibu Mkuu pamoja na Wajumbe wengine nane wanaoteuliwa na Waziri.

(c) Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 4 cha Sheria kinachohusu uteuzi wa Kabidhi Wasii Mkuu kama ifuatavyo-

(i) Kifungu hiki kinabadilisha uteuzi wa Kabidhi Wasii Mkuu ambapo atakuwa anateuliwa na Rais badala ya Waziri kama ilivyo sasa na kuanzisha nafasi ya Naibu Kabidhi Wasii Mkuu;

(ii) Kuweka utaratibu wa uteuzi wa Wasaidizi ambao watateuliwa na Waziri kutoka miongoni mwa Maafisa Sheria kutoka katika utumishi wa umma;

(iii) Kabidhi Wasii Mkuu atakuwa ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA mwenye majukumu ya kusimamia sheria zifuatazo:

- Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25 (*The Bankruptcy Act*);
- Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108 (*The Births and Deaths Registration Act*);
- Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 (*The Companies Act*);
- Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 (*The Law of the Child Act*);
- Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 (*The Law of Marriage Act*);

- Sheria ya Uthibitishaji Wasia na Uendeshaji Mirathi, Sura ya 445 (*The Probate and Administration of Estates Act*);
- Sheria ya Mdhamini wa Umma, Sura ya 31 (*The Public Trustee Act*);
- Sheria ya Muundo wa Wadhamini, Sura ya 318 (*The Trustees' Incorporation Act*); na
- Sheria nyingine yoyote inayoweza kumpa mamlaka na majukumu Kabidhi Wasii Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** inapendekezwa zaidi na Muswada huu kuwa, Kabidhi Wasii Mkuu apewe mamlaka ya kuandaa kanuni za kudumu na nyaraka nyingine za kisheria kwa ajili ya uendeshaji bora wa RITA. Katika mapendekezo hayo, iwapo mtumishi yeyote wa RITA atakiuka kanuni hizo atakuwa ametenda kosa la kinidhamu hivyo achukuliwe hatua na Naibu Kabidhi Wasii Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** maoni ya Kamati katika pendekezo hili ni kuwa, muswada uboreshwe zaidi ili hatua hizo za kinidhamu zichukuliwe kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma kwa sababu watumishi wa RITA ni sawa na watumishi wengine wa Umma ambao tayari wanawajibishwa na Kanuni za Utumishi wa Umma.

### 2.2.3 Sehemu ya Tatu ya Muswada:

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 (*The Criminal Procedure Act, Cap. 20*) ambayo ni Sheria inayoweka utaratibu unaopaswa kufuatwa katika uchunguzi na uendeshaji wa makosa ya jinai na masuala mengine yanayohusiana na haki jinai nchini. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kujumuisha maendeleo ya kiteknolojia pamoja na kuboresha vigezo vinavyotumika katika masuala ya kupokea na kuengua ushahidi mahakamani kama ifuatavyo:

(a) Ibara ya 8 ya Muswada ambayo inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 2 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinachohusu tafsiri ya maneno na

misamiati mbalimbali kwa kuboresha tafsri ya Mwendesha Mashtaka. Tafsiri hiyo inapendekezwa kuboreshwa ili kuzingatia marekebisho yanayofanyika katika muundo wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Hivyo, inapendekezwa Mwendesha Mashtaka kuwa ni Afisa Sheria au wakili wa Serikali anayeteuliwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Sura 430 na inajumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka na Naibu wake au mtu mwingine yeyote anayehusika na uendeshaji wa mashtaka kwa maelekezo ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

(b) Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 57 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinachohusu utaratibu wa kurekodi mahojiano kwa kuweka masharti mapya yanayopaswa kuzingatiwa na polisi yeyote anapokuwa anarekodi mahojiano kati yake na mtu yeyote kwa njia ya kinasa sauti au video. Masharti hayo ni:

(i) Kutumia kifaa chochote kinachoweza kunasa sauti au kurekodi video;
(ii) Mtu anayehojiwa anapaswa kufahamishwa kuhusu matumizi ya kifaa hicho;
(iii) Mtu aliyehojiwa au mwakilishi wake kupewa nakala ya mahojiano yaliyorekodiwa mara tu baada ya mahojiano kukamilika; na
(iv) Polisi husika kuaandaa hati inayoonyesha kukamilisha mahojiano ambayo itasainiwa na mtu aliyehojiwa na kumpatia nakala ya hati hiyo. Hata hivyo, hakutakuwa na sharti la mtu huyo kusomewa au kuweka saini/alama yake katika kila ukurasa wa hati hiyo.

Aidha, fasili ya (6) inapendekeza kuwa, mahojiano yaliyorekodiwa kwa utaratibu huu yatatumika kama ushahidi wa maudhui yaliyorekodiwa katika mahojiano bila ulazima wa kuwa na uthibitisho mwingine wa maandishi. Vilevile, fasili ya (7) inampa Jaji Mkuu mamlaka ya kuandaa kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya kurekodi mahojiano kwa njia ya vinasa sauti au video.

(a) Ibara za 10 inafanya Maboresho ya Kifungu cha 73 kinachohusu dhamana inayopaswa kuwekwa na wahalifu wazoefu kwa kujumuisha makosa ya madawa ya kulevya katika orodha ya makosa yaliyoainishwa. Marekebisho haya yataiwezesha Mahakama kumuamuru mhalifu mzoefu (*habitual offender*) katika madawa ya kulevya kuweka dhamana (*bond*) ikiambatana na wadhamini kwa kipindi kisichozidi miaka 3 ambapo atatakiwa awe amebadilika na kuwa na mwenendo mzuri.

(b) Ibara ya 11 inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 169 kinachohusu taratibu za Mahakama kutopokea ushahidi ambao umepatikana kinyume na sheria. Marekebisho yanayopendekezwa yanaongeza vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa na Mahakama kabla ya kuukataa ushahidi ambapo mahakama itapaswa kujiridhisha kuwa ukiukwaji wa sheria ulikuwa mkubwa na hivyo kuathiri utoaji wa haki jinai. Aidha, Mahakama itapaswa kubainisha sababu ilizozingatia katika kukataa ushahidi husika.

(c) Ibara ya 12 inapendekeza kufuta Kifungu cha 188 kinachohusu mamlaka ya mahakama kuzuia uchapishaji wa majina ya mashahidi kwenye vyombo vya habari na kukiandika upya. Kifungu kipya kinachopendekezwa kinampa Mkurugenzi wa Mashtaka mamlaka ya kupeleka maombi Mahakamani kwa ajili ya kupokea ushahidi kwa njia ya video pamoja na kuzuia mashahidi au nyaraka zinazoweza kusababisha mashahidi hao kufahamika kwa sababu za usalama wao.

(d) Ibara ya 13 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 205A kinachohusu upokeaji wa ushahidi wa wataalamu wa uchunguzi wa mitandao ya teknolojia, silaha/milipuko na utaalamu mwingine wowote. Kifungu hiki kinachopendekezwa kinaboresha masharti yaliyopo ambao yanatambua ushahidi wa wataalamu wa maandishi tu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa vitendo vya uhalifu vimezidi kuongezeka kwa kasi duniani, ni jambo zuri kwa Mamlaka za udhibiti wa makosa ya kijinai kuanzisha matumizi ya teknolojia

ya kisasa katika uchunguzi ili kupanua wigo wa udhibiti wa makosa ya kiuhalifu na kuongeza ufanisi kwa mamlaka husika.

### 2.2.4 Sehemu ya Nne ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu, Sura ya 368 (*The Extradition Act, Cap. 368*) ambayo inayohusu mahusiano ya kimataifa katika urejeshwaji wa wahalifu katika nchi walikotenda makosa. Muswada huu unapendekeza kuifanyia marekebisho sheria hii kupitia Ibara za 14 hadi 17 za Sheria ili kuboresha utaratibu wa urejeshwaji wa wahalifu hususani kwa kuondoa matakwa ya mfungwa anayetakiwa kurejeshwa katika nchi alikotenda kosa kukaa kizuizini kwa siku 15 kabla Waziri hajaidhinisha urejeshwaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** katika hili, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yana lengo la kurahisisha utoaji haki jinai kati ya Taifa letu na Mataifa mengine katika kudhibiti vitendo vya kiuhalifu kwa kuzingatia matakwa ya sheria hii ya mahusiano ya Kimataifa katika urejeshwaji wa wahalifu.

### 2.2.5 Sehemu ya Tano ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1(*The Interpretation of Laws Act, Cap. 1*). Sheria hii inahusu majumuisho ya kanuni za msingi zinazohusu maana, ufafanuzi na matumizi ya sheria zilizotungwa, na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Ibara za 18 na 19 za Muswada kwa kuboresha tafsiri ya maneno "Afisa Sheria". Tafsiri hiyo imejumuisha Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkurungenzi wa Mashtaka na Naibu wake, Wakili Mkuu wa Serikali na mawakili wa Serikali waliopo katika Utumishi wa Umma au Waandishi wa Sheria wenye cheo cha uandamizi na kuendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo kwa sababu yanafanyika ili kuendana na marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu nchini na Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu kama inavyoainishwa katika Hati Idhini husika.

### 2.2.6 Sehemu ya Sita ya Muswada;-

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Ukomo, Sura ya 89 (*The Law of Limitation Act, Cap. 89*) ambayo inaweka ukomo wa muda wa kufungua mashauri ya madai mahakamani. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa mujibu wa Ibara ya 21 ya Muswada ambapo Kifungu cha 44 kinaboreshwa ili kumpa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya sheria mamlaka ya kuongeza muda wa kufungua mashauri nje ya muda uliobainishwa na sheria.

**Mheshmiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuondoa sharti hilo la kiufundi*(legal technicality)* kwani limekuwa likisababisha Serikali kushindwa mashauri mbalimbali ambayo hata kama ina ushahidi na vigezo vya kutosha kushinda lakini inapoteza mashauri ya madai kwa sharti la kigezo la muda. Ni maoni ya Kamati kuwa, maboresho haya yataongeza uwigo wa Serikali kuwa na nafasi nzuri ya kushinda mashauri mengi ya madai hususani mashauri yanayotokana na Mikataba ya rasilimali za nchi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na hujuma mbalimbali zinazoweza kufanyika kwa kutumia kigezo cha muda.

### 2.2.7 Sehemu ya Saba ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171 (*The Law Reform Commission of Tanzania Act, Cap. 171*). Sheria hii inayoanzisha na kuainisha majukumu pamoja na mamlaka ya Tume ya Kurekebisha Sheria nchini inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

(a) Ibara za 23, 24, 27, 29, 30 na 31 zinapendekeza kufanya marekebisho ya vifungu vya 2, 4 na 8 ili-

(i) Kumpa Waziri mwenye dhamana ya mambo ya sheria mamlaka ya kutekeleza mambo mbalimbali kuhusu Tume ikiwemo kupeleka marejeo kwenye Tume, kupendekeza Wajumbe wa Kamati za Tume pamoja na kupokea taarifa ya muda kutoka Tume; na

(ii) Kuongeza wigo wa majukumu ya Tume ambapo itakuwa na uwezo wa moja kwa moja wa kutoa ushauri kuhusu mapendekezo ya kutunga sheria kwa Kamati ya Kitaalam ya Baraza la Mawaziri, pale inapoombwa kufanya hivyo pamoja na kupima utekelezaji wa sheria mbalimbali.

(b) Ibara ya 25 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 5 kinachohusu muundo wa Tume ili kurekebisha utendaji kazi wa Makamishna wa Tume ambapo idadi yao inapunguzwa kutoka makamishna kati ya wanne hadi tisa waliopo hivi sasa hadi kuwa na Makamishna wawili ambao watakuwa wanafanya kazi kwa muda (*part-time*).

(c) Ibara ya 26 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 6 kinachohusu masharti ya muda wa makamishna kuwa madarakani kwa kuboresha masharti ya kazi za Kamishna ambapo watateuliwa kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa awamu moja. Aidha, mapendekezo yanazuia mtu yeyote anayeshika nafasi ya juu katika mhimili wa Mahakama kuteuliwa kuwa Kamishna ijapokuwa mtu huyo anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume.

(d) Ibara ya 28 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 9 kinachoipa mamlaka Tume kutekeleza kazi zake yenyewe bila kusubiri kupelekewa marejeo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marekebisho yanapendekezwa kwa kuifuta fasili ya (1) na kuiandika upya ili kuipa Tume mamlaka ya kuanza kutekeleza kazi zake yenyewe lakini itoe taarifa kwa Waziri mwenye dhamana ya sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(e) Aidha, sharti la kutofanyia kazi masuala yaliyopo mahakamani yanayoihusu Jamhuri linapendekezwa kuondolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kutumia mapendekezo ya maboresho ya Sheria hii kwa kutekeleza maoni ya Kamati ya muda mrefu kuhusu kuboresha na kuimarisha mfumo wa Tume ya Kutunga Sheria katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ikiwa ni pamoja na kuainisha muda wa utumishi wa Makamishna wa Tume kwa lengo la kuimarisha nidhamu ya Utumishi katika Tume hii muhimu katika Sekta ya Sheria nchini.

Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa, maboresho haya, yataongeza uhuru wa Tume na kupunguza mlolongo wa taratibu za kiutendaji zisizo za lazima (*Beureaucracy)* katika kufanya maamuzi pamoja na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 2.2.8 Sehemu ya Nane ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai, Sura ya 256. Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai, Sura ya 256 (*The Mutual Assistance in Criminal Matters Act*) ni sheria mahsusi kwa ajili ya kuwezesha ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine katika masuala ya jinai.

Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho yafuatayo:

(a) Ibara ya 35 inapendekeza kurekebisha maneno au misamiati mbalimbali inayotumika katika sheria hii.

(b) Ibara ya 36 inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 2 kwa kuboresha tafsiri za misamiati mbalimbali inayotumika kwenye sheria.

(c) Ibara ya 37 inapendekeza kufanya maboresho katika Kifungu cha 4 kinachoainisha maeneo ambayo yatahusisha ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine kwa kuongeza

maeneo hayo. Maeneo yanayopendekezwa kuongezwa ni upatikanaji wa aina zote za data za kompyuta na simu, udukuaji wa vifaa vya posta na data za mawasiliano, ufuatiliaji wa kificho kwa njia za kielektroniki pamoja na kuwezesha kupokea ushahidi kwa njia ya video.

(d) Ibara ya 38 inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 5 ili kutoa fursa ya ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine kwa utaratibu ambao upo kwa mujibu wa mkataba au mazoea.

(e) Ibara ya 39 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 8 ambacho kinaainisha majukumu ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka kuhusiana na utekelezaji wa sheria hii ambapo kwa ujumla, pamoja na mambo mengine, Mkurugenzi huyo ndiye atakayekuwa na jukumu la kuratibu maombi ya ushirikiano yanayotumwa au kupokelewa kutoka nchi nyingine badala ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilivyo sasa.

(f) Ibara ya 40 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 9 cha sheria kinachohusu maombi ya nchi nyingine kusaidiwa na Tanzania. Mapendekezo hayo ni kuongeza nyaraka zinazopaswa kuwasilishwa ikiwa ni pamoja na maelezo ya aina ya uhalifu, taarifa fupi kuhusu kosa lilivyotendwa, mahakama yenye mamlaka na utambulisho wa mtuhumiwa.

(g) Ibara ya 41 inapendekeza kuongeza Vifungu vipya vya 9A, 9B na 9C vinavyoweka masharti ya usiri, lugha itakayotumika kuwa ni Kiingereza au kiswahili pamoja na namna gharama za kushughulikia maombi zitakavyobebwa.

(h) Ibara ya 42 inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 11 kinachohusu maombi yanayowasilishwa na nchi nyingine kwa ajili ya kukusanya ushahidi hapa Tanzania. Kimsingi, marekebisho ya kifungu hiki yanaboreshwa ili kumpa Mkurugenzi wa Mashtaka kushughulikia maombi hayo badala ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutokana na marekebisho ya muundo wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(i) Ibara ya 43 inapendekeza marekebisho ya kiuandishi katika Kifungu cha 25 kinachohusu maombi ya msaada katika uchunguzi unaoendelea nchi nyingine.

(j) Ibara ya 44 inapendekeza marekebisho ya kuongeza Kifungu kipya cha 25A kinachoruhusu uchukuaji wa ushahidi kwa njia ya mkutano wa video (*video conference*).

(k) Ibara za 45 na 46 zinapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 32 kinachohusu usajili wa amri mbalimbali na Kifungu cha 35 kinachohusu maombi ya kukusanya taarifa kwa kuzingatia maboresho ya muundo wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kumpa Mkurugenzi wa Mashtaka kusimamia utaratibu huo.

(l) Ibara ya 47 inapendekeza marekebisho ya kiuandishi katika Kifungu cha 38 kinachohusu uhakiki wa nyaraka.

(m) Ibara ya 48 inapendekeza marekebisho kwa kuongeza vifungu vipya ambavyo ni Kifungu cha 38A kinachohusu uhakiki wa ushahidi, Kifungu cha 38B kinachohusu upokeaji wa ushahidi wa kielektronic na Kifungu cha 38C kinachuhusu upokeaji wa aina nyingine yoyote ya ushahidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yana lengo la kuboresha na kuimarisha mfumo wa Kisheria katika ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine katika masuala ya jinai. Hii ni pamoja na kutambua matumizi ya teknolojia katika uhakiki nyaraka na ushahidi ili kuendana na nchini nyingine katika kushughulikia masuala ya Kijinai kati ya Tanzania na nchi husika.

### 2.2.9 Sehemu ya Tisa ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430. Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430 (*The National Prosecution Service Act)* ndiyo inayoanzisha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na kuainisha masharti ya uendeshaji wake kwa lengo la kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa haki

jinai nchini. Kimsingi, sheria hii inarekebishwa ili kuondoa vipengele vinavyowezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushughulika na masuala ya uendeshaji wa mashtaka na kuisimamia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kiutawala.

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo haya ni matokeo ya mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuanzisha Ofisi huru ya Taifa ya Mashtaka ya Jinai inayojitegemea. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho yafuatayo:

(a) Ibara ya 51 inapendekeza maboresho katika Kifungu cha 3 kwa kutoa tafsiri ya maneno Afisa Sheria ***(Law Officer***), wakili wa Serikali ***(State Attorney***), Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ***(Deputy Director of Public Prosecutions),*** Afisa Mwendesha Mashtaka wa Wilaya ***(District Prosecution Officer)*** na Afisa Mwendesha Mashtaka wa Mkoa (**Regional Prosecution Officer**). Aidha, ibara hii inafuta neno Mwanasheria Mkuu wa Serikali (***Attorney General***) katika tafsiri ya neno Mwendesha Mashtaka (***Public Prosecutor***).

(b) Ibara ya 52 ya Muswada inapendekeza kufuta Kifungu cha 4, 5, 6 na 7 vya sheria hiyo na kiviandika upya ambapo:

(i) Kifungu cha 4(1) na (2) kinahusu kutambua kuendelea kuwepo kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambayo itaongonzwa na Mkurugenzi wa Mashtaka;

(ii) Kifungu 4(3) kinaanzisha nafasi ya Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa za kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania;

(iii) Kifungu 4(4) kinaeleza kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa Msaidizi wa Mkurugenzi wa Mashtaka na atakuwa afisa masuuli wa Ofisi hii;

(iv) Vifungu vya 4 (5),(6),(7) na (8) vinatoa mamlaka kwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Afisa Sheria na Wakili wa Serikali kuwa wanaweza kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi wa Mashtaka baada ya kuteuliwa na Mkurugenzi huyo kwa ajili

hiyo. Aidha, Kifungu kinaeleza kuwa watakuwa na mamlaka kamili mbele ya mahakama kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

(v) Kifungu 5(1) kinampa mamlaka Mkurugenzi wa Mashtaka kuteua au kuajiri Maafisa Sheria, Mawakili wa Serikali na watumishi wengine wa umma katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwenye Mkoa na Wilaya nchini kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu na mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

(vi) Kifungu 5(2) kinaeleza kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa msimamizi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku na atakuwa ndiye mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wa Ofisi;

(vii) Kifungu 5(3) kinatoa mamlaka ya kuteua waendesha mashtaka wa kila Wilaya na Mkoa kuwa wafawidhi wa wilaya au mkoa alipoteuliwa;

(viii) Kifungu cha 6 kinatoa mamlaka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kutoa maelekezo na waraka mbalimbali kwa watumishi wa ofisi kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu ya ofisi na inaeleza zaidi kuwa mtumishi atakayekiuka maelekezo hayo atakuwa ametenda kosa la utovu wa nidhamu na atashughulikiwa na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka;

(ix) Kifungu cha 7 kinatoa mamlaka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kutunga Kanuni za Maadili ya Taaluma kwa Waendesha Mashtaka (*Code of Proffesional Conduct and Etiquettes for Public Prosecutors*) na atakayekiuka kanuni hizo anaweza kushughuliwa kwa mujibu wa Kanuni za utumishi wa Umma au kupitia Kamati ya Mawakili (*Advocates Committee*).

(c) Ibara ya 53 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 9 cha Sheria hiyo kinachohusu usimamizi wa uendeshaji wa mashtaka. Mapendekezo ya maboresho yanajumuisha kufuta maneno

ya pembeni (*Marginal note)* na kuyaandika upya pamoja na kuainisha upya majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

(d) Ibara ya 54 cha Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 19 cha sheria hiyo kwa kurekebisha sababu ambazo zinaweza kumuondoa Mkurugenzi wa Mashtaka na kuondoa sharti la Rais kushauriwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuchukua hatua dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

(e) Ibara ya 55 ya Muswada inapendekeza kufuta Kifungu cha 25 na kukiandika upya ili kuainisha chanzo cha mapato ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

(f) Ibara ya 56 ya Muswada inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 25A, 25B na 25C vinavyoeleza kuhusu masuala ya bajeti ya Ofisi, utekelezaji wa bajeti na utunzaji wa kumbukumbu za mahesabu ambazo zitakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*Controller and Auditor General*).

(g) Ibara ya 57 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 27 kwa kurekebisha Muundo wa Jukwaa la Taifa la Haki Jinai kwa kuongeza baadhi ya wajumbe.

(h) Ibara ya 58 inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 27A na 27B vinavyoanzisha Kamati ya Mawaziri ya Haki Jinai na Jukwaa la Haki Jinai la Mkoa. Kamati ya Mawaziri ya Haki Jinai itakuwa na jukumu la kutoa miongozo ya kisera na maelekezo ya mwenendo wa Haki Jinai. Jukwaa la Haki Jinai la Mkoa litakuwa na jukumu la kukutana na kujadili masuala ya kimkakati ya haki jinai katika mkoa husika.Lengo ni kuleta ufanisi katika mfumo wa haki jinai nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yana lengo la kuboresha na kuimarisha Ofisi ya Usimamizi na udhibiti wa makosa ya jinai nchini ili kuendana na Mabadiliko ya Mfumo wa Kisheria nchini kwa mujibu wa Hati Idhini iliyotolewa na Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni pamoja na kuboresha na kuimarisha Muundo wa Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa

Mashtaka nchini, kutenganisha masuala ya utawala na majukumu ya usimamizi wa mashtaka pamoja na kuainisha mfumo thabiti wa Kibajeti na Udhibiti wa Rasilimali fedha za Ofisi hii muhimu.

### 2.2.10 Sehemu ya Kumi ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu Yake) Sura ya 268. Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu Yake) Sura ya 268 *(The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, [Cap. 268]* ni sheria inayohusu utekelezaji wa mamlaka na majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na masharti ya uhusiano kati ya ofisi hiyo na ofisi nyingine za umma.

Kimsingi, sheria hii inarekebishwa ili kuendana na muundo mpya wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Hati Idhini iliyotolewa na Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho yafuatayo:

(a) Ibara ya 60 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 cha sheria hiyo kinachohusu tafsiri. Kifungu kinafuta tafsiri ya maneno ***Administrator – General, Investigative Organ na Legal Officer.*** Aidha kifungu kinafuta tafsiri ya maneno ***Code of Ethics na State Attorney*** na kuandika upya tafsiri za maneno hayo.

(b) Ibara ya 61 inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 3A kinachoainisha malengo ya Sheria hii kuwa ni kuimarisha na kujenga uwezo wa ofisi hiyo *(enhance and strengthen the capacity*):

(i) Kutoa ushauri wa masuala ya kisheria kwa Wizara, Taasisi za Serikali zinazojitegemea, Wakala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
(ii) Ufanisi katika uaandaji wa Miswada na Nyaraka kwa ajili ya kujadiliwa na Bunge;

(iii) Kutoa ushauri kwa Wizara,Taasisi za Serikali zinazojitegemea, Wakala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu mchakato wa utungaji wa Sheria;
(iv) Kushughulikia mashauri yaliyopo mahakamani au katika mabaraza ya utatuzi wa migogoro;
(v) Majadiliano ya makubaliano ya kiuchumi au kisiasa ndani na nje ya nchi ambazo Serikali ni sehemu au ina maslahi.

(c) Ibara ya 62 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4 kwa kuongeza maneno "***Constitution"*** na ***the Attorney General (Re-structure) Order, 2018 and"*** ili kuweka bayana kuwa usimamizi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, utekelezaji wa majukumu yake na uhusiano wa ofisi hii na ofisi nyingine za Umma utaongozwa na Katiba na Hati Idhini kuhusu mabadiliko ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(d) Ibara ya 63 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 5 kwa kueleza kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa ni Mkuu wa Baraza la Mawakili (bar) na atapata kipaumbele (*take precedence*) kila anapokuwa katika mashauri ya madai Mahakamani. Kifungu kinaeleza kuwa masharti hayo yatatumika kwa Wakili Mkuu wa Serikali, Afisa Sheria na Wakili wa Serikali wanapokuwa mahakamani kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(e) Ibara ya 64 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 6 cha sheria hiyo ili kumuondoa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutoa maelekezo kwa Maafisa Sheria waliopo ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

(f) Ibara ya 65 ya Muswada kinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 7 kwa kueleza kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa na jukumu la kuratibu wanasheria walio katika taasisi za Umma.

(g) Ibara ya 66 ya Muswada kinafuta Kifungu cha 8 cha sheria na kukiandika upya ili kuainisha majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(h) Ibara ya 67 ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 9 cha Sheria kwa kufuta maneno"***such officers***" na kuweka maneno" ***Law Officers and State Attorney"*** lengo ni kueleza bayana maafisa sheria watakaoajiriwa katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(i) Ibara ya 68 ya Muswada inarekebisha Sehemu ya Tatu ya Sheria kwa kufuta kichwa cha habari kidogo (a) na kukiandika upya ili kihusu vifungu maalum kuhusu mahusiano kati ya ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakili Mkuu wa Serikali na Kabidhi Wasii Mkuu.

(j) Ibara ya 69 ya Muswada inafuta kifungu cha 10 cha Sheria na kukiandika upya ili kuainisha namna ambavyo ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itahusiana na ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakili Mkuu wa Serikali na Kabidhi Wasii Mkuu.

(k) Ibara ya 70 inafuta Kifungu cha 11, 13 na 14 vilivyohusu uhusiano wa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kushughulikia mashauri ya madai na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimamia ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu.

(l) Ibara ya 71 ya Muswada inapendekeza kufuta kichwa cha habari cha Sehemu ya Nne na kuandika upya ili kihusu Mawakili wa Serikali na Afisa Sheria katika Taasisi za Umma.

(m) Ibara ya 71 ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 15 cha sheria kwa kuendelea kuwatambua maafisa sheria na mawakili wa Serikali katika Taasisi za Umma na kusimamiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Kifungu kinampa Mamlaka Wakili Mkuu wa Serikali kutoa Hati kwa maafisa sheria na mawakili wa Serikali katika Taasisi za Umma itakayowawezesha kuiwakilisha serikali mahakamani kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale ambapo mwanasheria Mkuu wa Serikali ni sehemu ya shauri.

(n) Ibara ya 73 ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 16 cha Sheria hiyo, kwa kueleza kuwa kazi ambazo kwa mujibu wa

Katiba au Sheria yeyote zinapaswa kutekelezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali zinaweza kutekelezwa na maafisa sheria au mawakili wa Serikali walioidhinishwa na mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria hii.

(o) Ibara ya 74 ya muswada inarekebisha Kifungu cha 16 kwa kuongeza kifungu cha 16A kinachoanzisha Chama cha wanasheria walio katika Utumishi wa Umma. Aidha kinaongeza kifungu cha 16B kinachohusu Orodha ya Mawakili wa Serikali.

(p) Ibara ya 75 ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 17 cha sheria ili kumruhusu Wakili Mkuu wa Serikali kuweza kupeleka hati ya kuunganishwa katika shauri lolote ambalo hakuwa na haki ya kuwakilisha ili aweze kuwa sehemu ya shauri hilo.

(q) Ibara ya 76 ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 18 ili kuweka utaratibu wa Katibu Mkuu wa Wizara yeyote akiona kuna haja baada ya kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali atateua Afisa Sheria au Wakili wa Serikali wa kusimamia mashauri mahakamani kwa niaba ya wakili Mkuu wa Serikali.

(r) Ibara ya 77 na 78 za muswada zinarekebisha kifungu cha 19 na 20 kwa kuondoa neno "*Legal Officer*"

(s) Ibara ya 79 inarekebisha Kifungu cha 21(3) ili kuweka bayana kuwa masuala ya usimamizi na nidhamu kwa wanasheria waliopo katika Taasisi za Umma yatasimamiwa na waajiri wao.

(t) Ibara ya 80 inarekebisha Kifungu cha 22 kwa kuainisha masharti ambayo yatatumika kwa Wizara na Taasisi za Umma katika kuomba ushauri wa kisheria kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(u) Ibara za 81, 82 na 83 za Muswada zinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 23, kwa kufuta kichwa cha habari cha sehemu ya Sita na kuiandika upya ili kihusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali

wengine katika Taasisi za Umma pamoja na kufanya marekebisho madogo katika Kifungu cha 24.

(v) Ibara ya 84 inarekebisha Kifungu cha 25 kwa kukifuta na kukiandika upya ili kuanzisha Timu ya Sheria ya Serikali (***Government Legal Team)*** ambayo itahusika na uchambuzi wa mikakati ya kisheria katika ushauri unaotolewa, masuala ya uendeshaji wa mashtaka na usikilizaji wa mashauri mahakamani (*undertake strategic legal analysis and forecast with regard to legal service rendered as well as prosecutorial and adjudicatory service provided).*

(w) Ibara ya 85 inafanya marekebisha madogo katika Kifungu cha 26 kwa kufuta maneno"***and other legal officers***"

(x) Ibara ya 86 inapendekeza kufuta Kifungu cha 27 na 28 cha sheria na kuviandika upya ambapo:

(i) Kifungu cha 27 kinaweka utaratibu wa kushughulikia masuala ya nidhamu ya maafisa sheria na mawakili wa Serikali waliopo katika utumishi wa umma; na

(ii) Kifungu cha 28 kinampa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutunga Kanuni, kutoa maelekezo na nyaraka nyingine kwa ajili ya usimamizi bora wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(y) Ibara ya 87 inapendekeza kufuta Jedwali la Sheria hii ambalo lilihusu Kanuni za Maadili kwa maafisa Sheria, mawakili wa Serikali na "***Legal Officers***".

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa nia nzuri ya kuimarisha Misingi ya Nidhamu ya Taaluma ya Sheria nchini kupitia mapendekezo haya. Hivyo, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwakuwa yana lengo la kuboresha na kuimarisha maeneo muhimu yafuatayo:-

(a) Kuanzisha mfumo rasmi wa usimamizi na uratibu wa masuala yote ya Wanasheria waajiliwa katika Utumishi wa Umma katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali,

(b) Kuanzisha Chombo cha kiusimamizi cha kuwatambua na kuwaunganisha Mawakili wa Serikali chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

(c) Kutenganisha majukumu ya Mawakili wa Serikali katika utumishi wa Umma na Majukumu ya Mawakili wa kujitegemea kwa lengo la kudhibiti uwepo wa maslahi binafsi ambayo yanaweza kuiathiri Serikali na hivyo kuathiri maslahi ya nchi kwa namna moja au nyingine,

(d) Kuainisha na kubainisha wazi mamlaka za Usimamizi na uwakilishi wa Serikali katika Mashauri ya Madai na Makosa ya kijinai miongoni mwa Ofisi husika zenye Mamlaka yanayoshabihiana, na

(e) Kuondoa mazingira ya kuingiliana kiutendaji kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sababu hizo kama zilivyoainishwa hapo juu, Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yana lengo zuri la kuboresha Mfumo wa kisheria nchini kwa manufaa ya Wanataaluma wenyewe, Serikali, Jamii ya Watanzania kwa ujumla na kwa ustawi wa taaluma ya sheria hapa nchini.**

### 2.2.11 Sehemu ya Kumi na Moja ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329. **Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 (The** *Prevention and Combating of Corruption Act*) inahusu masharti ya kuzuia, kuchunguza na kupambana na rushwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU).

Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Ibara ya 89 ya muswada ambayo inarekebisha Kifungu cha 34 cha sheria hiyo kinachohusu uhamishaji wa mali zitokanazo na uhalifu ili kuondoa maneno “Mwanasheria Mkuu wa

Serikali" na badala yake kumuweka "Mkurugenzi wa Mashtaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaridhia Marekebisho haya kwa kuwa yanaendana na maboresho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Hati idhini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.2.12 Sehemu ya Kumi na Mbili ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19**.** Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19 *(The Prevention of Terrorism Act)* inahusu masharti ya kukabiliana na ugaidi nchini pamoja na ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine duniani katika kupambana na ugaidi.

Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia Ibara ya 91 ya muswada ambayo inapendekeza kufuta Kifungu cha 34(3) cha sheria kinachohusu uwezo wa Mahakama ya juu ya makosa yaliyobainishwa na kukiandika upya.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaridhia marekebisho hayo kwa kuwa yana Lengo la kuweka masharti ya matumizi ya teknolojia katika uendeshaji wa kesi za ugaidi na pia kumlinda shahidi kwenye kesi hizo ili kuendana na hali halisi ya matumizi ya teknolojia duniani katika masuala ya udhibiti wa vitendo vya uhalifu.

### 2.2.13 Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Urejeshwaji wa Mali zitokanazo na Uhalifu, Sura ya 256. Sheria ya Urejeshwaji wa Mali zitokanazo na Uhalifu, Sura ya 256 *(The Proceeds of Crimes Act*) inahusu masharti mahsusi ya namna ya kushughulikia urejeshwaji wa mali zilizopatikana kutokana na uhalifu. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

(a) Ibara ya 93 inapendekeza kufanya Marekebisho ya jumla katika sheria yote kwa kufuta na kuandika upya baadhi ya maneno na misamiati mbalimbali iliyotumika kwenye sheria hiyo.

(b) Ibara ya 94 inapendekeza kufanya Marekebisho katika Kifungu cha 3 kinachohusu tafsiri ya maneno na misamiati iliyotumika kwenye sheria kwa kuboresha wigo wa makosa makubwa na makosa mahsusi.

(c) Ibara ya 95 inapendekeza kufuta Kifungu cha 31A kinachohusu kuzuia akaunti ya mtuhumiwa wa uhalifu wakati wa uchunguzi na kukiandika upya. Maboresho haya yanapendekeza kuongeza siku ambazo polisi wamepewa mamlaka ya kuzuia akaunti husika kutoka siku 7 hadi 14 wakati akitafuta amri ya mahakama kuidhinisha zuio hilo. Aidha, mahakama inaongezewa mamlaka kubadilisha zuio hilo aidha kwa kuongeza siku za zuio au kulifuta kabisa.

(d) Ibara ya 96 inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 31B na 31C vinavyohusu makosa na adhabu wakati wa ukusanyaji wa taarifa au nyaraka zinazohusu mali pamoja na utoaji wa taarifa za kiuchunguzi kwa watu wasiohusika na taarifa hizo.

(e) Ibara ya 99 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 42 kinachohusu notisi ya mali iliyozuiliwa kwa tuhuma za uhalifu kwa kuongeza Kifungu cha 42(3). Kifungu hiki kinatoa fursa kwa mtu aliyeathiriwa na amri ya kuzuia mali kuiomba mahakama ndani ya siku 14 baada ya amri kutolewa ili amri husika ibadilishwe au ifutwe au amri nyingine yoyote kwa kadri mahakama.

Aidha, Ibara ya 100 inapendekeza kufanya Marekebisho ya Kifungu cha 43 (3) kwa kukifuta na kukiandika upya ili kuweka vigezo ambavyo Mahakama itapaswa kuzingatia kabla ya kubadilisha amri inayotolewa chini ya kifungu cha 42. Vigezo hivyo ni kuzingatia kuwa mali husika haihusiki na uhalifu na kama upatikanaji ulipatikana kwa thamani halisi ambayo isingeweza kuibua mashaka kwamba mali hiyo ni ya kihalifu.

(f) Ibara ya 101 inapendekeza kufanya Marekebisho madogo katika kifungu cha 50 cha sheria.

(g) Ibara ya 102 inapendekeza kufanya Marekebisho ya kiuandishi katika kifungu cha 51.

(h) Ibara ya 103 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 62A ambacho kinaweka masharti ya namna afisa anayefanya uchunguzi anavyoweza kumtaka mtuhumiwa wa makosa makubwa kutoa taarifa za akaunti au mali inayoshutumiwa kwa makosa hayo.

(i) Ibara ya 104 inapendekeza kufuta Kifungu cha 76 kinachohusu rufaa kutokana na mali iliyofilisiwa kwa kuboresha masharti hayo ili utaratibu wa rufaa uzingatie sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Aidha, mtu yeyote anapokata rufaa chini ya kifungu hiki, utekelezaji wa amri ya kufilisi mali iliyokuwa imetolewa utasitishwa hadi rufaa hiyo itakapoamuliwa.

**Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Marekebisho haya ni muhimu kwasababu yana lengo la kuimarisha udhibiti wa mali zinazotokana na uhalifu kwa mujibu wa Sheria ya Urejeshwaji wa Mali zitokanazo na Uhalifu pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai chini.**

### 2.2.14 Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada:-

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii ya Muswada inahusu Marekebisho ya Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307. Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika, Sura ya 307 (*The Tanganyika Law Society Act*) ni mahsusi kwa ajili ya uanzishwaji wa Chama cha Mawakili Tanganyika (*The Tanganyika Law Society - TLS*) na masuala yanayohusiana na chama hicho. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

(a) Ibara ya 106 inapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 15 kinachohusu muundo wa Baraza ambalo linaundwa na rais, makamu wa rais na mweka hazina wa TLS pamoja na

wajumbe wengine 7. Marekebisho yanapendekeza kuongeza vifungu vidogo vipya na kuboresha mtiririko wake.

Vifungu vinavyoongezwa vinaweka sifa za mtu kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza hilo ambapo mjumbe husika anatakiwa kuwa:

(i) Raia wa Tanzania;
(ii) Amethibitishwa kuwa na akili timamu;
(iii) Hajatangazwa kuwa mufilisi; na
(iv) Amethibitishwa na Kamati ya Uteuzi kuwa na weledi.

Aidha, Marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kutoruhusu wafuatao kugombea ujumbe wa Baraza-
(i) Mtumishi wa umma;
(ii) Diwani;
(iii) Mbunge; au
(iv) Kiongozi wa chama cha siasa.

(b) Ibara ya 107 inapendekeza kuongeza Kifungu cha 15A kinachohusu kuzuia mjumbe wa Baraza kujihusisha na shughuli za kisiasa zilizoainishwa na sheria. Shughuli hizo zinajumuisha-
(i) Kugombea nafasi za kisiasa katika chama cha siasa;
(ii) Kupiga kampeni za kumuunga mkono au kumpinga mgombea yeyote katika chaguzi za kisiasa;
(iii) Kutoa hotuba za kampeni;
(iv) Kukusanya michango au kufanya harambee kwa ajili ya chama chochote cha siasa;
(v) Kupanga au kusimamia maandamano ya kisiasa au mikutano; au
(vi) Kuwa na nafasi ya madaraka katika vyama vya siasa.
(vii) Aidha, inapendekezwa na Ibara hii kuwa iwapo mjumbe atakiuka masharti hayo atakuwa amefanya makosa makubwa ya kimaadili na ikitokea, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kupeleka maombi katika Kamati ya Mawakili ili mhusika aondolewe kwenye orodha ya mawakili.

(c) Ibara ya 108 inapendekeza marekebisho kwa kufuta Kifungu cha 31 kinachohusu utungaji wa kanuni na kukiandika upya. Marekebisho yanayopendekezwa ni utungaji wa

kanuni ufanywe na Baraza kwa kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kisha kanuni hizo zitatakiwa kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, ***Kamati inaridhia mapendekezo ya Serikali kwa kwa kuwa yana lengo la kuimarisha misingi ya nidhamu, vigezo na mipaka ya kitaaluma kwa Mawakili wa Kujitegemea pamoja na sifa stahiki kwa Viongozi wa vyama vya Mawakili nchini ili kuimarisha taswira ya taaluma ya Sheria ndani na nje ya nchi yetu. Hii ni pamoja na kutofautisha Majukumu ya Chama cha Taaluma ya Sheria na Vyama vya Siasa kwa lengo la kutenganisha taaluma na shughuli za siasa pamoja na masharti mengine kama yalivyoainishwa na marekebisho haya.***

## 3.0 USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huu, Kamati ilibaini masuala mbalimbali yaliyohitaji maboresho katika Muswada au kuchukuliwa hatua nyingine za kiutendaji. Katika masuala hayo, Kamati ina maoni pamoja na mapendekezo mahsusi na ya jumla kwa kuzingatia mashauriano na Serikali kama ifuatavyo:

### 3.1 USHAURI MAHSUSI

**a) Maboresho ya Ibara ya 6(7) kwa kuweka Misingi ya Kisheria ya kushughulikia Masuala ya Maadili kwa Watumishi wa Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Ibara ya 6(7) Naibu Kabidhi Wasii Mkuu amepewa mamlaka ya kuwashughulikia watumishi wa RITA pale wanapokuwa wametenda makosa ya kimaadili. Hata hivyo, Ibara hii haijapendekeza misingi ya kisheria ambayo inapaswa kuzingatiwa katika kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi hao kama ilivyobainishwa kwenye maboresho ya muundo wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati imeshauriana na kukubaliana na Serikali kuwa, hatua hizo zichukuliwe kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi wa umma kama ilivyo kwa watumishi wote wa umma.

Kwa msingi huo, Ibara ya 6(7) imefanyiwa maboresho ya kimaandishi na kimaudhui ambapo maboresho ya kimaandishi amefanyika kwa kutenganisha majukumu ya Naibu Kabidhi Wasii Mkuu na kuyaweka katika fasili mpya ya (2) itakayosomeka kama ifuatavyo:

***(2) The Deputy Administrator General shall be the principal assistant to the Administrator General, accounting officer and the disciplinay authority of the agency.***

**Mheshimiwa Spika,** katika upande wa maudhui, Kamati imekubaliana na Serikali kuwa misingi ya sheria za utumishi wa umma izingatiwe katika kushughulikia masuala yote ya nidhamu yanayowahusu watumisi wa RITA. Hivyo, Ibara ya 6(7) itasomeka kama ifuatavyo:

***(7) A staff in the Registration, Insolvency and Trusteeship Agency who fails to comply with the orders, practice notes and other instruments issued unders subsection (6) commits a misconduct and shall be dealt with in accordance wih the laws governing the public sevice.***

**b) Maboresho ya Ibara ya 9 ili kuimarisha Uzingatiaji wa Haki za Mtuhumiwa wakati anafanyiwa Mahojiano**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza kuongeza masharti katika kifungu cha 57 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 kwa ajili ya kuwezesha kurekodi mahojiano yanayohusiana na masuala ya jinai kwa njia ya vinasa sauti au video. Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mapungufu katika Ibara hii kwa kuwa haijaweka misingi ya uzingatiaji haki mbalimbali za mtuhumiwa au shahidi kama vile haki ya kuwa na mwanasheria au uwakilishi mwingine wa ndugu au rafiki.

Kamati imeshauriana na kukubaliana na Serikali kuboresha masharti ya Ibara hii ili kuzingatia haki hizo ambapo Ibara ya 9 kifungu cha (5) inaboreshwa ili isomeke kama ifuatavyo:
***(5) An interview of a person by a police officer under this section may, if available, and subject to sections 53, 54, and***

***55 be undertaken by using an audio or video recording device and in such circumstances:***

**c) Maboresho ya Ibara ya 12 kwa kuondoa sharti la Mwendesha Mashtaka ya Serikali kusikilizwa peke yake (*ex-parte hearing*) katika Maombi yanayowasilishwa Mahakamani kuhusu kuchukua Ushahidi kwa Mikutano ya Video**

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara ya 12 ya Muswada yanakusudia kutoa ulinzi kwa mashahidi wanapotoa ushahidi mahakamani pale Mwendesha Mashtaka Mkuu anapoona kuwa kuwa hatari za kiusalama dhidi ya mashahidi hao. Katika maombi yaliyoainishwa, Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali anasikilizwa peke yake bila kutoa fursa kwa upande wa pili kusikilizwa (*ex-parte hearing*) ikiwemo maombi ya kupokea ushahidi kwa njia ya mikutano ya video (*video conferencing*).

Kamati ina maoni kuwa, Ibara hii iboreshwe zaidi ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza kuhusu fursa ya Mwendesha Mashtaka ya Serikali kusikilizwa peke yake (*ex-parte hearing*) wakati wa maombi ya ridhaa ya mahakama kupokea ushahidi kwa njia ya mikutano ya video. Hata hivyo, Serikali ilipendekeza kuwa Ibara hii iboreshwe ili iainishe kwamba maombi yaliyobainishwa yatapelekwa na DPP na kusikilizwa na mahakama kabla hati ya mashtaka haijawasilishwa mahakamani. Hivyo, Ibara ya 12 Kifugu cha 188(1) kitasomeka kama ifuatavyo:

***188(1) Notwithstanding any other written law, before filing a charge or information or at any stage of the proceedings under this Act, the court may, upon an ex-parte application by the Director of Public Prosecutions, order-***

**d) Maboresho ya Ibara ya 58 kwa kuanzisha Jukwaa la Haki Jinai la Wilaya**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 57 na 58 zinaanzisha Jukwaa la Haki Jinai Kitaifa na katika ngazi ya mkoa ambapo Jukwaa la Haki jinai la Taifa litahusika na masuala ya kisera ya haki

jinai wakati lile la mkoa litashughulikia masuala hayo kiutendaji katika ngazi ya mkoa. Kwa kuzingatia kuwa ukubwa wa nchi yetu pamoja na muundo wa utawala, Kamati imeshauriana na kukubaliana na Serikali kuanzisha Jukwaa kama hilo katika ngazi ya Wilaya ili kusogeza huduma ya utatuzi wa masuala ya haki jinai karibu zaidi na wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Jukwaa la Haki Jinai la Wilaya linapendekezwa kuundwa na Wajumbe wafuatao:

(i) Mwendesha Mashtaka wa Wilaya ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(ii) Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya;
(iii) Afisa Usalama wa Wilaya;
(iv) Mkuu wa PCCB wa Wilaya;
(v) Afisa Magereza wa Wilaya;
(vi) Mratibu wa Huduma za Jamii wa Wilaya;
(vii) Afisa Ustawi wa Jamii; na
(viii) Kamanda Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya ambaye atakuwa Katibu.

**e) Maboresho ya Ibara ya 72 kwa kuweka Mfumo wa Mawasiliano kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Taasisi za Umma kuhusiana na Hatua za Kinidhamu zinazo chukuliwa dhidi ya Wanasheria walioajiriwa katika Taasisi hizo.**

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoainishwa awali, mojawapo ya madhumuni ya msingi ya mapendekezo ya Muswada huu ni kuwezesha mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na mfumo wa sheria ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amepewa mamlaka ya kuwaratibu wanasheria wote waliopo katika uumishi wa umma. Kwa msingi huo, Kamati imeshauriana na kukubaliana na Serikali kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli hizo za uratibu kwa kuweka mfumo wa ubadilishanaji wa taarifa kati ya waajiri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hivyo, Ibara ya 79 itaboreshwa kwa kuongeza fasili mpya ya (4) kama ifuatavyo:
***(4) Employers of law officers and state attorneys shall have the duty to notify the Attorney General on all disciplinary cases***

***against law officers and state attorneys under their supervision and control.***

**f) Maboresho mbalimbali ya Kiuandishi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeshauriana na kukubaliana na Serikali kufanya maboresho mbalimbali ya kiuandishi katika Ibara za 16, 19, 39, 41, 44, 52, 66 na 72 kwa lengo la kuondoa utata wa kisheria uliobainika na kuweka msingi mzuri wa tafsiri na matumizi ya sheria.

## 3.2 USHAURI WA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza awali, uchambuzi na tathmini ya Kamati umebaini uwepo wa changamoto mbalimbali katika sheria ambazo zinapendekezwa kufanyiwa maboresho lakini changamoto hizo hazijatolewa mapendekezo katika Muswada huu. Kamati imeshauriana na kukubaliana na Serikali kuyafanyia kazi kwa wakati mwafaka. Maoni na mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:

**(a) Kuhuisha Sheria ya Chama cha Mawakili nchini (*Tanganyika Law Society Act, Cap. 307*)**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Chama cha Mawakili nchini (*Tanganyika Law Society Act, Cap. 307*) imeanza kutumika nchini tangu tarehe 1 Januari, 1955. Tangu wakati huo, sheria hiyo haijafanyiwa maboresho ya msingi kuhusu malengo, muundo na mfumo wa uendeshaji wa TLS hali inayosababisha changamoto zinazoonekana sasa kwa chama hicho kushindwa kuendana na zama zilizopo. Kamati inaishauri Serikali iifanyie tathmini sheria hiyo kwa lengo la kuihuisha hususan katika masuala yafuatayo:

(i) Kubainisha na kutenganisha mamlaka na majukumu ya Baraza la TLS na Sekretarieti yake;

(ii) Kuboresha masharti ya Mkutano Mkuu wa TLS;

(iii) Kuboresha masharti yanayohusu fedha za TLS; na

(iv) Kuweka masharti kuhusu *Chapter* za chama hicho;

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali kwa mara nyingine ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba ni watambue na kuwashukuru wadau Mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa weledi na umahiri wao walioonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. **Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu rasmi za Bunge (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb **– Makamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. George Simbachawene, Mb - Mjumbe;
4. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
5. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb-Mjumbe;
18. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;

22. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
23. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe;
24. Mhe. Emanuel A. Mwakasaka, Mb - Mjumbe;
25. Mhe. Dkt.Damas Daniel Ndumbaro, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuu Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge **Ndg.Stephen Kagaigai** kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Washauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndg.Stephano Seba Mbutu, Ndg. Maria Ndulugu, Ndg.Nesta Kawamala, Ndg.Evelyne R.Shibandiko, Ndg.Thomas A.Shawa na Makatibu wa Kamati Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg.Dunford P.Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg.Rahel Masima waliofanikisha kazi ya Uchambuzi na uratibu wa shughuli za Kamati kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamlika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**
7 SEPTEMBA, 2018

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro kwa kumwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba ya Sheria. Sasa ni zamu ya maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Ally Saleh (Makofi).

Mheshimiwa Ally Saleh kabla ya kuanza kusoma kwa kutumia Kanuni ya 64(1)(e) na Ibara ya 34 na 36 ya Katiba maelezo yaliyoko kwenye ukurasa wa pili *paragraph* ya tatu ya mwisho yanaondolewa na ukurasa wa tatu *paragraph* ya tatu kuhusu Mawakili yanaondolewa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo kidogo.

**MWENYEKITI:** Haya taratibu.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti kidogo kidogo, ipi na ipi?

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa pili *paragraph* ya mwisho.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti imeanzia nini *paragraph?*

**MWENYEKITI:** Imeanzia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutokufanya maamuzi...

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hewala.

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa tatu *paragraph* ya tatu kuhusu Mawakili wanajua kuwa lengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuleta mapendekezo...

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona sioni?

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa tatu.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ungeniambia kwa sababu hatufuatani mimi na wewe. Kwa sababu mimi nasoma humu wewe unasoma kwenye kitabu, kwa hivyo hatufuatani, ikifika wakati utaniambia mimi nitakwambia hewala, nitaiondoa.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nitoe maoni juu ya Muswada wa Sheria Namba 2 uliochapishwa tarehe 8 Juni, 2018 katika juzuu namba 99 ya gazeti la Serikali, muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria Mbalimbali 13 ambapo marekebisho haya yanalenga kuwezesha utekelezaji wa mabadiliko ya mfumo wa kisheria baada ya kufanywa kwa marekebisho ya mfumo huo kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali na matangazo ya Serikali na matangazo ya Serikali namba 48 na 49 na 50 ambapo Ofisi ya Kabidhi Wasii Mwanasheria Mkuu, Mwanasheria wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashitaka na Afisi ya Wakili Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni utamaduni wa msingi wa kisheria kuwa sheria zinaanza kutungwa na kufuatiwa na kanuni pamoja na kanuni mbalimbali za kiutekelezaji kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Serikali na maisha ya wananchi. Utaratibu huu unakiukwa na Serikali ya Awamu ya Tano hii ni kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano inaanza kutoa matamko kwanza na maelekezo ndipo unafuatwa utaratibu wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hutakiwa kufanya kazi zake zote kwa mujibu wa sheria kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(d) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalipa Bunge Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kutunga sheria. Kama Serikali inatoa maelekezo kupitia kwa Rais au Mawaziri na baada ya hapo kuleta muswada wa kisheria kuhalalisha maamuzi na maelekezo ya Serikali ni ishara kuwa, Serikali inapuuza mamlaka na hadhi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 ikiwa katika Mkutano Mkuu wa CCM, Rais John Pombe Magufuli alitangaza na kueleza Serikali kuhamia Makao Makuu Dodoma bila ya uwepo wa sheria. Pamoja na Kamati ya Bunge ya Sheria na Katiba kuhoji jambo hilo Mwanasheria

Mkuu wa Serikali alitoa kauli kuwa jambo hilo linatakiwa kufanyiwa kazi na Ofisi ya Waziri Mkuu akijua yeye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali bila kujali Wizara na Idara. Hatimaye katika mkutano huu wa Bunge sheria ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali kupitia Muswada wa Sheria Namba 3 uliowasilishwa na kupitishwa na Bunge pamoja na kuwa tamko lilitoka muda mrefu na idadi kubwa ya watumishi tayari kuhamishiwa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muswada huu wa leo yapo maeneo kadhaa ambayo Serikali inahalalisha uamuzi ambao umeshafanyika kwa siku kadhaa zilizopita. Mathalani kuanzisha kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kulifanyika wakati ambapo sheria zinabadilishwa katika muswada huu zinatoa utaratibu tofauti na maamuzi ambayo yalifanyika bila kuangalia masharti ya sheria, pamoja na kuwa utaratibu wa utungwaji wa sheria na maamuzi ulitakiwa kuangalia masharti ya sheria zilizopo kabla ya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni...

**MWENYEKITI:** Kifungu hicho kimeondolewa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wapi?

**MWENYEKITI:** Mpaka mwisho *paragraph* yote hiyo.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *paragraph* nzima?

**MWENYEKITI:** Ndio.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Kimeshaondolewa, Mheshimiwa Ally Saleh naomba uendelee *paragraph* inayofuata.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, hewala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni hayo hayo hata katika marekebisho ya Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika yanayopendekezwa na kifungu cha 105 cha muswada ambapo marekebisho yanayopendekezwa yanawanyima haki watu ambao ni watumishi wa umma, kama vile Madiwani, Wabunge na viongozi wa vyama vya siasa kuwa wajumbe wa baraza la uongozi wa Chama cha Mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni mwa mwaka huu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliingia kwenye mgogoro na Chama cha Mawakili wa Tanganyika na baada ya kukaa vifungu hivyo vinavyopendekezwa kwenye Kanuni za Uchaguzi bila kuzingatia kuwa hayakuwa mapendekezo ya Baraza la Uongozi na wala Mwanasheria wa Serikali hana mamlaka ya kufanya hivyo. Mawakili

**MWENYEKITI**: *Paragraph* inayofuatwa imefutwa yote.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hewala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kuwa Serikali sasa inatunga sheria kwa kumlenga mtu au taasisi au kumtafutia mtu wadhifa na haitungi kwa malengo mahususi ya kuwasaidia wananchi. Haitashangaza huko baadae sheria nyingi kufutwa baada ya CCM kukataliwa na wananchi kwa sababu ya kushindwa kusimamia taratibu ambazo tumejiwekea kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya sheria hii ambayo inalenga kifungu cha 2 na cha 3(a) na kifungu 4 ambacho lengo kubwa ni kuanzisha nafasi mpya ya Naibu Kabidhi Wasii Mkuu *(Deputy Administrator General)* pamoja na kumnyang'anya Waziri mamlaka ya kumteua Kabidhi Wasii Mkuu na badala yake Rais ndiye atafanya uteuzi huo. Ni wazi kuwa kifungu cha 36(2) cha Katiba ya nchi kinampa Rais mamlaka ya kuteua watu katika kushika nafasi ya madaraka ya kiuongozi pamoja na mamlaka hayo ya Kikatiba, kimsingi kifungu hiki kinaukakasi mkubwa hasa pale ambapo nchi inaweza ikawa na kiongozi mwenye mamlaka makubwa kama hayo ya kiuteuzi na akayatumia vibaya madaraka hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa kuwa wateule wengi wamekuwa wakifanya kazi kwa maelekezo badala ya sheria na kanuni zilizowekwa na hususani katika utekelezaji wa majukumu ambayo yanaweza kugusa maslahi ya mteua yaani yaani mtu anayeteua. Haishangazi siku hizi kusikia mtumishi wa umma mwenye mamlaka akisema anashindwa kufanya maamuzi fulani kwa sababu amepokea maelekezo kutoka juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani katika majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu na Naibu Kabidhi Wasii katika yale anayosimamia ikiwa ni pamoja na kutoa huduma ya ufilisi kwa watu binafsi *(bankruptcy),* ufilisi kwenye mahakama *(company liqudation)*, kusajili na kutoa hati ya kusajili kwa wadhamini wa vyama vya siasa, vikundi, makanisa,misikiti na mali ikiwa ni pamoja na kufuta usajili. Kwa uzito na unyeti wa majukumu haya isipoangaliwa vizuri mamlaka ya Rais katika uteuzi yanaweza kutumika vibaya katika kushawishi uonevu, hujuma na udhalilishaji kwa wale wenye milengo tofauti na matakwa ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuletwa kwa marekebisho ya sheria hii Waziri aliyekuwa na mamlaka ya kufanya uteuzi huu ni Waziri ndiye aliyekuwa na mamlaka ya kufanya uteuzi huu. Hii ikiwa ni kwamba, endapo uteuzi uliokuwa umefanywa na waziri haukufuata taratibu au una

upungufu Rais ana uwezo wa kutengua uteuzi kama huo. Endapo Rais kama binadamu anapoteua mtu bila kufuata taratibu bila vigezo tujiulize ni mamlaka gani itaweza kumwajibisha? Mfano...

**MWENYEKITI:** Kuanzia mfano hapo inaondolewa mpaka mwisho.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Naam.

**MWENYEKITI:** Kuanzia mfano Waziri wa Sera mpaka mwisho wa *paragraph* imeondolewa.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba haturuhusiwi kuonesha mfano wa namna ambavyo uteuzi unaweza kwenda visivyo, na imetokea ndani ya nchi hii, hewala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inazidi kuutaka Umma wa watanzania kuendelea kupigania mahitaji ya upatikanaji wa Katiba Mpya ili kupunguza mamlaka ya Rais hususani ya kufanya teuzi katika idara na vitengo nyeti ili kuepuka kufuata mamlaka na matakwa ya mtu binafsi badala ya matakwa ya taasisi ili kuepusha nchi yetu na udikteta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 9 cha muswada kinafanya marekebisho kifungu cha 57 ambapo kifungu kipya cha tano kinaongezwa mara baada ya kifungu kidogo cha 4 ambapo kifungu hicho kinachoongezwa kinatoa mamlaka kwa Maafisa Uchunguzi kutumia kifaa cha kunasa sauti na picha wakati wa mahojiano na mtuhumiwa ambapo baada ya kumaliza mahojiano Afisa Uchunguzi anatakiwa kumpatia mtuhumiwa nakala ya mahojiano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza ni kuwa *record* ya mahojiano hayo yataruhusiwa kutumika

mahakamani bila kuwa na nakala nyingine ya maandishi. Hii ikiwa na maana kwamba, kuna uwezekano mkubwa wa kubadili ushahidi pamoja na kwamba kifungu hiki kinaweza kuwa na nia njema ila ni moja ya kifungu ambacho kinaweza kuwa hatari sana na pengine kikawanyima watu wengi haki au kuwaweka hatiani wale wasio na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi ushahidi wa sauti umekuwa ukitumiwa vibaya kutokana na uwezo wa watu binafsi kuweza kuigiza sauti za watu wengine au uwezo wa kiteknolojia katika utengeneza sauti au kubadilisha picha, hivyo kutumia ushahidi huu wa sauti ni lazima uweze kuendana na uwezo wa kubaini aina za ushahidi wa sauti ulioghushiwa au kuchakachuliwa *(tempered audio evidence)* na sauti halisi ya mtuhumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza aya ya (d) kufutwa na kufanyiwa marekebisho kwa sababu kinatoa masharti kuwa hati itakayotolewa baada ya mahojiano kwa kutumia kinasa sauti na hati kutolewa haitakuwa na haja ya Afisa Uchunguzi kumsomea mtuhumiwa maelezo yake au kuweka sahihi kila ukurasa na mwisho wa hati hiyo kama ilivyo sasa. Jambo hili halipaswi kupitishwa na Bunge hata kidogo kwani likiachwa kama kifungu hiki kinavyosema litaleta madhara makubwa kwa jamii ikiwemo ongezeko la tabia ya Askari Polisi (Maafisa Uchunguzi) kubambikiza kesi wananchi kwa kutoa maelezo ambayo hayakusemwa wakati wa mahojiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Serikali inaweza kujificha katika hoja ya uwepo wa Kanuni ambazo zitatungwa na Jaji Mkuu kama inavyopendekezwa, lakini vema ikazingatiwa kuwa ni lazima utaratibu uwekwe kwa mujibu wa Sheria ili hata Jaji Mkuu akitekeleza madaraka yake aliyopewa na sheria afanye hivyo kwa mujibu wa masharti hayo lakini sio kutoa uhalali usio na mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12 cha muswada kinafuta na kuandika kifungu cha 188 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ambao taarifa mbalimbali

za masharti zinaweza zikazuiwa baada ya maombi rasmi kutoka kwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali. Pamoja na kuwa hata kabla ya marekebisho haya sheria ilikuwa inatoa mamlaka kwa Mahakama kuzuia taarifa za mashahidi kuwekwa wazi kwa minajili ya kulinda misingi ya utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa jambo hili lisipoangaliwa vizuri litazua mtanziko wakati wa kuendesha mashauri ya jinai kwa sababu upande unaotuhumiwa unaweza kushindwa kujitetea au kumhoji shahidi ambaye taarifa na nyaraka zake hazijawekwa wazi.

Pamoja na marekebisho hayo kumpa mamlaka Jaji Mkuu kuweka utaratibu bora wa utekelezaji wa masharti hayo ni vema Serikali ikawa makini na mfumo wa utoaji haki kwa sababu wanaweza kutumia kifungu hicho kuhukumu watu kwa makosa ya kutungwa na kupelekea kuikwa kwa misingi ya haki ya mtu kujitetea pamoja na kumhoji shahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya sheria ya mapato yatokanayo na uhalifu Sura ya 256. Kifungu cha 97 cha muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 38 cha Sheria ya Mapato yatakanayo na Uhalifu ambapo Mwanasheria wa Serikali bila kushirikisha upande wa mtuhumiwa anaweza kuomba Mahakama kuzuia mali za mtuhumiwa aliyejipatia mapato kwa njia ya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaongeza mamlaka kwa Mwanasheria wa Serikali bila kushirikisha upande mwingine wa mtuhumiwa jambo ambalo linaloweza kupelekea kuharibu mfumo wa utoaji haki kwa sababu kama mtuhumiwa atashinda shauri la jinai na wakati huo huo mali zake zilishikiliwa na Serikali ni wazi kuwa atakuwa amehukumiwa kabla ya uamuzi wa Mahakama. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kifungu hiki kifanyiwe marekebisho na kutoa nafasi upande wa pili kujibu hoja za Mwanasheria wa Serikali kabla Mahakama kutoa uamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu wengi ambao mali zao zilishikiliwa na kuharibika kabla hata ya shauri la jinai

halijamalizika na baadae Mahakama kuamua na kutowakuta na hatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Sheria ya Chama cha Mawakili wa Tanganyika Sura ya 307. Madhara ya kutunga sheria kwa kuangalia mtu yaani *personalities* yanapelekea kutungwa kwa sheria ambayo ukiisoma kwa umakini inakiuka Katiba na taratibu zingine ambazo zipo kwa sasa na hazifutwa kwa minajili hiyo*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mawakili wa Tanganyika ni chama cha wataalam ambapo katika vyama hivi kuna masuala mengi mtambuka ambayo kama Serikali wanapendekeza kufanya marekebisho ni lazima waanze na sera na kuwashirikisha wadau kutoa maoni yao na sio kama Serikali inavyofanya kwa kuleta marekebisho ya Sheria ya Chama cha Mawakili kwa kutumia Marekebisho ya Sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu unawazuia viongozi wa vyama vya Siasa ambao ni Mawakili kugombea nafasi ya Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili, hata hivyo ikumbukwe kuwa Mawakili ni sehemu ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao kwa namna moja ama nyingine wanazo haki zao za Kikatiba ikiwemo haki ya ya kugombea na kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu pia unamuongezea Mamlaka Mwanasheria wa Serikali kupeleka maombi kwenye Kamati ya nidhamu ya Mawakili ya kumuondoa Wakili kwenye orodha ya Mawakili wanaoruhusiwa kufanya shughuli za kisheria ikiwa itabainika amekiuka masharti yanayopendekezwa. Ikumbukwe kuwa Mwanasheria wa Serikali ni Mjumbe katika Kamati hiyo na kumuongezea nguvu nyingine kama inavyopendekezwa itamfanya Mwanasheria Mkuu kuwa Jaji katika shauri lake mwenyewe mshiriki*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wa Vyama vya Siasa hasa wa Upinzani wameendelea kukabiliwa na

mashauri mbalimbali ya jinai na mengi ya madai. Ukisoma kwa makini masharti yanayopendekezwa na muswada kuhusu Wakili ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili utagundua kuwa huenda Wakili huyo asiweze hata kumwakilisha mteja ambaye ni kiongozi wa Chama cha Siasa. Kwa kufanya hivyo Serikali inaanza kuleta ubaguzi wa kisiasa katika taaluma ya wanasheria nchini kwa kutengeneza jinai kwenye masuala ya haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh, hitimisho imeondolewa naomba uwasilishe.

**MHE. ALLY SALEH ALLY - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hewala ahsante *In Shaa Allah* hewala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA SHERIA NA KATIBA KUHUSU MUSWADA WA MABADILIKO YA SHERIA MBALIMBALI (NA.02) WA MWAKA 2018 *(WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL (NO. 2), 2018*) - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***(Yanatolewa chini ya kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016)***

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria namba 02 ulichapishwa tarehe 08 Juni, 2018 katika juzuu namba 99 ya Gazeti la Serikali. Muswada huu unapendekeza kufanyia marekebisho ya Sheria mbalimbali 13 ambapo marekebisho hayo yanalenga kuwezesha utekelezaji wa mabadiliko ya mfumo wa kisheria baada ya kufanywa kwa marekebisho

ya mfumo huo kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali na Matangazo ya Serikali namba 48, 49 na 50 ambapo ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu, Mwanasheria wa Serikali, ofisi ya Taifa ya Mashtaka na ofisi ya Wakili Mkuu.

**1.1 Ukiukwaji wa utaratibu wa kutunga sheria**

**Mheshimiwa Spika**, ni utamaduni na msingi wa kisheria kuwa Sheria zinaanza kutungwa na kufuatiwa na Kanuni pamoja na taratibu mbalimbali za utekelezaji kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Serikali na maisha ya wananchi. Utaratibu huu unakiukwa na Serikali ya awamu ya tano, hii ni kwa sababu Serikali ya awamu ya tano inaanza kutoa matamko na maelekezo kwanza ndipo unafuata utaratibu wa kisheria.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali hutakiwa kufanya kazi zake zote kwa mujibu wa Sheria, ibara ya 63(3)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kutunga Sheria. Kama Serikali inatoa maelekezo kupitia kwa Rais au Mawaziri na baada ya hapo kuleta muswada wa Sheria kuhalalisha maamuzi na maelekezo ya Serikali, ni ishara kuwa Serikali inapuuza mamlaka na hadhi ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka 2016 akiwa katika Mkutano Mkuu wa CCM Rais John Pombe Magufuli alitangaza na kuelekeza Serikali kuhamia Makao Makuu Dodoma bila uwepo wa Sheria. Pamoja na Kamati ya Bunge ya Sheria na Katiba ya Bunge kuhoji jambo hilo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa kauli kuwa jambo hilo linatakiwa kufanyiwa kazi na ofisi ya Waziri Mkuu huku akijua yeye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali yote bila kujali Wizara na Idara. Hatimaye katika Mkutano huu wa Bunge Sheria ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali kupitia muswada wa Sheria namba 03 uliwasilishwa na kupitishwa na Bunge pamoja na kuwa tamko lilitoka muda mrefu na idadi kubwa ya Watumishi kuhamishiwa Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, katika muswada huu yapo maeneo kadhaa ambayo Serikali inahalalisha uamuzi ambao

umeshafanyika kwa siku kadhaa zilizopita. Mathalani kuanzishwa kwa ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kulifanyika wakati ambapo Sheria zinazobadilishwa katika muswada huu zinatoa utaratibu tofauti na maamuzi ambayo yalishafanyika bila kuangalia masharti ya Sheria hiyo pamoja na kuwa utaratibu wa utangwaji wa Sheria na maamuzi ulitakiwa kuangalia masharti ya Sheria zilizopo kabla ya kufanya maamuzi.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Mheshimiwa Spika**, mazingira ni hayohayo hata katika marekebisho ya Sheria ya Chama cha Mawakili wa Tanganyika yanayopendekwa na kifungu cha 105 cha muswada ambapo marekebisho yanayopendezwa yanawanyima haki watu ambao ni watumishi wa umma, Madiwani, Wabunge na Viongozi wa Vyama vya Siasa kuwa wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Chama cha Mawakili.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Mheshimiwa Spika**, ni jambo la kusikitisha kuwa Serikali sasa inatunga Sheria kwa kumlenga mtu au taasisi au kumtafutia mtu wadhifa, na haitungwi kwa malengo mahususi ya kuwasaidia wananchi. Haitashangaza huko baadaye sheria nyingi kufutwa baada ya CCM kukataliwa na wananchi kwa sababu ya kushindwa kusimamia taratibu ambazo tumejiwekea kwa muda mrefu.

## 2.0 MAREKEBISHO YA SHERIA MAMLAKA NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KABIDHI WASII MKUU SURA YA 27

**Mheshimiwa Spika,** katika marekebisho ya Sheria hii ambayo yanalenga kifungu cha 2, cha 3A na kifungu cha 4 ambapo lengo kubwa ni kuanzisha nafasi mpya ya Naibu Kabidhi Wasii Mkuu (Deputy Administrator General) pamoja na kumnyanga'nya Waziri mamlaka ya kumteua Kabidhi Wasii Mkuu na badala yake Rais ndie atafanya uteuzi huo.

**Mheshimiwa Spika,** ni wazi kuwa kifungu cha 36 (2) cha Katiba ya nchi kinampa Rais mamlaka ya kuteua watu katika kushika nafasi au madaraka ya kiuongozi. Pamoja na mamlaka hayo ya kikatiba, kimsingi kifungu hiki kina ukakasi mkubwa hasa pale ambapo nchi inaweza kuwa na kiongozi mwenye mamlaka makubwa kama hayo ya kiuteuzi na akayatumia vibaya madaraka hayo.

**Mheshimiwa Spika,** nayasema haya kwa kuwa wateule wengi wamekuwa wakifanya kazi kwa maelekezo badala ya sheria na kanuni zilizowekwa hususani katika utekelezaji wa majukumu ambayo yanaweza kugusa maslahi ya mteua, haishangazi siku hizi ukisikia mtumishi wa umma mwenye mamlaka akisema anashindwa kufanya maamuzi fulani fulani kwa sababu amepokea maelekezo kutoka juu. Mathalani katika majukumu ya Kabidhi Wasii Mkuu na Naibu Wasii Mkuu katika yale wanayoyasimamia ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za ufilisi kwa watu binafsi (bankruptcy,ufilisi wa kwenye makampuni (company liqudation) ,kusajili na kutoa hati ya usajili kwa wadhamini wa vyama vya siasa,vikundi,makanisa,misikiti na mali ikiwa ni pamoja na kufuta usajili. Kwa uzito na unyeti wa majukumu haya, isipoangaliwa vizuri mamlaka ya Rais katika uteuzi yanaweza kutumika vibaya katika kushawishi uonevu, hujuma na udhalili kwa wale wenye mrengo tofauti na matakwa ya Rais.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuletwa kwa marekebisho ya sheria hii, Waziri ndie aliyekuwa na mamlaka ya kufanya uteuzi huu. Hii ikiwa kwamba endapo uteuzi uliokuwa umefanywa na Waziri haukufuata taratibu au una mapungufu Raisi anauwezo wa kutengua uteuzi huo. Endapo Rais kama binadamu anapoteua mtu bila kufuata taratibu au vigezo tujiulize ni mamlaka gani zaidi itamuwajibisha?

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inazidi kuutaka umma wa Watanzania kuendelea kupigania hitaji la upatikanaji wa katiba mpya ili kupunguza mamlaka ya Rais hususani ya kufanya teuzi katika idara na vitengo nyeti ili

kuepuka kufuata mamlaka na matakwa ya mtu binafsi badala ya matakwa ya taasis ili kuepusha nchi yetu na udikteta.

## 3.0 MAREKEBISHO YA SHERIA YA MWENENDO WA MAKOSA YA JINAI SURA YA 20

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 9 cha muswada kinafanya marekebisho kifungu cha 57 ambapo kifungu kipya cha 5 kinaongezwa mara baada ya kifungu kidogo cha 4 ambapo kifungu hicho kinachoongezwa kinatoa mamlaka kwa maafisa uchunguzi kutumia kifaa cha kunasa sauti na picha wakati wa mahojiano na mtuhumiwa ambapo baada kumaliza mahojiano Afisa uchunguzi atatakiwa kumpatia Mtuhumiwa nakala ya mahojiano hayo. Jambo la kushangaza ni kuwa rekodi ya mahojiano hayo yataruhusiwa kutumika mahakamani bila kuwa na nakala nyingine ya maandishi. Hii ikiwa na maana kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kubadili ushahidi. Pamoja na kwamba kifungu hiki kinaweza kuwa na nia njema ila ni moja ya kifungu ambacho kinaweza kuwa hatari sana na pengine kikawanyima watu wengi haki au kuwaweka hatiani wale wasio na hatia.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi ushahidi wa sauti umekuwa ukitumiwa vibaya kutokana na uwezo wa watu binafsi kuweza kuigiza sauti za watu wengine , au uwezo wa kiteknolojia katika kutengeneza sauti. Hivyo, kutumia ushahidi huu wa sauti ni lazima uweze kuendana na uwezo wa kubaini aina za ushahidi wa sauti ulioghushiwa au kuchakachuliwa (tempered audio evidence) na sauti halisi ya mtuhumiwa

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza aya ya (d) kufutwa au kufanyiwa marekebisho kwa sababu kinatoa masharti kuwa hati itakayotolewa baada ya mahojiano kwa kutumia kinasa sauti na hati kutolewa haitakuwa na haja ya afisa uchunguzi kumsomea mtuhumiwa maelezo yake au kuweka sahihi kila ukurasa na mwisho wa hati hiyo. Jambo hili halipaswi kupitishwa na Bunge lako hata kidogo kwani likiachwa kama kifungu hiki kinavyosema

litaleta madhara makubwa kwa jamii ikiwemo ongezeka la tabia ya Askari Polisi(Afisa uchunguzi) kubambikiza kesi wananchi kwa kutoa maelezo ambayo hayakusemwa wakati wa mahojiano.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa Serikali inaweza kujificha katika hoja ya uwepo wa Kanuni ambazo zitatungwa na Jaji Mkuu kama inavyopendekezwa lakini vema ikazingatiwa kuwa ni lazima utaratibu uwekwe kwa mujibu wa Sheria ili hata Jaji Mkuu akitekeleza madaraka yake aliyopewa na Sheria afanye hivyo kwa mujibu wa masharti hayo lakini sio kutoa uhalali usio na mipaka.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 12 cha Muswada kinafuta na kuandika kifungu cha 188 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ambao taarifa mbalimbali za mashahidi zinaweza zikazuiwa baada ya maombi rasmi kutoka kwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali. Pamoja na kuwa hata kabla ya marekebisho haya Sheria ilikuwa inatoa mamlaka kwa Mahakama kuzuia taarifa za mashahidi kuwekwa wazi kwa minajili ya kulinda misingi ya utoaji haki.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa jambo hili lisipoangaliwa vizuri litazua mtanziko wakati wa kuendesha mashauri ya jinai kwa sababu upande unaotuhumiwa unaweza kushindwa kujitetea au kumhoji shahidi ambaye taarifa na nyaraka zake hazijawekwa wazi. Pamoja na marekebisho hayo kumpa mamlaka Jaji Mkuu kuweka utaratibu bora wa utekelezaji wa masharti hayo ni vema Serikali ikawa makini na mfumo wa utoaji haki kwa sababu wanaweza kutumia kifungu hicho kuhukumu watu kwa makosa ya kubumba na kupelekea kuikwa kwa misingi ya haki ya mtu kujitetea pamoja na kumhoji shahidi.

## 4.0 MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU SURA YA 256

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 97 cha muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 38 cha Sheria ya Mapato yatakanayo na Uhalifu ambapo Mwanasheria wa Serikali bila

kushirikisha upande wa mtuhumiwa anaweza kuomba Mahakama kuzuia mali za mtuhumiwa aliyejipatia mapato kwa njia ya uhalifu.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili linaongeza mamlaka kwa Mwanasheria wa Serikali bila kushirikisha upande mwingine wa mtuhumiwa jambo linaloweza kupelekea kuharibu mfumo wa utoaji haki kwa sababu kama mtuhumiwa atashinda shauri la jinai na wakati huo huo mali zake zilishikiliwa na Serikali ni wazi kuwa atakuwa amehukumiwa kabla ya uamuzi wa Mahakama. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kifungu hiki kifanyiwe marekebisho na kumpa nafasi upande wa pili kujibu hoja za Mwanasheria wa Serikali kabla Mahakam kutoa uamuzi.

**Mheshimiwa Spika**, wapo watu wengi ambao mali zao zilishikiliwa na kuharibika kabla hata ya shauri la jinai halijamalizika na baadaye Mahakama kuamua na kutowakuta na hatia.

**5.0 MAREKEBISHO YA SHERIA YA CHAMA CHA MAWAKILI WA TANGANYIKA SURA 307**

**Mheshimiwa Spika**, madhara ya kutunga Sheria kwa kuangalia mtu au *personalities* yanapelekea kutungwa kwa Sheria ambayo ukiisoma kwa umakini inakiuka Katiba na taratibu zingine ambazo zipo kwa sasa na hazifutwa kwa minajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Chama cha Mawakili wa Tanganyika ni Chama cha Wataalamu ambapo katika vyama hivi kuna masuala mengi mtambuka ambayo kama Serikali wanapendekeza kufanya marekebisho ni lazima waanze na sera na kuwashirikisha wadau kutoa maoni yao na sio kama Serikali inavyofanya kwa kuleta marekebisho ya Sheria ya Chama cha Mawakili kwa kutumia marekebisho ya Sheria mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unawazuia viongozi wa Vyama vya Siasa ambao ni Mawakili kugombea nafasi ya

Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili, hata hivyo ikumbukwe kuwa Mawakili ni sehemu ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao kwa namna moja ama nyingine wanazo haki zao za kikatiba ikiwemo haki ya ya kugombea na kuchaguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, muswada huu pia unamuongezea mamlaka Mwanasheria wa Serikali kupeleka maombi kwenye Kamati ya Nidhamu ya Mawakili ya kumuondoa Wakili kwenye orodha ya Mawakili wanaoruhusiwa kufanya shughuli za kisheria ikiwa itabainika amekiuka masharti yanayopendekezwa. Ikumbukwe kuwa Mwanasheria wa Serikali ni Mjumbe katika Kamati hiyo, kumuongea nguvu nyingine kama inavyopendekezwa itamfanya Mwanasheria Mkuu kuwa Jaji katika shauri lake mwenyewe.

**Mheshimiwa Spika**, viongozi wa Vyama vya Siasa hasa wa Upinzani wameendelea kukabiliwa na mashauri mbalimbali ya jinai na mengine ya madai. Ukisoma kwa makini masharti yanayopendekezwa na muswada kuhusu Wakili ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili utagundua kuwa huenda Wakili huyo asiweze hata kumwakilisha mteja ambaye ni kiongozi wa Chama cha Siasa. Kwa kufanya hivyo Serikali inaanza kuleta ubaguzi wa kisiasa katika taaluma ya Wanasheria nchini kwa kutengeneza jinai kwenye masuala ya haki.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Ally Saleh (Mb)
**KNY. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**
7 Septemba, 2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh, sasa tunaanza mjadala wetu. Tutaanza na Mheshimiwa Salome Makamba, karibu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba na marekebisho haya ya sheria mbalimbali za nchi yetu. Kwanza kabisa siku ya leo ikiwa ni siku maaalum nianze kwa kumtakia uponyaji mwema Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye kimsingi yeye ni moja kati ya watu waliopelekea baadhi ya marekebisho makubwa ya sheria ya Chama cha Mawakili Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pale alipoishia Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, suala la kutenganisha Chama cha Mawakili kwamba viongozi wa chama hicho wasiwe wanasiasa linakiuka Katiba kwa kiasi kikubwa na linakiuka Katiba kwa sababu siasa ni maisha na maisha ni siasa, huwezi kuvitenganisha leo humu Bungeni tunao viongozi wa vyama mbalimbali vya kitaaluma, wapo viongozi wa bodi ya mainjinia, wapo viongozi wa bodi ya wahandisina na viongozi wa Chama cha Mawakili pia wanayo haki ya kuwa Wabunge na wanaokuwa na haki ya kuwa wawakilishi katika taaluma yao. Hilo tunapaswa tuliangalie kwa makini kwa sababu mimi naliona linachukuliwa zaidi kwa kulenga baadhi ya watu fulani na sio sheria kama tulivyofundishwa utungaji wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda mbele zaidi naomba nijielekeze kwenye sheria marekebisho ya sheria inayohusiana na *Administrator General* wa *RITA.* Waziri ameleta marekebisho anasema Mkurugenzi..., wameandika kwa Kiswahili lile neno nalo ni gumu, lakini ni *Administrator General* na *Deputy* wateuliwe na Mheshimiwa Rais. Hawa watu ukisoma katika moja kati ya majukumu ya *Administrator General* au hiyo taasisi moja kati ya majukumu yake ni kusajili bodi za wadhamini, wanasajili bodi za wadhamini wa vyama vya siasa, mambo ya kidini na mambo ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwenyekiti wa chama cha kisiasa. Unapompa mamlaka ya kumteuwa mtu anayesajili bodi ya wadhamini wa vyama vya kisiasa na mwenye mamlaka ya kufuta bodi hiyo ya wadhamini unaondoe ile *impartibility condition* ambayo *administrator general* anatakiwa kuwa nayo. Leo tunaweza kuona ni sawa kwa sababu Mheshimiwa Rais ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, lakini sisi watunga sheria lazima tujue leo kwako kesho kwangu, kesho itakapokuwa kwa upande mwingine Mwenyekiti wa chama kingine akapewa mamlaka ya kuteua *Administrator General* na *Deputy* wake madhara yake yatakuwa makubwa kwa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaiondoa ile dhana ya demokrasia ambao imejengwa na waasisi wa Taifa hili, mimi namshauri Mheshimiwa Waziri tuweke na sio tu kwa sababu ni Mwenyekiti wa chama lakini tuangalie mambo ya *cheques and balance* hebu angalia Mheshimiwa Rais akikosea kumchagua *Administrator General,* nani anaweza kutengua jambo hilo.

Nimesikitishwa na kufutwa mfano uliowekwa kwenye kitabu cha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa sababu umetolewa mfano ambao uko dhahiri. Sasa kwa sababu aliyevurunda kwenye kitu hicho yuko humu ndani amepata mamlaka ni ukurasa wa ngapi samahani naomba nisome, ukurasa wa tano imeelezwa vizuri tu Mheshimiwa Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge aliwahi kufanya uteuzi wa Mkurugenzi Kukaimu nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa *NSSF* na kwa sababu alikosea Rais alipata mamlaka ya kutengua uteuzi ule, lakini kwa sababu Waziri huyo yuko humu ndani amepata Mamlaka ya kufuta kwenye *Hansard* na sisi tunasema *Alhamdullah*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kutoa mifano ambayo imetokea kwenye Taifa hili sio *discussion power* ya mtu mmoJa hili ni suala la Taifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome subiri Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala si suala hapa la kukosea ama kutokukosea na wala si suala la kujadili kwa nini kifungu hicho kimefutwa, ni suala la kikanuni.

Ninaomba niseme utaratibu huo nikirudi kwenye Kanuni ya 64(1)(e) lakini ninapozungumza Kanuni hiyo ya 64(1)(e) ninakwenda pia kwenye ibara ya 36(1) ambayo ibara hiyo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hiyo ya 36(1) kwa ruhusa yako naomba niisome tu namheshimu sana mdogo wangu Salome na wala si kwamba ninazungumza kukosea ama kutokukosea kwa Waziri yeyote hata mimi nazungumza masuala ya kiutaratibu ya Kikatiba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais atakuwa na madaraka na yeye ndio mwenye madaraka ya kuteua watu, kushika nafasi za madaraka na viongozi wanawajibika kuweka sera na idara za Serikali na watendaji wakuu wanaowajibika kusimamia utekelezaji wa sera na taasisi hizo katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano na nafasi hizo zimetajwa katika Katiba hii, lakini Rais huyo huyo bila kuathiri masharti yoyote ibara ya 36(1), mamlaka ya Mheshimiwa Rais atakuwa na mamlaka ya kuanzisha kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Kwa hiyo kuna 36(1), kuna 36(2) hayo yote ni madaraka. Kwa hiyo kama haya ni madaraka ya Rais mimi kama Waziri ninapokosea ama nisipokosea, lakini madaraka haya ni ya Mheshimiwa Rais na sio suala la ku-*influence* kitu chochote, ni lazima tupambane kwenye...

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnadhimu wa upande wa pili ameomba kuhusu utaratibu kwa kusimamia Kanuni ya 64(1)(e) nacho kinasema; "Hatazungumzia mwenendo wa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Spika, Mbunge Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki ispokuwa tu kama kumetolewa hoja mahususi kuhusu jambo husika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo husika ndio hilo liko mzani na mfano uliotolewa ni dhahiri na mtoaji aliyekuwa anatoa maoi yake yuko sahihi hajavunja kanuni yoyote ya sheria au hajavunja kanuni yoyote ya Bunge hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome naomba uendelee lakini usirudie yale ambayo tuliyafuta kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani.

Narudia kusema tena yale ambayo yamefutwa kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni na Katiba naomba usiyarejee.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme hivi tunaposema ukimweka *Administrator General* ateuliwe na Mheshimiwa Rais tutakuwa tunakosa nafasi ya kurekebisha *Administrator General* kama a-*fit* kwenye ile *position*. Tunapomuweka Waziri awe na mamlaka yale endapo Waziri akikosea au *Administrator General* akishindwa ku-*perform* Mheshimiwa Rais an a fursa ya kumbadilisha yule *Administrator General* ndio mfano wangu na ndicho alichokikiri Mheshimiwa Jenista hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia mbaya tumeona teuzi nyingi zinafanyika kimakosa, tumeona wateule wengi wanashinda ku-*perform to the expectation of the*

*government* tunawezaje kuwatoa wakiwa hawa watu ni *Presidential Appointees*. Wakati mwingine tujifunze kutokana na makosa kuhusiana na jambo hili ndio maana tunasema fursa inapotokea Waziri hafanyi vizuri au ameteua mtu aliyeshindwa ku-*perform* vizuri tunapata *entrance* ya kuweza kumuweka mtu atakaye-*perfom* kwa maslahi mapana ya Taifa hili kupitia kiti cha Rais *and that is my all point. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja kwenye sheria najua hilo Mhsehimiwa Waziri amelichukua niende kwenye sheria ya urejeshwaji wa mali zitokanazo na uhalifu ambayo ni sehemu ya 13 ya marekebisho na ni Sura ya 256.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii samahani Mheshimiwa Waziri anasema Mkurugenzi wa Mashtaka kuweza kuwasilisha Mahakamani maombi ya upande mmoja yaani asikilizwe yeye peke yake, maombi ya kukamata mali iliyopatikana kwa njia ya uhalifu ambayo ama iko hatarini kupotea au kuharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia kwenye Taifa hili watu wanakamatiwa mali zao, wakati mwingine ni kwa hila tu wala hakuna uhalali wowote wa kukamata zile mali, watu wanafungiwa akaunti zao kwa hila tu basi hilo tuliache. Lakini kesi inaendelea Mahakamani mali zinakamatwa mtu anashindwa kuendesha maisha yake, anashindwa kuendesha biashara hilo tumeliacha leo huyo Mwendesha Mashtaka kabla Mahakama haijaamua kama zile mali ni za uhal ifu ama sio za uhalifu anapeleka maombi mali zile ziuzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza mazingira hapa ya kutaka kuwafanya watu wawe wanyonge ndani ya Taifa lao. Nafasi hii ni rahisi sana kuwa kutumika vibaya na Mwendesha Mashtaka na hii ni kama tu msingi wa ile hoja ya hati anayopeleka Mwendesha Mashtaka ambayo umefutwa kimahama anapeleka kuzuia mtu asipate dhamana kwa sababu yaani sababu anazozijua yeye mwenyewe na haulizwi mahali popote, ile ilifutwa kwa msingi

kama huu kwa sababu Mwendesha Mashtaka anaweza kum-*misuse powers* alizopewa. Mimi niiombe Serikali kwanza maombi ya kuweza kuziuza mali zile yasiwe *exparte,* yasikilizwe kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwe MWenyekiti, lakini pili maombi yale iwe ni *desecration* ya mahakama ku-*decide* kwamba mali zile ziweze kuuzwa ama zisiuzwe bila kumathiri mmiiki wa malizile kwa sababu kwa nchi hii ya leo unapokwenda najisikia vibaya kusema hivi kumekuwa na uvunjwaji mkubwa wa kanuni, sheria na taratibu hasa kwa Serikali ambayo tunaambiwa kila mtu ambaye ameteuliwa na Serikali hamna *neutral,* lazima kwanza mezani ukae na Ilani ya Chama cha Mapinduzi na hakuna *neutral* lazima uegemee upande wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali tuliyofikia sasa hivi uhuru wa Mahakama hawa Mawakili huko hali ni mbaya wote wameambiwa wanatekeleze ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa hali hii tukaruhusu na mali za watu zitaifishwe na kuuzwa, watu watafilisika, mali imeshauzwa, Serikali yenyewe hii iko hoi bin taabani ikija kuonekana mtu yule mali zake ni halali atachukua miaka 100 kuja kulipwa mali zake na kuirudishiwa.

Kwa hiyo, mimi niombe ombi kwa Mheshimiwa Waziri tuondoe suala la *exparte* kwenye maombi ya kuuza hizi mali, lakini iwe ni *desecration*ya Mahakama, uhuru wa Mahakama uzingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwe Mwenyekiti, mwisho kabisa niongelee hili suala la ushahidi wa ku-*record* kweli ni mzuri, mnasema kwamba shahidi atarekodiwa ushahidi wake na atapewa nakala. Niombe tunarudi kule kule sasa hivi tumekuwa kama watu ambao tunaishi kwa tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtuhumiwa anahojiwa yuko mahabusu, anamaliza kuhojiwa kwa video na picha anaambiwa anapewa nakala yake anaipeleka wapi? Uwezekano ni mkubwa sana kwa Waendeshwa Mashtaka

ku-*temper* na hizi *document* kwa hali ilivyo. Mimi nawapenda sana Waendeshwa Mashtaka na ni taaluma yangu lakini niseme tumefika pabaya lazima tupige ndulu. Ushahidi huu uandikwe kwa maandishi, usainiwe na chini ya yule anayechukuliwa ushahidi huu uwe chini ya mwanasheria, uwe chini ya wakili, usainiwe ndipo akabidhiwe ili...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Nakushukuru sana kwa *interest* ya muda nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamba, tunaendelea na Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka na baadae Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ajiandae.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia huu Muswada wa Sheria Wa Marekebishowa Sheria Na. 2 wa mwaka 2018 yaani *the Written Laws Miscellaneous Amendment Act, No. 2 of 2018.*

Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta muswada huu ambao una marekebisho ambayo ni ya muhimu sana, lakini la pili nampongeza Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu yenu kwa jinsi ambavyo mlikuwa mmejipanga mlipokuwa mkija kwenye Kamati mlionesha ushirikiano wa hali ya juu mpaka tumefikia hapa tulipo.

Mheshimiwa Mweyekiti, mimi sina mengi sana kwenye muswada huu kwa sababu mambo mengi tulikubaliana kwenye Kamati baada ya Serikali kama nilivyosema ilionesha ushirikiano mkubwa katika kurekebisha vifungu mbalimbali kwa hiyo, nntakuwa na machache.

Mheshimiwa Mweyekiti kwa mfano kwenye sehemu ya sita ya marekebisho ya muswada huu inahusianana Sura ya 89 ambayo inahusiana na ukomo ambayo ni *The Law of Limitation Act, Cap.* 89. Naipongeza Serikalikatika eneo hili

sana kwa sababu tumekuwa na matatizo mbalimbali na hasa kwenye kesi za msingi ambazo zimekuwa zikitupwa na Mahakama kwa sababu tu ya kitu kinachoitwa *legal technicalities.* Kesi ya msingi inakuwa inatupwa, muda unakuwa umepita, lakini sasa kwa kifungu hiki kinamruhusu sasa Mheshimiwa Waziri anayehusika na Wizara husika kufungua mashauri nje ya muda. Tumekuwa tukipoteza kesi nyingi hasa kwenye Halmashauri zetu kwa sababu ya kifungu hiki. Kwa hiyo, naipongeza Serikali sana kwa kuleta kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye sehemu ya 13 ya Marekebisho ya Sheria ya Urejeshwaji wa Mali, Sura ya 256 mali zinazopatikana kwa njia ya uhalifu. Ni kitu ambacho kimetokea mara nyingi sana kwamba hata katika mazingira ya kawaida sio Wabunge tu hata wananchi wa kawaida unaangalia kitu au unaangalia mali za mtu ambazo ukiangalia mazingira ya kawaida ile *circumstantial evidence* unaona kabisa kwamba mali hizo hazikupatikana kwa njia iliyo halali. Kwa hiyo, kwa kuleta kifungu hiki ni vizuri sana ila isipokuwa tu kwamba kifungu hiki kinapotekelezwa basi mali zile isije ikawa mtu labda ana hinda tu au mtu kaona tu kwamba huyu kwa nini ana mali nyingi basi kifungu hiki kitumike kuhakikisha kwamba haki inatendeka kama ilivyokusudiwa na asionewe mtu kwa sababu haki ya kumiliki mali ni haki ya Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ibara za 14 mpaka 19 kwenye masuala ya urejeshwaji wa wahalifu yaani *extradition.* Katika kifungu hiki kulikuwa na takwa hili ambalo lilikuwa linahitaji kwamba mhalifu akae siku 15 kabla hajapelekwa mahali au hajasafirishwa kwenda kukabiliana na tuhuma au shitaka linalomkabili. Hizo siku 15 kuna washitakiwa ambao wanahitajiwa kwa haraka, sasa kwa kuboresha kifungu hiki kwamba mshitakiwa aweze kuletwa hata kabla hazijafika hizo siku 15 basi kitapelekea ufanisi wa kesi pia kwenda haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna ibara ya tisa ambayo inarekebisha kifungu 57 kinachohusu utaratibu wa

kurekodi mahojiano. Kifungu kipo vizuri lakini mimi wasiwasi wangu hapa vile vinasa sauti sijui vitakuwa *specified* namna gani, kwa sababu viko vifaa vya aina nyingi na vingine ni rahisi sana kuwa *tempered*, sasa sijui Wizara katika hili imejipanga hasa kuwa na vifaa. Je, vitakuwa ni vifaa maalum ambavyo vitakuwa vinafahamika kwamba kifaa hiki hasa ndicho kinachotumika, lakini pia na ubora wa vifaa hivi ili ule utoaji wa ushahidi kwa kutumia vifaa hivi basi usije ukawa una mapungufu.

Mheshimiwa Mweyekiti, lakini kuna sehemu ya sheria hii ya Chama cha Mawakili, mimi naunga mkono kama ambavyo inapendekezwa ingawa kuna vitu vichache na naomba nikatae hii hoja ya kwamba kuna watu *specific* wanalengwa hapa. Kwa kutungwa sheria hii hapa hakuna *specialization* yoyote ya mtu kwa sababu wote tunahusika na sheria hii na mara nyingi kwenye *practice* sheria, haijawahi kutokea kwamba sheria hiyo inafanya kazi kwa Wapinzani imefanya kazi hata kwa Chama Tawala na mifano ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu kwenye lile suala la kazi au majukumu ya Baraza la Mawakili pamoja na ile *secretariat* wakati inaanzishwa sheria hii mwaka 1954 kwa wakati ule ilikuwa ni sawasawa kabisa, lakini mazingira kwa sasa yamebadilika sana, nadhani kuna umuhimu wa kuboresha baadhi ya majukumu ya Baraza, kwa mfano ukiangalia kwenye hii sheria *secretariat* inaonekana imepokwa majukumu mengisana yamepelekwa kwenye Baraza. Sasa mimi nadhani wayaangalie upya suala la lile ripoti za mwaka kuzipeleka kwenye Baraza hii ilikuwa ni kazi ya *secretariat* kabisa ukiangalia. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali iangalie upya ya katika yale majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Ahsante Mheshimiwa Mwakasaka, tunaendelea Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro na baadae Mheshimiwa Ally Saleh ajiandae.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia muswada huu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitoe shukrani zangu za dhati kwa WaziriPro Kabudi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika muswada huu. Muswada huu umebeba sheria 13 ukijumuisha vifungu 108; kuufikisha hapa ulipofika si kazi ndogo, kwa hiyo, tunatoa pongezi za dhati kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nichangie masuala machache, suala la kwanza ni Sheria ni ya Mamlaka ya Majukumu ya Kabidhi Wasii. Sheria hii inapendekeza Kabidhi Wasii na Msaidizi wake waweze kuteuliwa na Rais. Lakini haijaishia hapo tu, nimesema ni mtu au watu ambao lazima wawe na sifa ya kuteuliwa kuwa Majaji. Kwa hiyo sio kama Rais atateua kila mtu hapana huyo mtu awe na sifa ya kuweza kuwa Jaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi huu wa Rais unazingatia Katiba, ukisoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa kwenye ibara ya 36 (1), (2) na (3) zinampa Mamlaka Rais kuteua viongozi wa taasisi mbalimbali. Kwa hiyo leo tukisema tutunge sheria ya kupingana na Katiba sisi ndio tutakuwa tunafanya kosa. Kwa hiyo iko sahihi kabisa hasa ukizingatia kwamba mtu huyu anapewa mamlaka ya kusimamia sheria tisa, sio sheria moja sheria nyingine tisa, kwa hiyo ni nafasi muhimu sana nafasi ambayo uteuzi wake mamlaka yanapaswa kuwa ni Rais.

Mheshimwa Mwenyekiti, naomba niongelee mabadiliko katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, kuna mabadiliko mengi yanapendekezwa hapa ukiachilia mbali yale ya tafsiri ambayo yanatokana na kubadilika kwa muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Naomba niongelee suala la uchukuaji wa ushahidi wa kieletroniki, wengi wameongea na kuna mjadala mkubwa pia kuhusiana na suala hili. Kifungu kinachoongezwa hapa, ni kifungu cha 57(5) kinaleta suala jipya. Lakini tujiulize suala lipya hili linakuja

kutibu kitu gani? Lazima tuzingatie ukweli kwamba moja kumekuwa na maendeleo makubwa sana katika teknolojia hii ya *electronic*, lakini pili watuhumiwa nao wanahitaji haki yao ya kuhakikisha kwamba walichokisema wakati wa upelelezi ndio hicho hicho kinawasilishwa mahakamani hivi leo. Kwa hiyo Sheria ya Ushahidi Sura Namba 6 ilifanya marekebisho kupitia kifungu cha 40A, kifungu cha 76 na kifungu cha 78(a) kuruhusu kupokelewa ushahidi wa kielektroniki Mahakamani. Sasa Sheria ya Ushahidi imeruhusu kupokelewa, lakini kulikuwa hakuna sheria ambayo inasema ushahidi huo utapatikana vipi, utakusanywa vipi, utarekodiwa vipi? Sasa mabadiliko haya ya kifingu cha 57(5) yanakuja kutibu hilo sio tu tuongelee upokelewaji wake Mahakamani, lakini tuhakikishe huu ushahidi tunaupataje ili tusije tukaleta matatizo katika upatikanaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako tukufu lirejee kwenye *Written Laws Miscellaneous of Amendment Act No. 2 of 2017* ambayo ndio ilijadili na kupitisha upokeaji ushahidi wa ushahidi wa kielektroniki Mahakamani. Sasa wakati ule linajadiliwa hili ziliongelewa sheria mbalimbali kama *Cyber Crime Act,* Sheria ya Ushahidi, Sheria ya Mawasiliano na *Electronic Transaction Act* ambazo kwa ujumla zilikuwa zinachagiza upokelewaji wa ushahidi huo Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kifungu cha 57(5) kilichopendekezwa kuna mambo ambayo ni vizuri sana tuyazingatie, moja; sehemu (b) inasema Mtu atakayefanyiwa hayo mahojiano ya kielektroniki lazima atataarifiwa kwamba sasa tunatumia teknolojia hii ili asichukuliwe kwa ghafla na ili kumpa haki yake. Lakini sehemu (c) inasema kwamba kile kilichorekodiwa nakala pale pale atapewa yule aliyofanyiwa hiyo *recording.*

Kwa hiyo hii inahakikisha na kuondoa kabisa uwezekano wa kwenda kuibadilisha ile nakala iliyobaki mikononi mwa polisi kwa sababu huyo mtuhumiwa aliyerekodiwa atakuwa nayo. Lakini pia baada ya mahojiano hayo kutakuwa na *certificate*/kutakuwa na hati na ambayo

itakuwa imesainiwa pia na yule mtu aliyekuwa amefanyiwa hiyo *recording.* Kwa hiyo kifungu hiki hakiepukiki, tunakwenda sambasamba na teknolojia na hakiondoi haki ya ku-*record* kwa maandishi niliyokuwa nayo zamani ila kinakuja kuongeza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ni cha 188 ambacho kinaelezea kwa upana wake jinsi ya kuwalinda mashahidi, hivi sasa kwenye kesi mbalimbali mashahidi wanashindwa kutoa ushahidi kutokana na kutishiwa na kifungu hiki niipongeze sana Serikali kwa sababu kimeazimwa kutoka kwenye *Rome Statute* sheria ambayo imeanzisha Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu ya *ICC* imeazimwa kule, kwa hiyo ina kiwango cha kimataifa na sisi tunakileta kiwango cha kimataifa katika sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niruhusu niongelee kuhusiana na masuala ya mali ya uhalifu, hapa hatuongelei mali kwa ujumla wake, tunaongelea mali iliyopatikana kwa njia ya uhalifu. Wanasheria wanafalsafa moja wanasema mtu asinufaike kutokana na uhalifu wake, *no one should benefit from his own wrong.* Kama umechuma mahali kutokana na uhalifu acha sheria ichukue mkondo wake, lakini naomba nitoe ufafanuzi kwamba suala la kukamata mali duniani kote lazima linafanyika *exparte*, kwa nini? Mali inaweza ikawa ni fedha iliyoko benki. Unapotaka kwenda Mahakamani msikilize pande zote mbili siku ya pili ile fedha imehama benki utaikamata wapi? Mali inaweza ikawa ni nyumba, gari, unapoweza kufanya *application* ukaisikiliza mtu anahamisha hiyo mali, kwa hiyo kukamata dunia yote inafanyika *exparte.* Isipokuwa ku-*dispose,* kuuza hiyo inakuwa *interpret* na sheria hii haijasema kwamba itauza *exparte* hapana, imesema itakamata *exparte*.

Mheshimiwa Mwenyekti, naomba kuwakilisha naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, tunaendelea na Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kupata nafasi kuchangia walau kwa uchache katika muswada uliokuwa mbele yetu, lakini kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, lakini nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kumjaalia afya inayoimarika Mheshimiwa Tundu Lissu ambayo siku kama ya leo mwaka jana dakika chache tu kutoka sasa alinusurika kifo kutoka kwenye shambulio lililotokea hapa Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotanguliza kusema na mimi nina machache tu ya kuchangia katika hili na kubwa ni kuendelea kushangazwa kwangu na namna ambavyo tuna *misuse* nafasi ya kufanya mabadiliko ya sheria mbalimbali, kwamba miswada inayoletwa kwa ajili ya kufanya marekebisho ya sheria ina donyoadonyoa tu vitu vidogo vidogo na kuacha vitu vingine, jambo ambalo linatupelekea baada ya muda mfupi tuone tena inaletwa tena sheria hizo hizo kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hii sheria inayofanyiwa mabadiliko ya *TLS* mbali ya hiki kitu kimoja labda kwa maslahi mapana ya Serikali ndio wamekuja kufanyia marekebisho wameacha vitu vingi ambavyo *TLS* ilikuwa ikivilalamikia. Kwa muda mrefu *TLS* ilikuwa ikilalamika kwamba kulazimishwa kufanya Mkutano wa nusu mwaka kwao ni gharama kubwa na ni mzigo mkubwa kwa *TLS* imepeleka malalamiko hayo Serikalini, Mheshimiwa Waziri anafahamu, *AG* anafahamu lakini humu wanashindwa kuyafanyia marekebisho na muswada umekuja kwa ajili ya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanalalamika kuhusu *chapters* kupewa nguvu na zenyeweziwe *active* kuweza kuisaidia *TLS* kufanya kazi *zonal wise,* hili haliletwi na haya ni malalamiko ya *TLS.* Sasa unajiuliza haya mabadiliko yanayokuja kufanywa yanakuja kufanywa kwa ajili ya akina nani? Lakini mmegusa marekebisho wa muundo wa bodi, mnaacha pia kufanya marekebisho ya *functions* za bodi ambazo zina muingiliano mkubwa na *functions* za *secretariat* za *TLS.* Sasa kama kweli azma ya Serikali ni kuleta marekebisho

kwa ajili ya kuboresha sheria kwanini mnadonyoa donyoa? Kwa nini hamleti marekebishao ambayo yatakamilisha marekebisho makubwa ili *TLS* waweze kufanya kazi yao kwa umakini. Sasa tunaleta sheria kwa ajili ya kuwalenga watu, hapa hatulisaidii Taifa na ukisoma haya marekebisho, moja kwa moja utaona kwamba lengo la Serikali sio kutaka kuwaondoa wanasiasa katika nafasi za uongozi, lakini lengo lao ni kuhakikisha kwamba *TLS* inakuwa ndani ya mkono wa Serikali. Sasa hatuwezi kwenda namna hii na ndiyo maana unaona kwenye *amendment* hii hii iliyoletwa hapa huku ya *TLS* unaambiwa mwanasiasa asiwe kiongozi wa *TLS,* lakini sheria nyingine hapa inamtaka tena mwanasiasa amteue Wasii Mkuu; Wasii Mkuu ndiyo anasimamia Bodi za Vyama vya Siasa. Yeye anateuliwa na mwanasiasa, unategemea afanye haki? Kama kule *TLS* umeona hii haki inakosekana, huku inapatikanaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kesi Mahakamani, iko kesi ya madai namba 13 ya mwaka 2017 ya Ally Saleh *Vs* Vita na *AG* yuko miongoni mwa washtakiwa hiyo kesi, anafahamu. Yanayodaiwa humo ni hizo hizo *influence* za kisiasa kuvivuruga vyama vingine. *(Makofi)*

Sasa kwa nini tunaliona hili kule tu *TLS?* Lakini kama kweli Serikali imefika mahali pa kutambua kwamba kada wa chama fulani anaweza asitende haki kwa watu wengine kwa nini basi hamlet muswada wa ku-*amend* Tume ya Uchaguzi, haya si yako na si mnafahamu kwamba *returning officers* wote ni makada wa Chama cha Mapinduzi na haya malalamiko ya Watanzania kuporwa haki zao kwenye chaguzi sio ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kabudi umekusanya maoni ya Katiba Mpya unafahamu kilio hiki kilivyokuwa kikubwa, leo umepewa fursa kama Waziri, leta muswada sasa tubadilishe tuwe na Tume Huru Uchaguzi kwa sababu wale wanasiasa ambao ndiyo wanatangaza matokeo kwenye chaguzi ni makada wa CCM, tunacheza nao mechi moja, refa wa kwenu na ninyi mko humo humo, mnaachaje kushinda? Kwa CCM wao ni rahisi tu ni

kujidondosha tu eneo la *penalty* mnapata *penalty* kwa sababu refa wa kwenu. *(Makofi)*

Sasa hatuwezi kwenda namna hii na mkumbuke yanapoporwa matokeo ya uchaguzi hamtupori wagombea, mnawapora wananchi na sisi kama vyama vya upinzani kwa muda mrefu tumekuwa tukifanya kazi ya kuwazuia wananchi wanapoporwa kutochukua hatua mikononi. Sasa itafika mahali na sisi tutachola kuwazuia, hatutawatuma wachukue hatua mikononi lakini tutachoka kuwazuia wasichukue hatua na hili litakuwa baya kwa sababu na wao watafika mahali watachoka huku kudhulumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kabla Taifa halijaingia huko kubaya tumieni fursa ya kufanya *amendment* hata kama hamtaki mchakato wa Katiba Mpya uendelee basi fanyeni *amendment* kwenye yale maeneo ya msingi ili haki iweze kutendekea. Ninyi mkimuona mtu anafanya sawa tu, hapa mnamuona Fatma Karume anafanya sawa tu inawauma! Sasa pale ambapo mnapendelewa ninyi sisi mnafikiri inatuuma kwa kiasi gani? Sasa na sisi wote tuko kwenye nchi yetu hii tunahitaji usawa. *(Makofi)*

Kwa hiyo tuitumie fursa ya kufanya hizi *amendment* kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa na sio kuwashughulikia watu kwa sbabu haya mabadiliko ukiyasoma tu unaona kabisa hapa yaani unapata picha ya Tundu Lissu, unapata picha ya Fatma Karume. Fatma Karume sio mwanachama wa chama chochote pengine lakini kwa sbaabu tu anasimama kwenye anayoyaamini kwenu inakuwa tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matumizi mabaya ya Bunge lako, haya ni matumizi mabaya ya fursa ya kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linazungumzwa hapa suala la kumpa nguvu Mwendesha Mashtaka ya kukamata mali. Ukisoma marekebisho hayo unashindwa kutofautisha nani mwenye jukumu la kuhukumu sasa, kwa sababu hapa

unapofunga akaunti ya mtu kwa sababu tu unamtuhumu, hivi hii sio adhabu? Si tayari umeshaanza kumuadhibu? Yaani mtuhumiwa sasa anaanza kuadhibiwa kabla Mahakama haijamuadhibu. Hili haliwezi kuwa sawa! Tunaliangalia ndiyo tunarudi pale pale kwamba tunatunga sheria kwa kuwaangalia watu namna gani tutawakomesha badala ya kuangalia sheria hii italinufaisha vipi Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kuhukumu ni la Mahakama, kutuhumiwa mtu yeyote anaweza kutuhumiwa. Leo una-*freeze* akaunti, akaunti ya mtu ukiifungia kumuathiri yeye tu uliyemlenga kuna watu wanakwen da shule wanalipiwa ada, kuna watu wanalipwa mishahara, wewe unaifunga, unawaathiri watu wengi kisa tu unamtuhumu na watu tunatuhumiana kisiasa hapa, watu wangapi wako magerezani, watu wangapi wana kesi hapa za kubambikiwa, leo una-*freeze* akaunti zao, mbona tunataka tupeane *pressure* tu bure. Hebu tutunge sheria kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi. Tuache kuwalenga watu halafu ndiyo tunakuja kufanya *amendment. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi tawala zinapita, leo tupo kwenye hii Awamu ya Tano, itakuwa Awamu ya Sita. Sio kila anayekuja atakuwa na mtazamo ule ule. Tutakuwa tuna kazi ya kuzipa viraka vya sheria kila mwaka kila tunapobadilisha viongozi. Hili sio jambo jema kwa Taifa ambalo linataka kwenda mbele hasa linalotaka kuweka misingi ya kisheria na utawala bora inafanya mabadiliko kwa ajili ya maslahi mapana ya wananchi na sio kwa ajili ya kuwalenga watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtolea. Sasa namkaribisha mtoa hoja aweze kuhitimisha hoja yake tunaanza na *AG.* Karibu Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya

kuanza kuhitimisha hoja iliyoko mbele yetu kuhusu Muswada Namba Mbili wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaelekeza hoja zangu kwa hoja zilizotolewa na wachangiaji kadhaa hapa nikianza na maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani na hasa wasiwasi aliouonesha kuhusiana na suala la mamlaka ya Rais ya kutunga sheria na kwamba angependa kuona kwamba kila sheria itungwe na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda kusema kwamba masuala ya sheria kama wanavyofahamu wanasheria mbalimbali yanaongozwa pia na kitu kinaitwa nadharia ya sheria *(legal theory). Legal theory* unaweza ukaisema ni kama *manual* unayohitaji unapohitaji kutumia kitu kama gari au mashine au kitu chochote. *Legal theory,*inakuongoza. Katika masuala ya utungaji washeria, nadharia ya sheria au *legal theory* inatuambia ziko namna nne zinazosababisha kutengeneza sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya kwanza ni kwa kutumia Bunge na hii ndiyo wengi tunaifahamu na tumeizoea, lakini pia iko namna ya pili utengenezaji wa sheria kwa *codification,* kwa bahati mbaya sina neno kwa haraka la Kiswahili linaloweza kutafsiri hapa kwa haraka. Nikueleze tu watu wengi hawafahamu kwamba katika sheria zetu tuna sheria zinaitwa *codes* hazikutungwa na Bunge kuanzia mwanzo ingawa baadae Bunge lilifanya kazi ya kufanya marekebisho au kuweka nyongeza. Mojawapo ikiwa ni *Penal Code,* wengi hatujui kwamba haikutokana na Sheria ya Bunge,*Civil Procedure Code,* haikutokana na sheria ya Bunge, hizi zilitengenezwa kwa mfumo wa *codification.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya tatu ni sheria zinazotokana na maamuzi ya Mahakama *(court decisions)* wanasheria wanafahamu *by way of precedence.* Aina ya nne ni kutengeneza sheria inaitwa *Legislation by Rex* yaani mtawala mwenye mamlaka anakuwa anapewa nafasi pia ya kutengeneza sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria zetu ukienda katika Katiba, Ibara ile ya 36(1) inagusia mamlaka ya Rais ya kutengeneza sheria, lakini pia tuna sheria inayoitwa *Presidential Affairs Act* ambayo pia inampa nguvu Mheshimiwa Rais kuweza kutengeneza sheria na anaweza akatoa *decrees, orders* na *proclamations.* Hizi sheria zinazozungumzwa ambazo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakichangia zilitengenezwa kwa mtindo wa *orders. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka nikuhakikishie kwamba hapa hakuna Katiba iliyovunjwa, hakuna utaratibu uliovunjwa, Mheshimiwa Rais ana mamlaka haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze kwa ufupi kwenye hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Salome. Kuna hoja tatu ambazo zinahitaji kuzieleza kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ni suala la viongozi wa *TLS* wasiwe wanasiasa. Wachangiaji hawaelezi kwamba katika zile *qualifications* kuna *qualifications* zaidi ya wanasiasa, wasiwe watumishi na kadhalika na nyingine hazikuzungumziwa, imezungumziwa tu ya wasiwe wanasiasa, lakini hii ni sheria ya aina gani? hii ni sheria inayozuia *conflict of interest* na tuna sheria nyingi sana katika nchi hii zinazozuia *conflict of interest* na ni sheria za kawaida. Sasa hata ukienda kwenye kanuni ambazo Mheshimiwa Jaji Mkuu alizozitoa kwa ajili ya Mawakili zinaitwa *Professional Ethics and Etiquette Regulations* amezungumzia pia kuzuia *conflict of interest.* Wakili asiingie katika jambo ambalo ana *conflict of interest,* lakini ziko sehemu nyingi sana na Waheshimiwa Wabunge wanafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba *Administrator General* asiteuliwe na Rais na ni vyema ateuliwe na Waziri. Ni maoni lakini nataka kurudia tu kwamba Mawaziri wote kama alivyozungumza Mheshimiwa Jenista Mhagama wanateuliwa na Rais na wanatekeleza madaraka yao kwa niaba ya Rais. Sasa Rais anawateua Mawaziri na Waziri ndiyo

alikuwa anamteua *Administrator General,* hapa sasa inataka kusemwa Rais mwenyewe amteue *Administrator General.* Hata akiteuliwa na Waziri bado *indirectly* ameteuliwa na Rais kwa sababu Waziri anatekeleza madaraka ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuna suala la mali inayohusishwa na jinai. Katika muswada huu imeeleza waziwazi kwamba suala la uuzaji wa mali hizi linahusisha mali ambazo ama zinaweza kutoroshwa au zinaweza kuharibika. Kwa hiyo, hizo ndizo zitahusika na uuzaji huo. Lakini pia katika muswada huu huu kumewekwa *safe guard* kwamba baada ya uuzaji huo fedha zitawekwa katika akaunti maalum na kwamba kitakachotokea baadae kitategemea na maelekezo ya Mahakama au itakavyokuwa vinginevyo.

Kwa hiyo, ile mali kimsingi haipotei kwa sababu fedha zitawekwa kwenye akaunti maalum lakini ndiyo utaratibu pia hata kwenye Mahakama zetu kuna mambo mengi tu yanahusisha fedha na fedha zile inaamriwa ziwekwe kwenye akaunti maalum ya Mahakama na bada ya hapo kitakachotokea itaamriwa ama arudishiwe mlalamikiwa au zitataifishwa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) ninalihoji Bunge ili tuweze kuongeza nusu saa tumalizie shughuli yetu.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono tunaendelea kwa nusu saa. Namkaribisha mtoa hoja sasa amalizie hoja yake.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi na Bunge lako tukufu kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yaani *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2), Bill, 2018.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuongoza mjadala wa muswada huu kwa umahiri na kwa msingi huo maoni na michango iliyotolewa yameiwezesha Serikali kuboresha maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria chini ya Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mbunge) kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kuujadili muswada huu. Maoni na ushauri waliotupatia Kamati baada ya kusikiliza maoni ya wadau yalitusaidia kuboresha maudhui ya muswada huu kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Bunge lako litaona Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Kamati ambayo ilifanya kazi ya kuchambua muswada huu kwa niaba ya Bunge hili imekubaliana na mapendekezo ya Serikali katika sehemu zote za muswada na imetoa maoni ya kuhusu namna bora ya kutekeleza masharti yanayopendekezwa katika muswada huu. Naishukuru sana Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia Mheshimiwa Ally Saleh (Mbunge) ambaye aitoa maoni kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye Wizara ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu kwa ushirikiano waliotuonesha mimi pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa maandalizi na majadiliano ya muswada

huu katika hatua zote. Pia nawashukuru watendaji wa Wizara walioshiriki kwenye hatua za maandalizi na majadiliano ya muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wa muswada huu jumla ya Wabunge watano wamechangia muswada huu. Kwa namna ya pekee niwashukuru Wabunge waliochangia kwa kuongea na wale waliochangia kwa njia ya maandishi ingawa sijayapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri waliyoitoa wakati wa majadiliano kwenye Kamati na hapa Bungeni. Tumepokea maoni mazuri ambayo yamelenga kuboresha muswada huu kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia muswada hii ni shahidi kwamba Bunge hili linatambua umuhimu wa mapendekezo ya kurekebisha sheria hizi na leo nawashukuru sana kwa kuuchangia muswada huu kwa ustaarabu bila kubagazana sana wala kuzodoana. *(Makofi)*

Katika michango yao Wabunge wametoa hoja mbalimbali ambazo ningependa kuzitolea ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kueleza kwamba Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaani *Solicitor General* sio ofisi mpya kwa maana ya kuwepo, ofisi hii ilikuwepo mpaka mwaka 1965 ambapo Bunge hili kwa Sheria ya *The Solicitor General, Transfer of Duties and Powers Act of 1965, Act No.11 of 1966* Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alihamisha, hakufuta, alihamisha shughuli na mamlaka ya *Solicitor General* kwenda kwa *Attorney General* na sheria hiyo ingawa ilichapwa mwaka 1966 lakini kwa mujibu wa kifungu cha kwanza ili *apply retrospectively* ilitoka Oktoba, 1965.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba *Solicitor General* wa mwisho kwa *title* hiyo alikuwa ni Mheshimiwa Mark Bomani na mwaka huo

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Mheshimiwa Mark Bomani kuwa ndiyo Mwanasheria Mkuu wa kwanza wa Serikali Mtanzania na kwa maana hiyo aliona huyo huyo aliyekuwa *Solicitor General* mamlaka yake yawe *transferred* kwake anapokuwa *Attorney General.* Lakini kumsaidia kufanya kazi vizuri, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wakati huo alimpa *Attorney General* ma-*assistant General* watatu ambao pia ningependa Bunge lako Tukufu na wananchi wa Tanzania wafahamu. Alimteua Bob Makani kuwa *Assistant Attorney General,* pamoja na Arnold Kileo pamoja na Joseph Sinde Warioba kwa hiyo mamlaka ya *Solicitor General* yalikuwa *transferred* na sasa imependeza wakati huu na imempendeza Rais madaraka hayo yaliyokuwa yamehamishiwa kwa *Attorney General* sasa yarudi kwa *Solicitor General* mwenyewe. Kwa rejea, nendeni tena msome *Act No. 11 of 1966* ndiyo mtajua kwamba ofisi hii sio mpya, ilikuwepo ila mamlaka yalihamishwa na sababu ya wakati huo kumpa Bomani mamlaka hayo yote ilikuwa ni idadi ndogo ya wanasheria wa Tanganyika waliokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusisahau kwamba miaka hiyo hapakuwa na wanasheria wengi wa Tanganyika. Wanasheria wa kwanza wa Tanganyika waliorudi Tanganyika baada ya kusoma sheria Uingereza wa kwanza alikuwa Mkondya mwaka 1962, wa pili alikuwa Juma Mawalla mwaka 1962, wa tatu alikuwa Mark Bomani mwaka 1963 na ndiyo maana Serikali ya Jamhuri ya Tanganyika wakati huo ilichukua hatua ya kuwachukua wanafunzi wake wafuatao ambao walikuwa wamemaliza *degree* zao Makerere ili waende kusoma sheria kuongeza idadi ya wanasheria. Sasa idadi ya wanasheria imeongezeka, mashauri yameongezeka, kwa hiyo, imeonekana ni vyema tena kuirejesha ofisi ya *Solicitor General. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uteuzi wa *Administrator General,* imeelezwa vizuri maoni ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ambaye kwa mila na desturi ninatakiwa kumheshimu. Mama yangu na baba zake ni mabinamu kabisa wa damu, kwa hiyo, nitakuwa na staha kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu kama yale aliyoyaeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba uteuzi na kama alivyoeleza Mbunge kwamba uteuzi wa *Administrator General* na majukumu anayoyafanya haikuwa sahihi kuwekwa chini ya Waziri. Ana sifa ya kuwa Jaji wa Mahakama Kuu kama alivyo *Director of Public Prosecution.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwakumbushe wanasheria wote, mamlaka yoyote inapokwenda nje ya mamlaka iliyopewa Mahakama zina uwezo wa kufanya marekebisho kwa rejea. Tusome kesi ya *Patman Garments Industries Limited versus Tanzania Manufactures Limited* ambayo ni 1981, *Tanzania Law Reports* kesi Namba 303, uamuzi wa Mwakasendo, *Justice of Appeal.* Tusome uamuzi wa Kisanga *Justice of Appeal* kwenye kesi ya *Kukutia Ole – Pumbuni versus Attorney General, 1993 Tanzania Law Reports, Case Number 159,* lakini pia tusome kesi ya *Mohamed Nyaikoze versus Sophia Mussa* ya mwaka 1971 ambayo iko kwenye *1971 High Court Digest Number 413***,** utaona iko *very clear* mamlaka yoyote hayatakiwi kutumikiwa *arbitralily* au *unpropotional,* lakini pia msome kesi ya *Christopher Mbote Nyirabu versus Methusela Paulo Nyagaswa* iliyoamuliwa pia na *Court of Appeal.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkizisoma zote hizo na hasa wanasheria, mnapokuja kuchangia hapa msiache kusoma hizo kesi. Wasiokuwa wanasheria nawasamehe, lakini ambao ni wanasheria kama akina Mheshimiwa Mtolea turejee kwenye hiyo ili tuwasaidie wasiokuwa wanasheria kuelewa vizuri tafsiri ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la *Tanganyika Law Society* pia limeelezwa vizuri na baadhi ya wasemaji. Ningependa nieleze tu sheria hiyo sio *ad hominem,* hatuleti hapa sheria ambayo ni *ad hominem* na wala haimlengi mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa niwakumbushe Watanzania, Sheria ya *Tanganyika Law Society* ilitungwa wakati wa ukoloni na baadae kufanyiwa marekebisho. *Tanganyika Law Socoety is a statutory body, is*

*not association or society made under The Societies' Act* na inagusa taaluma ambayo ni vizuri ikasimamiwa kwa umakini kuliko taaluma nyingine yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *lawyers are maidens of justice, are the dispenses of justice* na ndio maana *standards* zinazowatawala wanasheria daima lazima ziwe juu kuliko watu wengine wote. Kwa hiyo, niwashukuru wale ambao wameeleza suala hilo kwa umakini na ni kweli kabisa Serikali inatambua upungufu uliopo katika Sheria ya Chama cha Wanasheria wa Tanganyika, hivyo Serikali inaona kuna haja na umuhimu wa kufanya mashauriano ya kina na chama hicho kutokana na kuacha misingi ya kuanzishwa kwake na kujihusisha na mambo yasiyohusika na kuanzishwa kwake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha.

Moja ambalo ningependa pia kulizungumzia ni Mamlaka ya *DPP* ambalo nalo pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelieleza vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo niwashukuru tena Wabunge wote waliochangia muswada huu kwa umahiri wao, kwa umakini wao, lakini pia kwa kuchangia kwa namna ambao inastahili muswada wa namna hii kuchangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana. Asante kwa kuhitimisha hoja yako.

Katibu tuendeelee.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Bunge Zima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2018 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No. 2) Bill, 2018)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:** ...Namba 2 wa mwaka 2018. Ukurasa wa tano...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu, Kanuni ya 88(10), lakini vilevile na Kanuni ya 77(1), (2), (3), (4) na (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo unaona na ukitaka nirejee kifungu ninaweza nikarejea ama nikazungumza kwa *summary,* kwa kadri utakavyoniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeingia kwenye Kamati ya Bunge tunaelekea kufanya maamuzi ya kupitisha kifungu kwa kifungu na hatimaye kupitisha sheria hii au mabadiliko haya ya sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukirejea Kanuni ya Uhalali wa Shughuli za Bunge, sehemu ya saba, nasoma kama ifuatavyo; "Akidi kwa kila Kikao cha Bunge wakati wa kufanya maamuzi itakuwa ni nusu ya Wabunge wote, kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 94 ya Katiba, isipokuwa kwamba idadi hiyo haitahusu hoja kuhusu uamuzi wa kubadilisha masharti yoyote ya Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 98 ya Katiba."

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba (2) inasema; "Mbunge yeyote aliyehudhuria anaweza kumjulisha Spika kwamba, Wabunge waliopo ni pungufu ya akidi inayohitajika kwa ajili ya shughuli inayoendelea." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na (3) inasema; "Endapo Spika ataridhika kwamba, ni kweli idadi ya Wabunge walio ndani ya Ukumbi wa Bunge ni pungufu ya akidi inayohitajika, basi atasimamisha shughuli za Bunge kwa muda atakaoutaja na atamuagiza Katibu kupiga kengele."

Mheshimiwa Mwenyekiti, (4); "Bunge litakaporudia baada ya wakati uliotajwa kukamilika Spika atahakikisha kama idadi ya Wabunge waliopo kama inafika akidi inayohitajika, ili kuruhusu uamuzi kufanyika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ambavyo nimesema (5), nimalizie; "Endapo Spika, ataridhika kwamba, bado idadi ya Wabunge waliomo ndani ya Ukumbi wa Bunge haifiki akidi inayohitajika, basi ataahirisha shughuli za Bunge hadi muda mwingine atakaoutaja." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndio kama hivi unavyoona hapa, sihitaji kutumia nguvu nyingi sana kukushawishi. Hili Bunge lina Wabunge 393 na nusu ya akidi ni

193 kwa makadirio ya chini na sasa hivi tunaelekea kufanya uamuzi na tuko 67...*(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mmeshahesabu?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshahesabu. Kwa hiyo, tunaomba kwa sababu kanuni inakuruhusu kupiga kengele, tupige kengele hapa tusubiri kama watu wako huko nje waje. Na ikishindikana...

**MHE. MBUNGE FULANI:** Wako msikitini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** ... basi itabidi tuahirishe...

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa Halima, umeeleweka; kwa vile sasahivi hatupitishi maamuzi, bado kulihoji Bunge tuendelee halafu watakapoingia tutaangalia wakati huo wako wangapi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kwa kifungu ni maamuzi.

**MWENYEKITI:** Tutakapolihoji Bunge ndio maamuzi ya Bunge ndio inatakiwa akidi ya Bunge, sasa hivi tuko kwenye Kamati tunaendelea mpaka hapo tutakapoanza maamuzi, watakapokuwa hawajatimia tutaamua la kufanya. Tuendelee.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:** Ukurasa wa tano.

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 7
Ibara ya 8

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

*(Ibara Iliyotajwa Hapo Juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 42
Ibara ya 43

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 44

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55

Ibara ya 56
Ibara ya 57

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 58

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 66

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 72

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75
Ibara ya 76
Ibara ya 77
Ibara ya 78

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 79

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 80
Ibara ya 81
Ibara ya 82
Ibara ya 83
Ibara ya 84
Ibara ya 85
Ibara ya 86
Ibara ya 87
Ibara ya 88
Ibara ya 89
Ibara ya 90
Ibara ya 91
Ibara ya 92
Ibara ya 93
Ibara ya 94
Ibara ya 95
Ibara ya 96
Ibara ya 97
Ibara ya 98
Ibara ya 99
Ibara ya 100
Ibara ya 101
Ibara ya 102
Ibara ya 103
Ibara ya 104

Ibara ya 105
Ibara ya 106
Ibara ya 107
Ibara ya 108

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa Taarifa.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru tena. Nilisoma vifungu vyote kwa mantiki ya kwamba uhalali wa shughuli, ukanielekeza kwamba tumalize kifungu kwa kifungu tukifika kwenye kufanya uamuzi ndio tutafanya yale maelekezo ya kikanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa ninaomba Kiti chako kwa kutumia Kanuni ya 77 utoe maelekezo kengele ipigwe, Kanuni ya 77(3), ili waliokuwa nje waje, lakini vilevile utoe maelekezo kwa makatibu watuhesabu, ili kwa kumbukumbu za Bunge ijulikane wangapi. Kisha maelekezo ya Kikanuni yafuatwe kama kawaida na nusu saa inaisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima umeshaeleweka. Ninamkaribisha Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante...

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Waziri, hapo hapo unaweza kusubiri. Mheshimiwa Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mhshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sambamba kama utaridhia analolizungumza Mheshimiwa Halima, mimi ningependa kuongezea kwamba kwanza leo ni siku takatifu ya Ijumaa kuna wadau wameenda kuswali, lakini vilevile kuna uwezekano kuna wale ambao wanakuwa ni wazembe wa kuhudhuria Bungeni.

Kwa hiyo, endapo utaridhia kwamba, ikihesabika ikaonekana pengine hatutaweza kutosha, ukiwatoa wale walioenda msikitini na walioomba udhuru, basi waliobaki wote itabidi wakatwe posho ya siku ya leo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Manyanya.

Mheshimiwa Waziri, karibu.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Akidi hamna.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sware naomba usubiri, Mheshimiwa muache atoe hoja yake halafu tutawaita kwanza. Waheshimiwa subirini basi tufanye kwa utaratibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Atatuhoji ngoja, atatuhoji.

**MWENYEKITI:** Tutapiga kengele, tutawaita.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima utaratibu ufuatwe.

**MWENYEKITI:** Sawa, nimefahamu.

Mheshimiwa Waziri endelea, baadae *Sergeant-At-Arms* atapiga kengele.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments Bill (No. 2), 2018),* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa mwaka 2018 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments Bill (No. 2), 2018)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono. Sasa naagiza *Sergeant-At-Arms* apige kengele kwa dakika tatu waweze kuingia ndani ambao wako nje ya jengo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge waingie ndani ya ukumbi wa Bunge)*

**MWENYEKITI:** Basi muwe wastahimilivu kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, dakika tatu zimeisha, lakini naona kama wametimia au vipi? Ahsante. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile kazi zote kwa siku hii tumekamilisha imebaki kulihoji Bunge, naahirisha shughuli

zote za Bunge hadi Jumatatu, tarehe 10 Septemba, saa 3:00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7:23 mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu Tarehe 10 Septemba, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*